

**MITINDO MAMBOLEO YA UBAADAUSASA KATIKA NYIMBO TEULE ZA  
JAMII YA KIKALENJIN ZA KARNE YA ISHIRINI NA MOJA**

**NA**

**KIMUGUNG K. SYLVESTER**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI YA  
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII**

**CHUO KIKUU CHA MOI ELDORET, KENYA**

**2015**

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa ili kutosheleza mahitaji ya digrii katika chuo kikuu chochote. Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna ruhusa ya kutolesha sehemu yoyote bila idhini yangu na ya chuo kikuu cha Moi.

.....  
Kimugung K. Sylvester

.....  
Tarehe

SASS/PGK/05/12

Tasnifu hii imetahiniwa na kuidhinishwa na sisi tukiwa wasimamizi kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Moi.

.....  
Prof. Issa Y. Mwamzandi

.....  
Tarehe

IDARA YA SANAA NA ELIMU,  
CHUO KIKUU CHA KABIANGA,  
S.L.P 2030-20200,  
KERICHO-KENYA.

.....  
Dkt. Mosol Kandagor,

.....  
Tarehe

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA,  
CHUO KIKUU CHA MOI,  
S.L.P. 3900-30900,  
ELDORET-KENYA.

**TABARUKU**

Kwa mamangu mpendwa;

Veronica Kabon Kimugung

Aliyenipenda tangu utotoni mwangu

Na babangu;

Kimugung Toroitich

Aliyenifunza kuwajibika maishani mwangu

**ABSTRACT**

This study examined postmodernist styles in selected Kalenjin songs of 21<sup>st</sup> century. The research was conceived against the backdrop of a tendency that breaks away from the conventional Kalenjin songs. The selected songs at a glance would appear to be fragmented with no specific theme being addressed therein. In order to achieve the objective of the research, twenty four songs were chosen from the five Kalenjin sub-tribes, namely, Kipsigis, Nandi, Keiyo, Marakwet and Tugen. We hypothesized that the selected songs depicted postmodern styles and tendencies as a strategy to communicate the realm of the Kalenjin world as perceived by its subjects. The study enlisted the postmodern theory which contends that the attempt to explain social and cultural developments by means of a single account or a major narrative is no longer possible or acceptable and that ideas cannot express a historical reality. Instead everything is text, image and simulation. Data was sampled purposely using the two approaches: songs which were sung in the 21<sup>st</sup> century until August 2014 and those that exhibited postmodernist tendencies. Data was collected via transcription of recorded songs, confirmed by a native speaker to ascertain their accuracy and then translated to Kiswahili. The data was qualitatively analyzed using the tenets of postmodernism theory and presented in prose form. The study found out that, the postmodern styles that defined the selected Kalenjin songs of the 21<sup>st</sup> century are mini-narratives that are highly fragmented, intertextual and replete with pastiche. The used of mini-narratives in selected the Kalenjin songs texts served to counter established authoritative beliefs in religion, human institutions, education and political ideologies which oppress the masses. Fragmentation in the selected song texts were shown to be the preferred mode of presentation as the song texts relied on situational narratives as opposed to the grand narratives that found favoured with Aristotle and Plato. The study also found out that the selected song texts

are highly intertextual as they cite other texts like Kalenjin oral narratives, proverbs, similes, Biblical texts and Kenyan Constitution to buttress their messages. Lastly the used of pastiche was portrayed when specific Kalenjin song texts appropriated other Kalenjin song texts. This was mainly seen by use of similar words, statements and lines in the selected songs. Pastiche was also depicted when songs used same plot, flash back and a common technique where artists send greetings to specific fans. From these findings we concluded that the postmodern styles were of great importance in depicting postmodern tendencies in Kalenjin oral literature. The study makes a contribution to scholarship through the understanding of the postmodern styles used in Kalenjin songs and usage of Kiswahili language to explain them. Furthermore, the styles in the songs are identified and explained in detail hence creating an invaluable record for future reference.

## **IKISIRI**

Utafiti huu unatalii mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo teule za Kikalenjin za Karne ya Ishirini na Moja. Utafiti uliibuliwa kutokana na nyimbo za Kikalenjin za Karne ya Ishirini na Moja zilizozuka na kukaidi kaida za jadi zilizozoeleka. Nyimbo zilizoteuliwa zinaonekana kama vijihadithi visivyomuwala na kutokuwa na maudhui mahususi. Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, nyimbo ishirini na nne ziliteuliwa kutoka lahaja zifuatazo za Kikalenjin: Kikipsigis, Kitugen, Kinandi, Kimarakwet na Kikeiyo. Nadharia tete ya utafiti ni kuwa nyimbo za Kikalenjin za Karne ya Ishirini na Moja zinadhihirisha mitindo ya ubaadausasa ili kuakisi hali halisi ya jamii ya Kikalenjin kama inavyofasiriwa na wenyeji. Utafiti huu unatumia nadharia ya ubaadausasa inayopinga dhana ya kuelezea maendeleo ya jamii kwa kutumia mtazamo moja au simulizi kuu. Nadharia hii inasema kuwa simulizi kuu haikubaliki tena katika dunia ya kisasa. Aidha, mawazo hayawezi kuyasimamia historia halisi na ishara haziwakilishi hali halisi. Usampuli wa kimaksudi ulitumiwa kupata data zilizochambuliwa kwa kutumia mikakati miwili: nyimbo zilizoimbwa baada ya Karne ya Ishirini na Moja hadi Agosti 2014 na zilizodhihirisha mitindo ya ubaadausasa. Data zilikusanywa kupitia unukuzi wa nyimbo zilizorekodiwa, kuthibitishwa na wazungumzaji asilia kuhakikisha kwamba ujumbe wa lugha asilia umehifadhiwa na kisha kutafsiriwa hadi lugha ya Kiswahili. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya ubaadausasa na kasha kuwasilishwa kwa njia ya kimaandishi na kinathari. Utafiti huu uligundua kwamba mitindo ya ubaadausasa iliyojitokeza katika nyimbo za Kikalenjin za Karne ya Ishirini na Moja ni simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi. Matumizi ya simulizi ndogo ndogo ilijitokeza kupitia upingaji wa mamlaka yaliyokuwa yamezoeleka katika jamii. Mamlaka hayo ni dini, taasisi za binadamu, elimu na kaida za kisiasa. Ilibainika kuwa mamlaka hayo ni kandamifu kwa maisha ya binadamu na hivyo basi nyimbo hizi kuyapinga. Matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi ilibainika pale matini ya nyimbo za Kikalenjin zilivyovunjwavunjwa na

zizizomuwala. Hivyo basi kuakisi hali halisi ya dunia ya kisasa. Hii ni tofauti na mapendekezo ya akina Aristotle na Plato kuwa fasihi lazima iwe na mshikamano na muwala. Matumizi ya mwingiliano matini ilibainika pale nyimbo teule za Kikalenjin ziliporejelea kazi za awali kujenga maudhui yao. Katika utafiti huu tuligundua kuwa nyimbo teule zilirejelea simulizi za jadi za Kikalenjin, methali, tasbihi, matini ya Bibilia na Katiba ya Kenya. Hatimaye matumizi ya mtindo wa uigaji wa vipande vya simulizi ilibainika pale matini ya nyimbo teule za Kikalenjin zinapoigana. Mtindo huu unaonekana katika matumizi ya maneno na mistari sawa na nyimbo teule. Vilevile mtindo wa uigaji wa vipande vya simulizi ulionekana pale nyimbo zilipotumia ploti, mtindo wa kisengere nyuma na utumaji wa salamu kwa mashabiki uliosawa. Kutokana na matokeo haya; tulihitimisha kuwa mitindo ya ubaadausasa ni nyenzo kuu ya uwasilishwaji wa fasihi simulizi za Kikalenjin. Utafiti huu unachangia katika taaluma ya usomi kwa kueleza mitindo ya ubaadausasa iliyotumiwa katika nyimbo za Kikalenjin na pia kutumia lugha ya Kiswahili katika kueleza mitindo hiyo. Fauka ya hayo, mitindo ya ubaadausasa inabainishwa na kuelezwa kwa kina na hivyo basi kuwa hifadhi kwa siku za usoni.

## YALIYOMO

<a href="#"><u>IKIRARI</u></a> .....	
<a href="#"><u>TABARUKU</u></a> .....	
<a href="#"><u>ABSTRACT</u></a> .....	
<a href="#"><u>IKISIRI</u></a> .....	
<a href="#"><u>ORODHA YA MAJEDWALI</u></a> .....	
<a href="#"><u>ORODHA YA VIFUPISHO</u></a> .....	
<a href="#"><u>UFAFANUZI WA DHANA</u></a> .....	
<a href="#"><u>FASILI ZA ISTILAHU</u></a> .....	
<a href="#"><u>SHUKRANI</u></a> .....	
<a href="#"><u>SURA YA KWANZA</u></a> .....	
<a href="#"><u>MISINGI YA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.0 UTANGULIZI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.1 USULI WA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.2 SUALA LA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.3 MALENGO YA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.4 NADHARIA TETE</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.5 UMUHIMU WA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.6 UPEO WA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.7 MISINGI YA KINADHARIA</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI</u></a> .....	

<a href="#"><u>1.9 MBINU ZA UTAFITI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.9.0 UTEUZI WA USAMPULI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.9.1. UKUSANYAJI WA DATA</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.9.2 UCHAGUZI WA SAMPULI YA NYIMBO</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.9.3. UTAFITI WA MAKTABANI</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.9.4. VIFAA</u></a> .....	
<a href="#"><u>1.9.5. UCHANGANUZI WA DATA</u></a> .....	
<a href="#"><u>SURA YA PILI</u></a> .....	
<a href="#"><u>HISTORIA NA MITINDO YA UBAADAUSASA KATIKA KAZI ZA FASIHI</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.0 UTANGULIZI</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.1 VIPINDI MBALIMBALI VYA HISTORIA YA DUNIA HADI KUFIKIA KIPINDI CHA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.2 USULI NA CHIMBUKO LA NADHARIA YA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3 NADHARIA YA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.0 UFAFANUZI WA DHANA YA NADHARIA YA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.1. TOFAUTI BAINA YA VIPINDI VYA USASA NA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.2 WAASISI WAKUU WA NADHARIA YA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.2.0 JEAN FRANCOIS LYOTARD</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.2.1 JEAN BAUDRILLARD</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.2.2 FREDRICK JAMESON</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.3 MATUMIZI YA NADHARIA YA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.4 MITINDO YA UBAADAUSASA KATIKA KAZI ZA FASIHI</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.4.0 USULI WA KUCHIPUKA KWA MITINDO YA NADHARIA YA UBAADAUSASA</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.4.1. SIMULIZI NDOGO NDOGO</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.4.2. UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.4.3 MWINGILIANO MATINI</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.3.4.4 UIGAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI</u></a> .....	
<a href="#"><u>2.4 HITIMISHO</u></a> .....	
<a href="#"><u>SURA YA TATU</u></a> .....	
<a href="#"><u>SIMULIZI NDOGO NDOGO NA UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI KATIKA NYIMBO ZA KIKALENJIN</u></a> .....	
<a href="#"><u>3.0 UTANGULIZI</u></a> .....	
<a href="#"><u>3.1 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA SIMULIZI NDOGO NDOGO</u></a> .....	
<a href="#"><u>3.1.1 DINI</u></a> .....	

<a href="#"><u>3.1.2 TAASISI ZA BINADAMU</u></a>	.....
<a href="#"><u>3.1.3 ELIMU</u></a>	.....
<a href="#"><u>3.1.4 KAIDA ZA KISIASA</u></a>	.....
<a href="#"><u>3.2 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI</u></a>	.....
<a href="#"><u>3.3. HITIMISHO</u></a>	.....
<a href="#"><u>SURA YA NNE</u></a>	.....
<a href="#"><u>MWINGILIANO MATINI NA UIGAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI KATIKA NYIMBO ZA KIKALENJIN</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.0 UTANGULIZI</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA MWINGILIANO MATINI</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1.0 UREJELEAJI WA SIMULIZI ZA JADI ZA KIKALENJIN</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1.1 UREJELEAJI WA METHALI</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1.2 UREJELEAJI WA TASHBIHI</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1.3 UREJELEAJI WA BIBILIA TAKATIFU</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1.4 UREJELEAJI WA KATIBA YA KENYA</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.1.5 UREJELEAJI WA NYIMBO NYINGINE</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.2 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA UIGAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI</u></a>	.....
<a href="#"><u>4.3 HITIMISHO</u></a>	.....
<a href="#"><u>SURA YA TANO</u></a>	.....
<a href="#"><u>MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO</u></a>	.....
<a href="#"><u>5.0 UTANGULIZI</u></a>	.....
<a href="#"><u>5.1 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI</u></a>	.....
<a href="#"><u>5.2. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO</u></a>	.....
<a href="#"><u>5.2.1 HITIMISHO LA UTAFITI</u></a>	.....
<a href="#"><u>5.2.2 MAPENDEKEZO YA UTAFITI</u></a>	.....
<a href="#"><u>5.3. HITIMISHO LA SURA</u></a>	.....
<a href="#"><u>MAREJELEO</u></a>	.....
<a href="#"><u>KIAMBATANISHO 1</u></a>	.....

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 1: vipindi vya dunia hadi kufikia kipindi cha ubaadausasa.....	30
Jedwali 2: kuchipuka kwa mitindo ya ubaadausasa.....	46

**ORODHA YA VIFUPISHO**

K19	-Karne ya kumi na tisa
K21	- Karne ya Ishirini na Moja
K20	- Karne ya Ishirini
n.k	-na kadhalika
TY	-Tafsiri Yangu
MP	-Matini Pokezi



MA

-Matini Asilia

**UFAFANUZI WA DHANA****Mitindo mamboleo ya ubaadausasa**

Dhana hii ya mitindo mamboleo ya ubaadausasa imetumiwa kurejelea vipengele vya ubaadausasa vinavyotumiwa kuwasilisha kazi za fasihi. Vipengele hivi ni mihimili vya nadharia ya ubaadausasa.



## **FASILI ZA ISTILAHU**

Fasili hii inatokana na hali kwamba uwanja huu wa utafiti hujaandikwa sana katika lugha ya Kiswahili na hivyo baadhi ya istilahi hupewa visawe tofauti na wataalamu mbalimbali.

Fasili hii inampa fursa yeyote yule anayefahamu istilahi hizi kwa Kiingereza kuweza kuelewa visawe vya maneno hayo kama yalivyotumika katika tasnifu hii.

Jamii nzima	-	Plurality of the society
Kaida za kisiasa	-	Political ideologies
Kipindi cha Mwamko	-	Renaissance
Kipindi cha Tamaduni Simulizi	-	Oral Culture
Kipindi cha ubaadausasa	-	Postmodernism
Kipindi cha Ulimbende	-	Romanticism
Kipindi cha urazini	-	Enlightenment
Kipindi cha Usasa	-	Modernism
Kipindi cha Victoria	-	Victorian period
Kuvunjikavunjika tamaduni	-	Cultural fragmentation
Maisha yasiyoendeshwa kwa kutegemea dini	-	Secularization
Mitindo ya ubaadausasa	-	postmodern styles
Mradi wa mwamko	-	Enlightenment goals
Mwingiliano matini/wingimatini	-	Intertextuality
Sanaa kwa ajili ya sanaa	-	Arts for arts sake
Simulizi kubwa/kuu	-	Grand narratives
Simulizi ndogo ndogo	-	Minni-narratives
Taasisi za binadamu	-	Human institutions
Tamaduni kongwe	-	Traditional culture
Tofauti za kitamaduni	-	Cultural differentiation
Ubunaji wa visaasili	-	Myth creation
Uchopekaji wa vipande vya simulizi	-	Fragmentation
Uchunguzi kifani	-	Case by case method

Uhalisia wa kimaajabu	-	Magical realism
Uigaji wa vipande vya simulizi	-	Pastiche
Ukuaji wa miji	-	Urbanization.
Ukuaji wa viwanda	-	Industrialization
Upagani	-	Paganism
Upingaji wa Kaida	-	Antifoundational
Upanuaji wa soko	-	Market liberalism
Urasimu	-	Bureaucratization
Urazini	-	Rationalization

## **SHUKRANI**

Kukamilika kwa tasnifu hakungewezekana bila ushirika, mawaidha na msaada niliopokea kwa watu mbalimbali. Ninawajibika kuwatolea shukrani watu hao wote kwa msaada wao. Mwanzo namshukuru Maulana kwa kunipa nguvu na siha njema wakati wote nilipokuwa nikifanya utafiti huu.

Shukrani za kipekee ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Issa Y. Mwamzandi na Dkt. Mosol Kandagor ambao kila mara walinitia motisha ya kuzingatia utafiti kwa dhati. Sina maneno ya kuelezea mchango wao na wema walionionyesha nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Nawashukuru sana kwa kazi ya sulubu mlionifanyia licha ya nyie kuwa na kazi nyingi. Nina deni kubwa kwa wazamili wenzangu Omari Nyamweya, Tecla Muge, Risper Okemwa, Muli Margaret Kamene, Biwott Bittok, Kemei Marlon, Mwati Michael, Machanga Elphas, Marceline Baya na Doris Ombati kwa msaada wao na motisha walionitia nilipokuwa katika hali ya kuvunjika moyo.

Shukrani za dhati ziwaendee wafadhili wangu walioniwezesha kukamilisha karo za shahada hii ya uzamili. Kwanza kwa dadangu Ann Kimugung, Timothy Kosgei na marehemu Barnaba Kurui (Mungu ailaze roho yako mahala pema peponi) kwa mchango mlioniandalia huko Nairobi tarehe 29/11/2012. Pili, kwa wanakamati wote mkiongozwa na Katekista Kirui, shemeji Julius na mkwe Risper kwa kuniandalia mchango mwengine uliofanyika nyumbani tarehe 09/12/2012. Hongera kwenu wote. Ni kupitia michango hiyo niliweza kufadhili masomo yangu. Mungu awabariki.

Hatimaye, kazi hii yote haingewezekana bila msaada na mapenzi ya mpenzi wangu Joyce Toroitich aliyenitia shime ya kukamilisha utafiti huu. Tasnifu hii ni kilele cha mapenzi yako, bila shaka Jalali atakutunikia kombe lako hadi lifurike.

## **SURA YA KWANZA**

### **MISINGI YA UTAFITI**

#### **1.0 UTANGULIZI**

Sura hii inaeleza usuli wa utafiti na suala la utafiti, katika maelezo hayo, tumebainisha kinaganaga pengo la kiakedemia lililojalizwa na utafiti huu. Kisha, malengo na nadharia tete ya utafiti yalitolewa, huku ukifuatwa na ufafanuzi wa umuhimu wa utafiti huu. Mipaka ya utafiti huu imefafanuliwa katika sehemu ya upeo wa utafiti kabla ya kujadiliwa kwa misingi ya nadharia ya ubaadausasa iliyoongoza utafiti huu. Aidha, mapitio ya maandishi mbalimbali pamoja na tahakiki zilizotumia nadharia ya ubaadusasa yamejadiliwa. Hatimaye, mbinu za utafiti zimejadiliwa, zikiwemo uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, vifaa vilivyotumika na uchanganuzi wa data.

#### **1.1 USULI WA UTAFITI**

Fasihi simulizi ni utanzu mmojawapo wa fasihi. Fasihi simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee wenye kutoa fursa njema ya kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia aina hii ya fasihi ni uti wa mgongo wa maendeleo ya binadamu, kwani ndani yake kuna masimulizi, maigizo, tathmini za mazingira na mahusiano ya kijamii (Kirumbi 1975, Wamitila 2008, Njogu na Chimerah 2008). Kwa hivyo fasihi simulizi ina uhusiano mkubwa na jamii, na kadri jamii inapobadilika, huathiri fasihi simulizi. Mathalan, fasihi tuliyojua katika K20 ni tofauti na fasihi ya K21. Katika fasihi za jadi kulikuwa na sifa za uwasilishwaji wa fasihi simulizi zilizokuwa zimezoeleka. Kulingana na Mrikaria (2009) sifa hizi zilianza kuchukua mkondo tofauti mwishoni mwa K20 na mwanzoni mwa K21. Hata hivyo tunapozungumzia mabadiliko hayo katika fasihi simulizi huwa haieleweki vizuri. Hii ni kwa sababu fasihi simulizi huhusishwa na jamii maalum (Ntaragwi 2004).

Ili kushadidia hoja hii Ntaragwi anamnukuu Escarpist (1974: 4) anayesema kuwa fasihi simulizi lazima ichukuliwe kama iliyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii maalumu. Anachomaanisha Escarpist ni kwamba fasihi simulizi lazima ihusiane moja kwa moja na jamii dhahiri kwa mfano jamii ya Wakalenjin, Wakikuyu, Waluhya na Wakisii. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti umejikita katika nyimbo za Kikalenjin.

Mathalan, jamii ya Wakalenjin imesheheni vijitanzu mbalimbali vya fasihi simulizi. Hii ni kutokana na mila, desturi na tamaduni zao. Kwa mujibu wa Kipkorir (1985) na Chesnai (1991) wao hudhaniwa walihama kutoka mto wa Nile kule Sudan Kusini au Uhabeshi Magharibi miaka 2,000 iliyopita. Kabila hili limeundwa na lahaja nane ambazo ni: Kikeiyo, Kimarakwet, Kikipsigis, Kinandi, Kipokot, Kitugen, Kiterik na Kisebeei. Makundi hayo huzungumza lahaja tofauti za lugha ya Kikalenjin. Hata hivyo lahaja za Kimarakwet, Kinandi, Kikeiyo, Kikipsigis na Kitugen hufanana kwa asilimia kubwa. Watu wengi wa lahaja hizo wanaishi katika Bonde la Ufa nchini Kenya. Kama jamii yoyote ya Kiafrika, Wakalenjin wana tanzu mbalimbali za fasihi simulizi inayohusishwa na simulizi za jadi, vitendawili, methali, vitanza ndimi na nyimbo.

Katika kabila hili nyimbo ziliimbwa nyakati mbalimbali kama wakati wa kucheza kwa watoto, kufanya kazi, sherehe za kuzaliwa, utoaji wa majina, tohara na arusi. Nyimbo hizi zilitumiwa kwa madhumuni mbalimbali kama vile kuhifadhi utamaduni, kuburudisha, kuelimisha kaida za jamii, kuipa jamii mwelekeo, kuunganisha vizazi vya jamii, kufundisha, kukuza ushirikiano, kuabudu muumba wao (Asis), pamoja na kuziendeleza stadi za lugha (Chesnai, 1991).

Kabla ya K21 nyimbo za Kikalenjin zilikuwa zimejengeka katika mfumo uliozoeleka wa kufikisha ujumbe kwa hadhira, mfumo uliolenga zaidi kurithisha mila, desturi na

tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hii ina maana kurithishana mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi cha kale (babu, bibi na wengineo wa umri wao) kwa kukifundisha na kukirithisha kizazi kipya (ambacho ni watoto na wajukuu wao). Katika uimbaji wa nyimbo ilikuwa ni lazima pande zote mbili ziwepo, yaani fanani (anayerithisha, msimuliaji) na hadhira (anayerithishwa, msimuliwaji). Fanani hujitahidi kutumia mbinu mbalimbali kuijenga kazi yake ili iweze kuvutia hadhira. Maneno yanayoimbwa au matini yenye mpangilio maalumu, muktadha unaofungamana na wimbo, kwa mfano sherehe, ibada, kilio, ufugaji, uwindaji ndege shambani na kuvuna, ala au vyombo vya muziki na sauti ya mwimbaji ilikuwa inafanana kuanzia mwanzo hadi mwisho (Chesanai 1991, Wamitila 2003).

Kutokana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kisayansi, kiteknolojia na kisanaa sifa hizi za nyimbo zilibadilika hasa baada ya K21. Nyimbo hizi za K21 zilikusishwa na vipengele tofauti na zile zilizozoeleka. Mitindo iliyoanza kujitokeza ama ni matumizi ya simulizi ndogo ndogo za visa visivyoana, mwingiliano matini, ukosefu wa mshikamano wa mawazo au unukuzi wa nyimbo kutoka tamaduni zingine na ufafanuzi. Zaidi ya hayo, mitindo mingine ni matumizi ya kinaya, ukosefu wa mahadhi, wizani na toni, matumizi ya ukinzani, wimbo wa wingi maana na usiofuata mfumo wowote wala toni, wimbo unaosawiri mambo kulingana na miktadha maalumu, matumizi ya teknolojia kama kurekodi na kuhifadhiwa kwenye kanda za video, kupingana kwa jozi na maana ya wimbo hutokana na wasikilizaji kuliko hata watunzi (Kramer 1996). Ni vipengele hivi vilivyojitokeza mwishoni mwa K20 na mwanzoni mwa K21 ndivyo tunavyoviita mitindo mamboleo ya ubaadausasa.



Utafiti wa mitindo mamboleo ya ubaadausasa katika nyimbo ulifanywa na Kramer (1996) aliyeonyesha mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo za Beethovens *String Quarter*, Ives *Putmans Camp* na Mahler *Seventh Symphony*. Kramer alidhihirisha mitindo ifuatayo: mwingiliano matini, unukuzi na brikolojia. Hata hivyo utafiti huu ulifanywa katika nyimbo zilizoimbwa kabla ya K21 na tena katika miktadha ya nchi za Kimagharibi.

Katika Afrika Mashariki tafiti nyingi zinazohusiana na mitindo mamboleo ya ubaadausasa zilifanywa katika nyanja ya fasihi andishi (Mwamzandi 2013; Waliaula 2010; Khamis 2008; Gromov 2008; Khamis 2007; Ritgerotil 2006; Bertoncini 2004). Tafiti zilizofanywa hadi sasa zinazohusiana na nyimbo zimeshughulikia mambo tofauti: Suriano (2007) aliangalia lugha itumiwayo katika nyimbo za *Bongo Flewa* na *Hip-Hop* na jinsi nyimbo zinavyotumiwa katika miktadha ya kisiasa. Lugha ambayo inatumiwa hasa katika nyimbo hizi ni mchanganyiko kati ya Kiswahili na Kiingereza (Swanglish). Suriano aliwanukuu (Nyairo na Ogude 2005) ambao walionyesha jinsi wimbo *Unbwogable* ulioimbwa na Gidi Gidi Maji Maji ulivyotumiwa na wanasiasa wakati wa kampeni nchini Kenya mwaka wa 2002. Wanyama (2005) aliangalia ujumi katika muziki wa tohara ya Wabukusu. Wanyama alieleza kuwa vipengele vya ujumi katika muziki wa tohara ya Wabukusu vimejifungia katika fani, maudhui na utendaji.

Utafiti uliofanywa katika nyimbo za Kikalenjin ni ule wa Simatei (2010). Simatei alidhihirisha jinsi nyimbo za Kikalenjin zinavyotumiwa kuleta umoja. Umoja huu unatokana na mila, desturi na tamaduni zilizoshabihana katika kabila la Kikalenjin. Simatei alihakiki wimbo wa Jane Kotut ulio na mada *Rift Valley*. Katika wimbo huu Simatei anabainisha jinsi Kotut anavyosema kuwa Rift Valley ni sehemu ambayo

Wakalenjin wanaishi. Mwimbaji huyu alitaja lahaja zote za Wakalenjin na kuwahimiza kushirikiana.

Kwa hivyo kutokana na fafanuzi hizo ni wazi kwamba utafiti wa mitindo ya ubaadausasa katika fasihi simulizi, hususani, nyimbo za Kikalenjin haujafanywa kwa kina. Kwa hivyo utafiti huu wa mitindo mamboleo ya ubaadausasa katika nyimbo za Kikalenjin za K21 umefanywa ili kujaza pengo la kiakedemia.

## **1.2 SUALA LA UTAFITI**

Utafiti huu uliibuliwa kutokana na nyimbo za Kikalenjin za K21 zilizozuka na kukaidi kaida za jadi zilizozoeleka. Nyimbo hizi zilionekana tofauti na za zamani kutokana na matumizi ya mitindo ya ubaadausasa. Mitindo hii ya ubaadausasa imezuka katika nyimbo hizi mwishoni mwa K20 na mwanzoni mwa K21 hasa kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisayansi, kijamii, kiteknolojia na kisanaa.

Nyimbo za Kikalenjin zilizozuka katika K21 zilionyesha upingaji wa mamlaka ya kijamii yaliyokuwa yamezoeleka. Baadhi ya mamlaka hayo ni dini, demokrasia, elimu, ndoa, taasisi za binadamu na kaida za kisiasa. Mamlaka hayo yalikuwa yanathaminiwa na jamii kuwa yangesuluhisha changamoto zilizokuwa zinakumba jamii. Lakini zilisababisha maangaiko na hata hadhi na gharama ya juu kwa maisha ya binadamu. Ni kutokana na changamoto hizi ndipo nyimbo za Kikalenjin za K21 zikaanza kushamiri na kupinga mamlaka hayo, kuchipua kipengele cha simulizi ndogo ndogo. Kwa hivyo ni katika miktadha hii ambapo tulidadisi jinsi mtindo wa simulizi ndogo ndogo unavyotumika katika nyimbo za Kikalenjin za K21 kusuluhisha changamoto hizi.

Isitoshe, nyimbo za Kikalenjin za K21 zilionyesha kuvunjwavunjwa na zisizomuwala kuanzia mwanzo hadi mwisho. Nyimbo hizi zilikaidi mapendekezo ya akina Aristotle na

Plato kuhusu utunzaji wa sanaa. Aristotlele na Plato walikuwa wamependekeza sanaa lazima iwe yenye muwala na mshikamano. Yaani sanaa lazima iwe na mwanzo, kati na mwisho. Nyimbo za Kikalenjin zilizozuka katika K21 zilikaidi kaida hii na kusawiriwa kwa kutumia vijihadithi vingi visivyooana, kuchipua kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi. Kwa hivyo katika utafiti huu tumechanganua kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21.

Fauka ya hayo, nyimbo za Kikalenjin za K21 zimeimbwa na wingi wa urejeleo matini. Urejeleo huu umefanya nyimbo za Kikalenjin kujenga ujumbe wao. Kwa hivyo katika utafiti huu tumehakiki jinsi nyimbo za Kikalenjin zinavyorejelea kazi zingine za awali.

Hatimaye nyimbo za Kikalenjin za K21 zilizozuka zilikuwa zinaonyesha mfanano kwa upande mkubwa. Hii ni tofauti na sanaa ya kipindi cha usasa iliyosisitiza sanaa kwa ajili ya sanaa. Sanaa kwa ajili ya sanaa ilikuwa inasisitiza wasanii kuwa na upekee na ubunifu wa hali ya juu, yaani sanaa iliyokuwa tofauti kabisa na yoyote nyingine. Nyimbo za Kikalenjin za K21 zilikaidi madai hayo na kuonyesha matini ya nyimbo ambayo yalikuwa yanafanana, kuchipua kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi. Utafiti huu basi ulihakiki kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21.

Utafiti huu basi umejikita katika mitindo minne ya nadharia ya ubaadausasa iliyotumika katika matini ya nyimbo za Kikalenjin za K21 ambazo ni simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi. Utafiti ulitumia nyimbo ishirini na nne kutoka lahaja tano za Kikalenjin ambazo ni Kitugen, Kinandi, Kimarkwet, Kikipsigis na Kikeiyo.

### **1.3 MALENGO YA UTAFITI**

1. Kufafanua sifa za ubaadausasa katika kazi za fasihi za kibaadausasa.
2. Kuchanganua vipengele vya simulizi ndogo ndogo na uchopekaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin.
3. Kuchanganua vipengele vya mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin.

#### **1.4 NADHARIA TETE**

1. Kazi za kifasihi za kibaadausasa zinadhihirisha sifa za ubaadausasa.
2. Nyimbo teule za Kikalenjin za K21 zimeimbwa kwa kutumia vipengele vya simulizi ndogo ndogo na uchopekaji wa vipande vya simulizi.
3. Nyimbo teule za Kikalenjin za K21 zimeimbwa kwa kutumia vipengele vya mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi.

#### **1.5 UMUHIMU WA UTAFITI**

1. Umuhimu wa utafiti huu unatokana na ukweli kwamba tafiti nyingi zimeshughulikia mitindo ya ubaadausasa katika fasihi andishi. Ni tafiti chache mno ambazo zimeshughulikia mitindo ya ubaadausasa katika fasihi simulizi. Utafiti huu hivyo basi umenuia kujaza pengo hili.
2. Kuimarisha maandishi kuhusu nyimbo za Kikalenjin za K21. Hii ni kwa sababu nyimbo nyingi za Kikalenjin hivi sasa zinapatikana katika kanda za video. Kanda hizi za video huenda zikaharibika siku za usoni. Kwa hivyo utafiti huu unaweka hifadhi ya kudumu baadhi ya nyimbo za Kikalenjin katika maandishi.
3. Kuongeza ufundi kuhusu mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo zilizoimbwa katika K21. Hivi sasa ufundi huu ni mchache na kama upo umetekelezwa katika nyimbo za Kimagharibi.

4. Utalii wa matumizi ya mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo za Kikalenjin za K21 ni utafiti mwafaka utakaosaidia kueleweka kwa maudhui mamboleo katika jamii ya kisasa.
5. Kutumia lugha ya Kiswahili katika kueleza mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo. Hatua hii imepanua matumizi ya lugha ya Kiswahili katika tafiti. Aidha, ni njia moja ya kuondoa vizingiti vinavyokumba maelezo, mawasiliano na utafiti kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Swala hili ni muhimu kwa kuwa hivi sasa Kiswahili ni lugha ya taifa na inayoenea kwa kasi katika Afrika Mashariki.

### **1.6 UPEO WA UTAFITI**

Uchunguzi huu ulihusu mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo za Kikalenjin za K21. Ingawa kuna nyimbo za makabila mengi, utafiti huu ulijihusisha na nyimbo za Kabila la Kikalenjin tu. Nyimbo hizo zilizotumika katika utafiti huu ni zile zilizodhihirisha mitindo ya ubaadausasa. Halikadhalika, nyimbo hizo ziliimbwa mwanzoni mwa K21 hadi Agosti mwaka wa 2014.

Kwa kuwa jamii ya Kikalenjin ni jumuishi ya lahaja nyingi, data za utafiti huu ulijikita katika lahaja tano ambazo ni Kikipsigis, Kinandi, Kitugen, Kimarakwet, na Kikeiyo. Lahaja hizi tano zilichaguliwa kwa sababu ya kukaribiana kwa lahaja zao (Chesaina 1991). Uchambuzi wa data hata hivyo haukuzingatia migawanyo hii ila ilitumika katika ukusanyaji wa data pekee.

Ingawa kuna nyimbo nyingi kutoka lahaja hizo utafiti huu ulichukua nyimbo ishirini na nne pekee. Hii ni kwa kuwa zilitosheleza kukidhi mahitaji ya utafiti huu. Ikumbukwe kwamba nyimbo nyingi za K21 zilidhihirisha mitindo ya ubaadasasa, na hizi zilitumiwa tu kama kielelezo cha nyimbo za Kikalenjin za K21. Aidha, lahaja zingine za Kikalenjin

ziliikuwa na nyimbo zilizoimbwa katika K21 na zilibainisha mitindo mipya ya ubaadausasa. Hata hivyo, utafiti huu haukuzishughulikia nyimbo za lahaja hizo ila tulijikita katika nyimbo ishirini na nne tulizoteuwa.

### **1.7 MISINGI YA KINADHARIA**

Utafiti huu wa ubaadausasa katika nyimbo za Kikalenjin uliongozwa na nadharia ya ubaadausasa inayohusishwa na wataalamu Jean-Francois Lyotard, Jean Baudrillard, Fredric Jameson, Michel Foucault, Jacques Derrida na Richard Rorty (Hicks 2004). Matumizi ya dhana ya ubaadausasa ulianza miaka ya 1940 kama mtindo wa usanifu wa mijengo ambao ulidhihirisha kanuni zilizoenda kinyume na usasa na urazini. Baadaye dhana hii ilihusishwa na sanaa nyingine kama nyimbo, uchoraji na fasihi. Kama anavyosema Rice na Waugh (2001) dhana hii ya ubaadausasa ilitumiwa na mwanahistoria Arnold Toynbee mnamo mwaka wa 1947 kuelezea historia ya nchi za kimagharibi zilizotawaliwa na wasiwasi na ukosefu wa mantiki. Tofauti na madai hayo Bertens (1995) anamnukuu Welsch (1987) anayeelezea kuwa dhana hii ilitumiwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1870. Kwa mujibu wa Keller na Best (1991) dhana hii ya ubaadausasa ilionekana kutumiwa katika vitabu na makala mbalimbali: mfano *Mass Culture* (1950) na mwana historia Bernard Rosenberg, *The Landmarks of Tomorrow* (1957) na mwanauchumi Peter Drucker, *The Sociological Imagination* (1959) na mwanasosiolojia C. Wright Mills, *The Revolution in Western Thought* (1961) na Huston Smith na *An Introduction to Contemporary* (1964) na Geoffrey Barraclough. Hata hivyo hakuna uhusiano mkubwa katika matumizi ya neno ubaadausasa na jinsi lilivyotumiwa katika miaka ya baadaye. Dhana hii ya ubaadausasa ilipata mwelekeo kamili ilipoanza kutumiwa katika uhakiki wa fasihi mnamo miaka ya 1950; pale Charles

Olson alipotumia kuchambua mashairi yanayoenda kinyume na usasa (Bertens, 1995). Naye Barry (2002) anaeleza kuwa neno hili hasa liliwekwa msingi imara na Jean-Francois Lyotard katika makala yake, *The Post modern Condition: A Report on Knowledge (1979)*.

Kwa mujibu wa Bertens (1995) dhana hii ya ubaadausasa ni ngumu kuifafanua. Hii ni kwa sababu makala mengi yametumia dhana hii katika miktadha tofauti tofauti. Kwa sababu hiyo dhana hii imekuwa na ugumu kuifafanua. Madai kama haya yanatolewa na Klages (1990) anayesema kuwa dhana hii ni changamano kwa sababu imetumika katika nyanja mbalimbali: sanaa, usanifu majengo, muziki, filamu, fasihi, sosholojia, mawasiliano, mitindo mipya na teknolojia.

Kulingana na Carter (2006) ubaadausasa ni dhana yenye fasili nyingi na wahakiki hawajaweza kukubaliana kuhusu fasili yake. Baadhi ya wahakiki huona ubaadausasa kama maendeleo ya baadaye ya dhana au kipindi cha usasa ila wengine uona kuwa ni dhana geni kabisa. Hata hivyo Carter anaeleza kuwa dhana hii ya ubaadausasa hutumiwa na wengi kuelezea umuhimu wa vyombo vya habari katika jamii zilizotawaliwa na mfumo wa kibepari katika K20. Rice na Waugh (2001) wanamtaja mwandishi wa riwaya kutoka Marekani ambaye katika mwaka wa 1980 alielezea ubaadausasa kuwa si maendeleo tu bali pia mabadiliko ya baadaye ya dhana au nadharia ya usasa. Aidha, wengine wanaeleza kuwa kuna kazi za kisanaa zilizoandikwa kabla ya ubaadausasa zinazoweza kuelezwa kama za ubaadausasa. Sim (2001) anataja kazi za Rabelais na Laurence Sterne kama baadhi ya kazi za aina hii. Aidha, baadhi hueleza ubaadausasa kama mwondoko unaopinga mawazo yanazohusishwa na usasa.

Kwa ufupi nadharia ya ubaadausasa ni dhana inayotumiwa kuhusisha upingaji wa tamaduni ambazo zimetawala mfumo wa maisha ya watu wa Ulaya katika karne kadhaa zilizopita. Kwa mujibu wa Bertens (1995) watu wa kwanza kupinga kanuni hizo ni pamoja na John Cage, Charles Olson, Robert Rauschenberg na Merce Cunningham. Mapinduzi haya yalifanyika katika Olson's Mountain College mwaka wa 1952. Waasisi hawa walikataa tamaduni za kimagharibi zilizokuwa zinaenda kinyume na mapitio ya ukweli ya binadamu. Pia walishuku imani za urazini na uelewaji wa mapitio yote ya binadamu. Naye Sim (2001) anasema kuwa wanabaadausasa wanashuku mifumo yote ya mamlaka, ufunuo wa hekima, tamaduni na kaida za kisiasa. Mfumo huu wa kushuku ni falsafa unaoitwa upingaji wa kaida. Kwa hivyo falsafa hii inashuku misingi yote iliyodaniwa ni ya ukweli. Kwa mfano umaksi, wao huona ubaadausasa hauna maana katika maisha na inafaa kutupiliwa mbali. Falsafa hii huliza maswali kama, ni nini hakikisho la ukweli katika dai hili? Mapinduzi haya yalipata cheki kutokana na wanafalsafa wengi na hasa Mjerumani Friedrich Nietzsche, aliyependekeza uchunguzi wa imani zote za binadamu. Mradi huu wa mwamko ulilenga kuiendeleza imani kuwa iwapo watu wataasi utamaduni, sheria za kidini na watumie urazini na umantiki hali hii ingeweza kuleta suluhisho kwa matatizo ya kijamii (Barry, 2002).

Imani hizo ambazo zilishukiwa na Friedrich Nietzsche ndizo kile Lyotard anaziita simulizi kuu (Fairlamb 1994; McHale 1992). Kwa hivyo simulizi kuu hasa ni nini? Hizi ni simulizi ambazo hujaribu kutoa suluhisho na kutatua matatizo ya binadamu kama vile Umaksi, dini na visasili. Kulingana na Carter (2006) jaribio la kuelezea ukuaji wa jamii na tamaduni zake kwa kutumia simulizi kuu na nadharia hazifai na hazikubaliki tena. Hii ni kwa sababu simulizi kuu hazina uhusiano wowote na historia halisi. Kwa mfano Sim



(2001) anaeleza kuwa simulizi ya Umaksi ilisisitiza ukombozi wa binadamu kutoka minyororo ya ubepari. Hata hivyo, umaksi haujaweza kuleta ule uhuru ulioahidi na hivyo basi kukosa kuaminiwa.

Bernstein (1992) anaeleza kuwa uchunguzi wa simulizi kuu ulisasabisha uporomokaji wake. Uporomokaji huu ndicho kile Wegesa na Macharia (2008) na Sim (2001) wanakiita simulizi ndogo ndogo. Kulingana na Sim, Lyotard anasema kuwa simulizi ndogo ndogo ni njia faafu ya kueneza na kubuni maarifa. Hii ni njia mojawapo wa kubomoa simulizi kubwa ambazo zilikuwa zinahodhi maarifa. Kwa hivyo hatutegemei simulizi kubwa tena kutupa mwelekeo wa maisha yetu. Simulizi hizi kubwa zitafifia zenyewe. Kulingana na Wegesa na Macharia (2008) wanauchanganuzi wa ubaadausasa wanakataa simulizi kubwa na mahala pake kuchukuliwa na simulizi ndogo ndogo na ‘vijihadithi’ vinavyosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha yao. Kulingana na McHale (1992) simulizi hizi ndogo huzingatia maslahi ya watu binafsi na kufanya simulizi zao kukubalika. Aidha, ni katika simulizi hizi ndogo ambapo watu hueleza (kuimba) mitazamo yao kuhusu mambo yao halisia.

Sim (2001) anaeleza kuwa katika sayansi mbinu hii ya kutumia simulizi ndogo ndogo ni nyenzo kuu katika kusuluhisha matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii ni kwa sababu mbinu hii huwawezesha kutafuta kweli kinzani, udhaifu na yasiyojulikana ambayo huwezekana kupitia simulizi ndogo ndogo ambazo zinakumba sehemu ndogo kuliko simulizi kubwa ambazo zinakumba ulimwengu mzima.

Utafiti huu basi uliangazia mifumo hii ya, dini, elimu, kaida za kisiasa, taasisi za binadamu na imani za kitamaduni na namna ilivyoleta madhara badala ya mafanikio kwa

wanajamii, hali ambayo ilisababisha kuzuka kwa njia mbadala za kuwasilisha na kutatua matatizo yanayoikumba jamii.

Wegesa na Macharia (2008) wanaeleza kuwa ubaadausasa ni mfumo ambao unahusu mambo ambayo yanafanyika katika mahala fulani kwa wakati maalumu, mambo ambayo yanafanyika wakati uliopo na huweza kubadilika wakati wowote, mambo ambayo hufanyika kwa muda mfupi na yanaweza kubadilika wakati wowote. Wanabaadausasa hawadai ukweli, mantiki au uthabiti wowote. Kutokana na maelezo hayo ubaadausasa ni dhana yumbulivu. Na hii inatufanya tuulize, Je, wanabaadausasa wanachukua msimamo wowote unaohusiana na suala la maadili? Je, kuna kigezo chochote cha kutumia? Kulingana na Sim (2001) changamoto ambayo tunakumbana nayo tunapohasi utamaduni na sheria za dini hasa ni kigezo kipi tutatumia kudai kitu fulani ni kizuri au kibaya? Lyotard alijadili dhana hii katika kitabu chake *Just Gaming* (1979) alitetea hoja hii kwa kusema kuwa kuhasi utamaduni huu haumaanishi mfumo wa ubaadausasa umeporomoka kama inavyodaiwa na wahasi wa ubaadausasa. Lyotard alipendekeza mtindo unaoitwa uchunguzi kifani ambao mtu anachukulia uchukulizi kuwa hakuna kigezo chochote cha kutumiwa kuhakiki wema au ubaya wa kitu fulani. Huu mfumo Lyotard aliuhita upagani. Kwa muhtasari Lyotard anakataa kitovu kinachotumiwa kuasisi ukweli au ubaya wa kitu chochote. Wanabaadausasa hawachukui msimamo wowote unaohusiana na suala la maadili. Hii ina maana kuwa hawaweki mipaka ya wazi kati ya wema na ubaya.

Kipengele hiki kuhusu uyumbulivu wa ubaadausasa kilikuwa muhimu katika utafiti huu kubainisha namna kaida zilizowekwa, ziwe za kidini, kisiasa na kitamaduni zilivyokiukwa na badala yake njia mbadala kutumiwa.

Kwa mujibu wa Grant (2001) Lyotard alipendekeza njia mbadala ya kusuluhisha matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni. Hii ni kwa sababu kaida za zamani za Umaksi, mradi wa mwamko na upanujaji wa soko vimejaribu lakini havitoshelezi. Baada ya kaida hizo kutotosheleza vikundi mbalimbali kama *socialism na Barbarism* (ambamo Lyotard alikuwa mwanachama) vilibuniwa ili kuleta majaribio ya kusuluhisha matatizo ya kijamii. Ithibati kamili ya kufeli kwa kaida hizo ilionekana kupitia maandamano ya wanafunzi na wafanyakazi nchini Paris mwezi wa Mei mwaka wa 1968 ambao walipinga uongozi mbaya wa serikali. Kwa hivyo Lyotard alipendekeza njia mbadala ambayo ni pamoja na majaribio katika muktadha husika.

Kipengele hiki kilikuwa kitovu kikuu cha utafiti kubainisha ni vipi nyimbo za Kikalenjin huangazia changamoto mbalimbali za jamii kwa kuzingatia miktadha mahususi.

Kwa upande wa mitindo ya uwasilishaji wa fasihi; ubaadausasa hurejelea mabadiliko ambayo yanakiukwa. Ubaadausasa ukataa kaida zilizojikita katika uhalisia, msuko uliofuatana kiwakati au kikronolojia, sauti moja iliyotawala usimulizi wote, tofauti iliopo baina ya sanaa ya juu na sanaa ya chini, tofauti iliopo katika tanzu na hitimisho zilizo funge (Sim 2001; Barry 2002; Klages 1990). Baadhi ya sifa hizi zinazotambulisha ubaadausasa ni pamoja na ukosefu wa mshikamano wa mawazo, ukosefu wa mahadhi na toni, paranoia, kuchanganya mitindo mingi katika kazi fulani ya sanaa ili kuiunda upya, ukiukaji wa muda wa mpangilio uliozoeleka na brikolojia, utumizizi wa kinaya, wizi wa mawazo au maandishi, matumizi ya hadithi ndogo ndogo zisizooana, dhana changamano, usimulizi wa kazi fulani katika miktadha tofauti, unukuzi wa kazi fulani au ufafanuzi, uvunjaji wa sarufi au kanuni zote za lugha. Baadhi ya vipengele hivi ndivyo utafiti huu

ulilenga kuchunguza ili kubainisha upekee wa mtindo hii, umuhimu wake na athari zake katika usawiri wa maudhui mamboleo.

Mitindo hiyo imetumiwa na wahakiki wengi sana. Kwa mfano Barry anamnukuu Eliots katika makala yake *The Waste Land*, ili kuthibitisha dhana ya kuweka mawazo pamoja bila utaratibu wowote. Katika makala haya Eliot anaweka kwa pamoja vipande vipande vya hadithi bila utaratibu maalum. Vile vile Cuddon katika Barry (2002) anaeleza ubaadausasa kama nadharia inayochukua mawazo mbalimbali na kuyaweka pamoja. Mawazo hayo yanaweza yasihusiane kwa vyovyote vile. Fauka ya hayo, mawazo hayo huwekwa pamoja bila kutumia utaratibu maalumu. Kwa mfano Barry anamnukuu Dadaists (1917) ambaye alitumia mfumo huu alipoandika mashairi yenye mishororo iliyotolewa magazetini bila taratibu maalum. Aidha, unatumia maigizo ya kazi ya kisanaa yenye kubeza.

Mitindo ya ubaadausasa imetumiwa na waandishi na waimbaji wengi sana. Kulingana na Lewis (2001) baadhi ya waandishi hawa ni: Gunter Grass and Peter Handke (Wajerumani); Georges Perec and Monique Wittig (Wafaransa); Umberto Eco and Italo Calvino (Waitaliano). Nayo katika nyanja ya muziki mitindo hii imetumiwa na waimbaji wa nyimbo pendwa na muziki zilizolibuniwa na Wamarekani weusi tangu K20 (Scott 2001). Lewis (2001) anamnukuu Fredrick Jameson aliyeandika makala *Postmodernism and Consumer Society* (1983) na kusema kuwa waandishi wa ubaadausasa hawavumbui tena mitindo mipya hasa kwa sababu mitindo mipya ilishabuniwa tayari. Kwa hivyo wanabaadausasa wanachukua mitindo ya kizamani na kujaribu kuunganisha au kuichanganya ili kuunda upya kazi za kisanaa. Jambo lingine ni kuwa kaida ya wakati kama inavyofuatiliwa katika kazi za kihalisia haizingatiwi. Kwa mfano, masimulizi

mengi yanaweza kufanyika wakati mmoja. Sim (2001) anaeleza kuwa wanabaadausasa hawaamini kuwa lazima kuwepo na ukamilifu au mshikamano unaotokana na muunganiko wa wahusika, mandhari, ploti na maudhui kama ilivyokuwa katika kazi za kisanaa za zamani. Walilenga kuunda simulizi (nyimbo) zao kwa njia mpya. Kwa mfano, matini inaweza kugawanyika katika vijisehemu tofauti vilivyotenganishwa na nafasi zilizo wazi. Katika nafasi hizi msanii anaweza kuweka ishara mbalimbali za maneno ambayo hayana mahusiano na wimbo wenyewe. Halikadhalika hitimisho inaweza kuwa na mawezekano kadhaa. Aidha, kazi za ubaadausasa zina mizunguko hivi kwamba si rahisi kutenganisha kazi za sanaa na ulimwengu halisi au kutofautisha viwango tofauti vya diskosi. Yaani, kazi za ubaadausasa zina mwingiliano wa matini (McHale 1992; Barry 2002; Klages 1990). Kulingana na Barry (2002) kazi za kifasihi za ubaadausasa huonyesha kukosekana kwa aina fulani ya hitimisho na uchambuzi huzingatia huo ukosefu. Kwa mujibu wa nadharia ya baadausasa, ulimwengu hauna mshikamano na nyimbo za kibaadausasa hudhihirisha dhana hii.

Katika utafiti wetu tulichunguza namna mitindo hii ya ubaadausasa ilivyojitokeza katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Kwa muhtasari, vigezo vifuatavyo vilitumika kama mihimili ya nadharia ya ubaadausasa katika utafiti huu:

1. Simulizi kuu na simulizi ndogo - nadharia ya ubaadausasa hushuku simulizi kuu ambazo hudai kumiliki ukweli halisi. Kwa mfano teknolojia, urazini, utamaduni, dini, sheria na mfumo wa kiuchumi na Umarx. Badala yake hupendelea simulizi ndogo ambazo watu hutoa maoni yao kuhusu suala fulani katika muktadha na wakati maalum.

2. Uchopekaji wa vipande vya simulizi - ni upinduaji wa nyenzo ambazo zilikuwa zimezoeleka katika uwasilishwaji wa kazi za sanaa. Nyenzo hizo ni pamoja na ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Katika Ploti, hakuna mantiki katika mpangilio wa matukio na visa. Wahusika na mandhari hubadilika ghafla, maudhui huwa changamano na sio rahisi kueleza juu yake.
3. Mwingiliano matini - ubaadausasa hutambua simulizi zingine hasa za watunzi wengine na kuzitumia kama sehemu ya masimulizi ya kazi mahususi ya kisanaa.
4. Uigaji wa vipande vya simulizi - kazi zozote zinazotumia mtindo huu huwa zimeundwa kwa upande mkubwa na maneno, virai, sentensi, aya, mizani na maonyesho kutoka kazi zingine.

### **1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI**

Kutokana na uchunguzi wetu, uwanja wa utafiti juu ya mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo teule za Kikalenjin haujatafitiwa. Kwa sababu hii, hakukuwa na maandishi yanayohusu mada hii kwa njia ya moja kwa moja. Nyingi ya kazi zinazohusiana na mada hii zimeegemea katika fasihi andishi. Hata hivyo maandishi haya yalikuwa ni muhimu katika utafiti huu kwani yalijenga msingi wa uhakiki wa nyimbo teule za Kikalenjin za K21.

Carter (2006) anatoa kwa muhtasari baadhi ya sifa zinazodhihirisha mitindo ya ubaadausasa katika fasihi ambazo ni: ukosefu wa tuni na mahadhi, matumizi ya visa vidogo vidogo visivyooana na ukosefu wa mshikamano wa mawazo. Carter anaona kuwa sifa hizo zinawakilisha dunia ya kisasa. Haya ni mawazo ambayo husherehekewa na wanabaadausasa kwani wanayaona kama njia ya kujikomboa kutokana na mifumo ya awali ambayo haikuruhusu mabadiliko. Mawazo ya Carter yalikuwa muhimu katika

utafiti huu kwani yameainisha sifa mbalimbali za mitindo ya ubaadausasa ambazo utafiti huu ulizichambua katika muktadha wa nyimbo za Kikalenjin katika K21.

Kramer (1996) alijadili mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo za Beethovens *String Quarter*, Ives *Putmans Camp* na Mahler *Seventh Symphony*. Kramer alidhihirisha mitindo ifuatayo: mwingiliano matini, unukuzi na brikolojia. Sawia na Kramer, Gloag (2012) alidhihirisha mtindo wa matumizi ya simulizi ndogo ndogo ya visa visivyoona katika nyimbo za John Cage, Dj Spooky, George Rochberg na John Zorn. Gloag na Kramer walichambua mitindo katika nyimbo zilizoimbwa kabla ya K21 hasa katika nchi za Kimagharibi. Tafiti hizi za Kramer na Gloag zilifaa utafiti huu hasa kwa sababu wamechambua mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo, lengo ambalo ndilo la utafiti huu.

Best na Keller (1991) wamejadili nadharia ya ubaadausasa kwa kina. Kwanza kabisa wataalamu hawa wamejadili kwa kina usuli wa kuchipuka kwa nadharia ya ubaadausasa. Wanasema kuwa nadharia ya ubaadausasa ilichipuka kutokana na mabadiliko ya kihistoria, kiuchumi, kisiasa, kijamii na kielimu. Maelezo hayo yalikuwa muhimu katika utafiti huu kuelewa kwa kina nadharia ya ubaadausasa iliyoongoza utafiti huu. Vile vile wataalamu hawa walijadili kwa kina usuli wa kuchipuka kwa mitindo ya ubaadausasa. Kulingana na wataalamu hawa mitindo ya ubaadausasa ilichipuka baada ya sanaa ya juu kusambaratika. Mawazo hayo yalifaidi utafiti huu kwani mtafiti aliweza kuelewa jinsi mitindo iliyohakikiwa ilivyochipuka katika fasihi.

Lewis (2001) katika nakala yake alijadili kwa kina mitindo ya ubaadausasa inayojitokeza katika fasihi. Baadhi ya mitindo ambayo alijadili na ilifanikisha utafiti huu ni uchopekaji wa vipande vya simulizi na uigaji wa vipande vya simulizi. Katika mitindo hiyo Lewis alifafanua maana ya dhana hizo, jinsi ilivyochipuka na matumizi yao katika fasihi.

Maelezo hayo yalifaidi utafiti huu kwani hiyo ndiyo baadhi ya mitindo ya ubaadausasa ambayo utafiti huu ulihakiki katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21.

Childs na Fowler (2006) katika kamusi yao ya fasihi, wamefafanua kwa kina mitindo ya ubaadausasa ambayo utafiti huu ulichanganua. Kwa upande wa mwingiliano matini wanahoji kuwa ni dhana inayotumiwa kuelezea matini yoyote yawe nyimbo, riwaya na filamu yanayorejelea matini mengine. Mawazo hayo yalisaidia utafiti huu kuhakiki nyimbo ambazo zilikuwa zinarejelea kazi zingine za awali. Kwa upande wa mtindo wa uigaji wa vipande vya simulizi Childs na Fowler wanahoji kuwa kazi zozote zinazotumia mtindo huu huwa zimeundwa kwa upande mkubwa na maneno, virai, sentensi, aya, mizani na onyesho kutoka kazi zingine. Mawazo hayo yalikuwa muhimu katika utafiti huu kubainisha nyimbo ambazo zilikuwa zimetumia mtindo huu.

Ritgerotil (2006) alichambua mitindo ya ubaadausasa katika filamu teule itwayo *The Simpsons*. Katika filamu hii mtaalamu huyu ameonyesha mitindo ya ubaadausasa iliyotumiwa ambayo ni mwingiliano matini, utohalisia na simulizi ndogo ndogo, paronia na uundaji wa simulizi kwa njia ya kubeza. Zaidi ya hayo, Ritgerotil amedhihirisha umuhimu wa mitindo hii ya ubaadausasa katika filamu hii. Utafiti huu ulifaidika kutokana na utafiti wa Ritgerotil hasa kwa sababu taaluma ya filamu na nyimbo hukaribiana katika uwasilishwaji wake. Kwa hivyo mtafiti wa utafiti huu aliweza kuangalia jinsi filamu hiyo ilivyochambuliwa na kutumia maarifa hayo kuhakiki mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo teule za K21.

Campbell (1983) alichunguza nyimbo za Waswahili katika tasnifu yake ya uzamifu yenye mada *Nyimbo za Kiswahili: A Socio-Ethnomusicological Study of a Swahili Poetic Form*. Campbell alichunguza baadhi ya sifa zinazosheheni nyimbo za Waswahili kama



matumizi ya vina na mizani na hivyo basi kuwa na mdundo wa kishairi. Utafiti wa Campell ulikuwa muhimu katika utafiti huu kutokana na kwamba umeeleza sifa zinazosheheni nyimbo za Waswahili. Sifa hizi ni tofauti na mitindo ya ubaadausasa. Kwa hivyo mtafiti wa utafiti huu aliweza kulinganisha sifa hizo na zile zilizoibuka baada ya K21. Hata hivyo tofauti ya utafiti wa Campell na huu umejitokeza katika upeo wa utafiti. Campell amejikita katika nyimbo za Waswahili ilhali utafiti huu unaangalia nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Vile vile yeye hakuchunguza mitindo ya ubaadausasa.

Wamitila (2008) alijadili kwa kina kipengele cha dhima ya nyimbo katika jamii. Nyimbo huwa kama hifadhi au rekodi za matukio muhimu ya kihistoria katika jamii mbalimbali, nyimbo huweza kuakisi vipengele mbalimbali vya jamii hiyo, huweza kutumiwa kama burudani, huakisi umbuji na ujumi wa tamaduni mbalimbali, kuhamasisha na kuelimisha jamii. Maelezo hayo ya Wamitila kuhusu nyimbo yalifaidi utafiti huu katika kuangazia umuhimu wa nyimbo katika jamii ya Wakalenjin.

Chesaina (1991) alizungumzia kwa kina fasihi simulizi ya jamii ya Kalenjin. Zaidi ya hayo aliangalia historia ya jamii ya Wakalenjin tangia walipohama kutoka mto Nile kule Sudan Kusini hadi wanapoishi sasa. Vilevile ameelezea mila na desturi zao kwa mfano tohara. Pia Chesainai alijadili lahaja nane zinazojumuisha kabila la Kikalenjin na kuonyesha jinsi lahaja zao zinavyokaribiana na hivyo wao kuweza kuelewana kwa urahisi. Fauka ya hayo, aliweza pia kujadili sifa na majukumu mbalimbali ya nyimbo za Kikalenjin kama vile kuadilisha jamii. Mawazo ya Chesainai yalisaidia utafiti huu kupata historia na maendeleo ya kabila la Wakalenjin, sifa zilizokuwa zikimiliki nyimbo za Kikalenjin hasa kabla ya kubadilika na umuhimu wao katika jamii ya Wakalenjin.

## **1.9 MBINU ZA UTAFITI**

### **1.9.0 UTEUZI WA USAMPULI**

Usampuli wa kimaksudi ulitumiwa kuteua nyimbo teule zilizoshughulikiwa katika tasnifu hii. Aina hii ya usampuli imechaguliwa ili kuhakikisha kwamba nyimbo zinazochaguliwa zina mitindo ya ubaadausasa. Hizi ni nyimbo ambazo zimeimbwa na waimbaji mbalimbali kuanzia mwaka wa 2000 hadi 2014. Vilevile nyimbo hizi zilidhihirisha vipengele vya mitindo ya ubaadausasa. Ili kupata sampuli wakilishi ya nyimbo za Kikalenjini, tasnifu hii ilitumia nyimbo ishirini na nne; nne kutoka kila mojawapo wa lahaja hizi: Kinandi, Kikeiyo, Kimarakwet na Kitugen. Nyimbo nane ziliteuliwa kutoka lahaja ya Kikipsigis, hii ni kwa sababu lahaja hii ina waimbaji wengi kushinda lahaja za Kinandi, Kikeiyo, Kimarakwet na Kitugen. Lengo la kufanya hivyo ni kupata data wakilishi ya vipengele vya mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo hizo. Mtafiti aliteua lahaja hizo tano kutokana na sababu zifuatazo:

Kwanza, kabisa lahaja hizi tano zina nyimbo zilizoimbwa baada ya K21 na zinadhahirisha mitindo ya ubaadausasa. Vilevile lahaja zao zinakaribiana na lahaja ya mtafitiya Kikeiyo. Kwa hivyo mtafiti aliweza kusanya data bila kuwa na changamoto nyingi. Maeneo wanamoishi lahaja hizi ni sehemu tofauti tofauti kwa hivyo tuliweza kupata data wakilishi ya jamii nzima ya Kikalenjini. Lahaja za Kimarakwet na Kikeiyo wanaishi kaunti ya Elgeiyo Marakwet, Lahaja ya Kitugen wanaishi kaunti ya Baringo, lahaja ya Kikipsigis kaunti ya Bomet na lahaja ya Kinandi kaunti ya Uasin Gishu. Pia lahaja hizo zinatofautiana kwa idadi ya wazungumzaji, Kikipsigis ni lahaja kubwa ikifuatiliwa na Kinandi, Kitugen, Kikeiyo na Kimarakwet. (<http://dickinsg.intrasun.tcnj.edu/nations/kenya/kalenjin.html-07/06/2013>).

Kutokana na sababu hizo data ambazo zilikusanya zilikuwa sampuli wakilishi.

### **1.9.1. UKUSANYAJI WA DATA**

Data ya kimsingi iliyotumika katika utafiti huu ilikuwa nyimbo za lahaja za Kikipsigis, Kinandi, Kikeiyo, Kimarakwet na Kitugen. Ukusanyaji wake ulikuwa na hatua mbili. Hatua ya kwanza ilihusisha kununua kanda zilizo na nyimbo zenyewe na hatua ya pili ilihusu kuzidadavua nyimbo hizo kwa misingi ya nadharia tete za utafiti. Ili kupata nambari kubwa ya nyimbo nilinunua kanda sita za lahaja za Kikeiyo, Kitugen, Kinandi na Kimarakwet huku nikinunua kanda tisa zenye nyimbo za lahaja ya Kikipsigis. Nilinunua kanda nyingi za Kikipsigis kwa sababu lahaja hiyo ina waimbaji wengi sana kushinda lahaja za Kikeiyo, Kitugen, Kinandi na Kimarkwet na vile vile nilikuwa ninahitaji nyimbo nane tofauti na lahaja hizo zingine nilizohitaji nne nne pekee. Kanda nilizonunua zilikuwa za waimbaji tofauti tofauti. Kila kanda ya nyimbo ilikuwa na nyimbo kumi (10); kumaanisha kwa lahaja moja nilikuwa na nyimbo sitini (60). Kwa hivyo katika lahaja za Kikeiyo, Kitugen, Kinandi na Kimarkwet nilikuwa na nyimbo mia mbili na arobaini (240) huku nikiwa na nyimbo tisini (90) katika lahaja ya Kikipsigis. Katika lahaja zote za Kikeiyo, Kitugen, Kinandi, Kikipsigis na Kimarkwet nilikuwa na nyimbo mia tatu na thelathini (330). Nyimbo hizi zilikuwa ni nyingi zaidi kuliko idadi niliyotumaini kutumia (ishirini na nne) katika utafiti. Hata hivyo, nilihisi ilikuwa vizuri kuwa na hazina kubwa ya nyimbo katika data ambazo ningeweza kurejelea baadaye kama ningelazimika kufanya hivyo. Ili kuhakikisha kwamba nyimbo hizo zimeimbwa baada ya mwaka wa 2000 niliangalia tarehe iliyokuwa imenakiliwa kwenye kanda mahususi.

### **1.9.2 UCHAGUZI WA SAMPULI YA NYIMBO**

Baada ya kupata nyimbo hizo, nilianza kutafuta sampuli ambayo ningetumia katika uchunguzi wangu. Mwanzo nilihifadhi nyimbo zote niliyonunua kwenye tarakilishi ili

niwe na marejeleo ya kudumu. Halafu nilianza shughuli ya kuchagua sampuli ambayo ningetumia katika utafiti huu. Shughuli hii ilifanywa katika hatua zifuatazo:

Hatua ya kwanza, nilisikiliza nyimbo hizo kwa umakini huku nikizingatia mihimili ya nadharia ya ubaadausasa. Nyimbo ambazo zilidhihirisha mitindo ya ubaadausasa; nilizidavua na kukusanya katika sehemu moja kwenye faili ya tarakilishi kwa mujibu wa lahaja. Hata hivyo niligundua kuwa katika nyimbo za lahaja moja, nyimbo nyingi (zaidi ya niliyohitaji katika utafiti huu) zilikuwa zinadhihirisha mitindo ya ubaadausasa. Ilipofanyika hivyo nilidavua wimbo ulio na mitindo mingi kuliko nyimbo zingine na hatimaye kubakia na nyimbo nne nne katika lahaja za Kikeiyo, Kitugen, Kinandi na Kimarkwet na nane katika lahaja ya Kikipsigis.

Hatua ya pili, nyimbo hizo nilizodavua katika hatua ya kwanza nilizisikiliza kwa mara ya pili huku nikinukuu kwenye daftari.

Hatua ya tatu, nyimbo hizo nilizorekodi katika hatua ya pili zilithibitishwa na wazungumzaji asilia ili kuhakikisha kwamba zimenukuliwa kwa njia ipasavyo.

Hatua ya nne, nilizitafsiri nyimbo hizo hadi lugha ya Kiswahili ili mtu asiyelewa lugha ya Kikalenjin aweze kusoma pia. Ikumbukwe kwamba haikuwa lazima nyimbo hizo zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mitindo ya ubaadausasa inajitokeza hata katika lugha ya Kikalenjin.

### **1.9.3. UTAFITI WA MAKTABANI**

Katika utafiti wa maktabani, vitabu, majarida na maandishi mbalimbali yalisomwa ili kupata habari muhimu kuhusu suala la mtindo na nyimbo. Aidha, maelezo kuhusu nadharia ya ubaadausasa ambayo ilitumiwa katika utafiti huu yalisomwa. Tahakiki

zilizotumia nadharia ya ubaadausasa pia zilisomwa kama msingi wa kuzihakiki nyimbo teule za K21 za Kikalenjin.

#### **1.9.4. VIFAA**

Vifaa vilivyotumiwa kukusanya na kupata data za utafiti huu ni kompyuta, vidude vya masikio, kanda za nyimbo zilizorekodiwa na daftari la kuandikia data na kalamu. Kanda za nyimbo zilizorekodiwa kama chanzo kikuu cha kupata data zilisikizwa kwa kompyuta na vidude vya masikio. Data za utafiti zilinukuliwa kwenye daftari kwa kutumia kalamu.

#### **1.9.5. UCHANGANUZI WA DATA**

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya ubaadausasa. Mihimili ya nadharia ya ubaadausasa iliyochanganuliwa katika utafiti huu ni simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi. Matokeo ya uchanganuzi huu yamejadiliwa katika sura ya tatu na nne.

Katika sura ya tatu, tulichanganua mihimili ya simulizi ndogo ndogo na uchopekaji wa vipande vya simulizi. Aidha, katika sura ya nne tulichanganua mihimili ya mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi. Ili kurahisisha urejelezi, kila mstari katika wimbo umepewa nambari. Katika uchanganuzi wetu tulirejelea wimbo mahususi kwa kutumia mistari, hata hivyo wimbo mzima unapatikana katika Kiambatanisho I.



## **SURA YA PILI**

### **HISTORIA NA MITINDO YA UBAADAUSASA KATIKA KAZI ZA FASIHI**

#### **2.0 UTANGULIZI**

Sura hii ya pili inatalii vipengele vya ubaadausasa katika muktadha wa utafiti huu. Katika sehemu ya kwanza ufafanuzi umetolewa wa vipindi mbalimbali vya historia kabla ya kipindi cha ubaadausasa, usuli na chimbuko la nadharia ya ubaadausasa. Kisha ufafanuzi umetolewa wa dhana ya nadharia ya ubaadausasa, tofauti iliyopo baina ya vipindi vya usasa na ubaadausasa, waasisi wakuu wa nadharia hii na matumizi yake katika fasihi. Pia usuli wa kuchipuka kwa mitindo ya ubaadausasa umejadiliwa. Hatimaye sura imefafanua mitindo minne ya nadharia ya ubaadausasa katika fasihi ambayo ni msingi mkuu wa utafiti hii.

#### **2.1 VIPINDI MBALIMBALI VYA HISTORIA YA DUNIA HADI KUFIKIA KIPINDI CHA UBAADAUSASA**

Kwa mujibu wa Best and Kellner (1991) nadharia yoyote ile huakisi jamii na huchipuka kutokana na tamaduni za jamii. Tamaduni hizo zinapokua na kubadilika, nadharia hasa huibuliwa na wataalamu ili kueleza tamaduni hizo kwa njia faafu. Hata hivyo katika sehemu ifuatayo tutaeleza kwa muhtasari vipindi mbalimbali vilivyojitokeza tangu binadamu aumbwe hadi katika kipindi cha ubaadausasa. Kisha tutajadili usuli na chimbuko la nadharia ya ubaadausasa. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kuonyesha kwamba kabla ya nadharia hii, kulikuwepo na mabadiliko ya kihistoria, kiuchumi, kisiasa, kijamii na kielimu yaliyotokea katika jamii za nyakati zilizopita hadi hivi sasa; na kuchangia kuchibuka kwa nadharia ya ubaadusasa.

Kulingana na Hutcheon (1985) imebainika kwamba kuna hawamu sita za mabadiliko kabla ya kufikiwa kwa kipindi cha ubaadausasa. Hawamu ya kwanza ni kipindi cha Tamaduni Simulizi kilichoanza tangia binadamu aumbwe na kujua kuzungumza. Kipindi hiki kilikuwa kimetawaliwa na sifa zifuatazo: hakukuwa na maandishi yoyote ya sheria na maarifa yaliyosisitizwa yalitegemea wakati uliopo, maandishi hawakuwepo, hakuna maisha ya siri, haki za binadamu asikufuatwa, hakukuwa na pesa na jamii ilikuwa inathamini hupeanaji wa zawadi.

Kufikia miaka ya 1550; kipindi cha utamaduni simulizi kilibadilika na kuingia Kipindi cha Mwamko. Katika kipindi hiki watu wengi walikuwa wamejua kuandika na kusoma, maandishi wa bibilia ulijitokeza, ugunduzi wa kisayansi, ukuaji wa sayansi asilia, udadadisi wa ukweli wa bibilia, imani katika Mungu moja, maisha ya kisiri yalibuniwa na haki za kibinadamu zilianza kuheshimiwa.

Kipindi hiki cha Mwamko kilifika tamati katika miaka ya 1660. Kipindi kilichofuata ni Kipindi cha Urazini. Kipindi cha Urazini kilianza katika karne ya kumi na nane (1660-1789). Mary Klages (1990) ameoredhesha sifa zifuatazo za kipindi hiki:

- Binadamu alianza kuwa na udhabiti, ushikamano na kujielewa mwenyewe.
- Urazini ulithaminiwa na kuonekana kuwa ni upeo wa juu katika binadamu. Ni kutokana na urazini huu ndipo binadamu aliweza kujielewa na kuelewa dunia yake.
- Iliaminika kuwa hekima iliyotokana na urazini haikuwa na upendeleo na ilisawasishwa na sayansi. Sayansi hii ndiyo iliyochukuliwa kuwa ya ukweli bila kuzingatia hekima ya mtu mahususi.



- Hekima iliyotolewa na sayansi hii ilichukuliwa kuwa ya ukweli na inayodumu milele.
- Iliaminika kuwa hekima inayotolewa na sayansi hii ya urazini ingeleta ukuaji na ukamilifu katika taasisi zote za binadamu.
- Urazini ulidhihirisha ukweli, sheria na mfumo wa maadili. Kwa hivyo uhuru wa aina yoyote ulikuwa lazima uheshimu sheria zilizofumbuliwa kupitia urazini wa binadamu.
- Sayansi ya urazini ilichukuliwa kama hekima muhimu katika jamii. Sayansi hii ilikuwa isiyo na upendeleo; kwa hivyo wanasayansi hawa walifaa kufuata sheria za urazini ili hekima yao iwe huru bila mapendeleo.
- Lugha iliyotumika katika utoaji na ueneaji wa hekima ilifaa kuwa razini. Lugha razini ni lugha ambayo maneno yake yaliweza kusimamia kile kitu kinachoashiria.

Kipindi cha Urazini, kilifuatwa na Kipindi cha Ulimbende. Kipindi hiki kilikuwa kipindi cha mapinduzi ya kisiasa na mabadiliko katika jamii. Mapinduzi ya Kisiasa yaliyotokea ni kama mapinduzi ya Amerika (1775) na mapinduzi ya Ufaransa (1789). Vilevile mabadiliko katika jamii yaliyotokea ni pamoja na mapinduzi ya viwanda, ukuaji wa tabaka la kati, uanzishaji wa miji, uthamini wa uvumbuzi kuliko vitu vya kawaida na kuwa na hari ya kupigania haki za binadamu. Baina ya miaka ya 1832-1898 kipindi cha Victoria kilichipuka. Katika kipindi hiki kiasi cha watu wa tabaka la kati na wale ambao walijua kuandika na kusoma waliongezeka. Ni katika kipindi hiki ndipo riwaya na sanaa za majengo zinazohusiana na Victoria zilichipuka.


Miaka ya 1898-1945 hurejelewa kama kipindi cha usasa. Kwa mujibu wa Barret (1997) kipindi hiki kilianza wakati wa kipindi cha urazini (1660-1789). Mwanasayansi Isaac Newton aliongoza imani kuwa kupitia sayansi dunia inaweza kubadilishwa. Vilevile wanafalsafa Rene Descartes (1596-1650) na Immanuel Kant (1724-1804) walisema kuwa ukweli ungeweza kupatikana kupitia urazini. Hii iliwapelekea wanasiasa kuamini kuwa kupitia urazini ukweli ungepatikana na hivyo basi kukua na kuimarika kwa jamii. Hayo yalipelekea mapinduzi yaliyofanyika katika Kipindi cha Urazini (Amerika na Ufaransa), vita vya kwanza na pili vya dunia. Nyenzo muhimu za kipindi hiki ni demokrasia, ubepari, ukuaji wa viwanda, sayansi, uhuru na ukuaji wa miji.

Kwa mujibu wa Hutcheon (1985) ni baada ya mwaka wa 1945 ambapo utamaduni wa ubaadausasa ulianza kuzungumziwa. Utamaduni huu ulikuwa changamano hasa ukilinganishwa na tamaduni zilizopita. Sifa nyingi za usasa ziliweza kujitokeza katika ubaadausasa na hivyo basi wakati mwingine huwa vigumu kutofautisha vipindi hivi viwili (Carter 2006; Barry 2002). Hata hivyo kipindi hiki cha ubaadausasa ni tofauti na usasa hasa kwa kuwa ubaadausasa unahusu uashiraji wa dunia upya kwa kutumia teknolojia, televisheni, filamu na tarakilishi (kama vile tutakavyojadili hapo chini). Kulingana Wegesa na Macharia (2008) ili kuelewa kipindi hiki cha ubaadausasa ni lazima tuitazame kwa kutumia nadharia. Kwa hivyo nadharia ya ubaadausasa iliweza kubuniwa ili kuhakiki mabadiliko hayo katika jamii (Ritgerotil 2006).

Jedwali la 1 lililoko katika ukurusa unaofuata linaonyesha kwa muhtasari vipindi sita vya historia vilivyojadiliwa hapo juu. Vipindi hivi vilianza kipindi cha utamaduni simulizi hadi kipindi cha ubaadausasa.

**Jedwali 1: VIPINDI MBALIMBALI HADI KUFIKIA KIPINDI CHA UBAADAUSASA**

<p>Kipindi cha Tamaduni Simulizi (0-1550)</p>	<p>Kipindi cha Mwamko (1550-1660)</p>
---	---



## 2.2 USULI NA CHIMBUKO LA NADHARIA YA UBAADAUSASA

Kulingana na Khamis (2008:8) nadharia yoyote ile huchipuka kutokana na sababu mbili.

Sababu ya kwanza ni kutokana na misingi ya nadharia zilizotangulia ambazo hurekebishwa ili ziwe zenye uwezo wa kutazama na kueleza vyema zaidi somo fulani.

Pili nadharia huchipuka kutokana na mabadiliko ya kihistoria, kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiteknolojia na kielimu yanayotokea katika jamii fulani. Nadharia ya ubaadausasa ilichipuka kutokana na sababu hizi mbili kama vile tutavyodhihirisha katika sehemu ifuatayo:

Kwa mujibu wa Best na Keller (1991) miongo minne (1970) iliyopita ilishuhudia mijadala kuhusu ubaadausasa katika sanaa mbalimbali duniani. Je, kipindi cha usasa katika sanaa kimefika kikomo? Je, kipindi cha ubaadausasa kingefuata? Katika falsafa, mijadala ilijadiliwa kama falsafa ya usasa imefika tamati, na wengi kusherehekea falsafa ya ubaadausasa iliyohusishwa na Nietzsche, Heidegger, Derrida, Rorty na Lyotard. Mijadala hiyo ya wanafalsafa hawa ilisababisha kuipuliwa kwa nadharia ya ubaadausasa ili kuelezea kipindi hiki kipa cha ubaadausasa na kusuluhisha matatizo yaliyokuwa yanakumba jamii.

Waasisi wa ubaadausasa walikosa tamaduni kongwe, wanausasa na siasa, nao wanausasa waliitikia waasisi wa ubaadausasa ama kwa kuwapuuza, kuwasuta, kuwasikiliza au kujadiliana nao. Waliopinga nadharia ya ubaadausasa waliona kama ni wingu la kupita, bunilizi za wasomi ili kuelezea diskosi mpya au dhana za kiitikadi zinazotaribu kupinga kipindi cha usasa. Hata hivyo mijadala hii ya ubaadausasa haikufifia kwa sababu ilizua mambo mapya yaliyostahili kujadiliwa na yaliyopiku kipindi cha usasa.

Kipindi cha usasa (iliyoasisiwa na Marx na Weber) kilikuwa na sifa za ubunifu, uungwana, mwamko na urazini. Urazini ulithaminiwa kuwa ungeleta ukuaji wa hekima, ukweli na maendeleo katika jamii. Kipindi hiki cha historia kilidhihirishwa kupitia njia za maisha ya kila siku kama sanaa ya usasa, bidhaa za kuuzwa katika soko, teknolojia, njia za mawasiliano na usafiri. Ni kupitia njia hizi ndipo kipindi hiki cha kihistoria kilisababisha dhana za ubinafsi, maisha yasiyoendeshwa kwa kutegemea dini, ukuaji wa viwanda, tofauti za kitamaduni, upatiani majina wa bidhaa na uuzaji kwa ajili ya faida, ukuaji wa miji, urasimu na urazini. Ni dhana hizi zote zilizokuwa zinaunda kipindi hiki

cha usasa. Hata hivyo kipindi hiki cha usasa kilijaa changamoto chungu nzima kama umasikini, udhalimu, utabaka, ubepari, taasubi za kiume na ukoloni. Zaidi ya hayo kipindi hiki cha historia kilisababisha kuzuka kwa taasisi za binadamu, matendo na diskosi zilizoruhusu matumizi ya mamlaka kandamifu. Kwa hivyo kipindi hiki cha kisasa kilisababisha mambo yaliyokuwa kinyume na matarajio ya wanajamii. Badala ya usasa kusuluhisha matatizo ya kijamii, ukandamizaji ulizidi kushamiri. Imani juu ya usasa ilionekana kupungua licha ya waasisi walioutetea usasa kama vile Habermas kulisitiza kuwa usasa ulikuwa bado haujafikia kikomo na hivyo bado ungeweza kusuluhisha matatizo ya jamii.

Waasisi wa nadharia ya ubaadausasa (Baudrillard, Lyotard na Harvey) walisitiza kuwa mabadiliko ya teknolojia, jamii na tamaduni ni dhana mpya na zinahitaji uhakiki kwa kutumia nadharia tofauti na mpya. Vilevile mabadiliko ya teknolojia kama tarakilishi, vyombo vya habari na mifumo mipya ya maarifa yalisababisha mandhari tofauti na ya awali. Baudrillard na Lyotard waliona mabadiliko hayo kama mitindo mipya ya habari, maarifa na teknolojia. Nao wanaumax Jameson na Harvey waliona mabadiliko hayo kama upeo wa juu wa kibepari duniani. Mabadiliko hayo yalisababisha kuvunjikavunjika tamaduni na uashiriaji, tamaduni na uzoefu mpya. Mabadiliko hayo ya kihistoria, kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiteknolojia na kielimu ndiyo yaliyozaufikra kuwa jamii zimo katika vipindi vya ubaadausasa.

## **2.3 NADHARIA YA UBAADAUSASA**

### **2.3.0 UFAFANUZI WA DHANA YA NADHARIA YA UBAADAUSASA**

Nadharia ya ubaadausasa imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali. Barry (2002) anamnukuu Cuddon anayesema kuwa ubaadausasa ni mtazamo usiofuata mfumo mmoja

wa mawazo bali hutumia mtindo wa kuunganisha vipengele tofauti vya maandishi visivyo na uhusiano vilivyochukuliwa bila kutumia utaratibu maalum. Aidha, unatumia maigizo ya kazi ya kisanaa yenye kubeza. Vilevile Barry (2002) anamnukuu Lyotard anayefafanua maana ya Ubaadausasa kama kushuku kwa simulizi kuu. Simulizi kuu kama Ukristo, Umarx na itikadi za Kisayansi haziaminiki tena na mahala pake panafaa pachukuliwe na simulizi ndogo ndogo. Simulizi hizi ndogo ndogo ni za muda tu, fanyifu na yenye suluhu, zisizo dumu milele. Simulizi ndogo ndogo ni msingi wa kusuluhisha matatizo maalum yanayowakumba watu mahususi.

Kulingana na Carter (2006) ubaadausasa ni neno lenye maana nyingi na wahakiki hawajaweza kukubaliana kuhusu fasili yake. Baadhi ya wahakiki huona ubaadausasa kama maendeleo ya baadaye ya dhana ya usasa. Aidha, baadhi hueleza ubaadausasa kama mwondoko unaopinga mawazo yanazohusishwa na usasa. Dhana ya ubaadausasa vilevile hutumiwa kueleza nafasi ya vyombo vya habari katika jamii zilizotawaliwa na mfumo wa kibepari mwishoni mwa K20. Zaidi ya hayo, Carter (kama hapo juu) anasema ubaadausasa ni hali ya kushuku elimu yoyote na hii imeathiri taaluma nyingi za masomo na taasisi za binadamu kama sosiolojia, sharia na elimu ya jamii. Kwa watu wengi ubaadausasa ni ukataaji wa dini na sheria zote za binadamu. Uandishi wa ubaadausasa huvuruga mbinu zote za uandishi zilizozoeleka. Hii imepelekea wanafunzi wa fasihi kufafanua ubaadausasa kama kitu chochote ambacho hawakielewi au kukieleza. Kwa muhtasari, Carter anafafanua ubaadausasa kuwa majaribio ya kueleza ukuaji wa tamaduni na jamii kwa kutumia simulizi kuu kama umaksi, dini, sharia na tamaduni haikubaliki wala kuaminika na kuwa haihusiani na historia halisi.

Sim (2001) amefafanua maana ya nadharia ya ubaadausasa kwa mtazamo wa kifalsafa. Sim anasema kuwa ubaadausasa ni mfumo wa kushuku mambo yakiwemo mamlaka, hekima tunazopokezwa na jamii, itikadi za tamaduni na siasa. Shauku ni aina ya falsafa hasi inayokataa nadharia zozote zinazodhani kuhodhi ukweli au kuwa na njia ya kung'amua ukweli. Istilahi mwafaka inayoweza kueleza aina hii ya falsafa ni upingaji wa kaida. Upingaji wa kaida, upinga imani zozote zilizodhaniwa kweli kwa njia ya kudadisi ukweli huo.

### **2.3.1. TOFAUTI BAINA YA VIPINDI VYA USASA NA UBAADAUSASA**

Kulingana na Barry (2002) na Carter (2006) kuna sintofahamu ya kutofautisha vipindi vya usasa na ubaadausasa. Hata hivyo Barry (kama hapo juu) anasema kuwa kipindi cha usasa kilitumiwa kwa upande mkubwa katika kuzungumzia kazi za K20. Kipindi cha ubaadausasa kilianza kutumika katika miaka ya 1980. Naye Carter (2006) anasema kuwa wataalamu wengine wanaamini kuwa kipindi cha ubaadausasa ni maendelezo ya vipengele vya kipindi cha usasa ilhali wengine huona kuwa ni tofauti kabisa. Vilevile wataalamu wengine wanataja kazi za kisanaa zilizotungwa kabla ya usasa lakini zinajumuishwa kama kazi za ubaadausasa. Ili kushadidia hoja hii Sim (2001) anataja kazi za Francois Rabelais na Laurence Sterne kama baadhi ya kazi za aina hii.

Barry (2002) anamnukuu (Arnold 1992) ili kuonyesha tofauti iliyopo baina ya vipindi hivi viwili. Barry anasema kuwa vipindi hivi viwili vinadhihirisha kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi lakini katika hali tofauti. Kipindi cha usasa kinadhihirisha kipengele hiki katika hali ya furaha huzuni, masikitiko, kukosa rajua na kukata tamaa kuhusu dunia. Kwa mfano Ezra Pound anaita kazi yake *The Cantos*; 'rag bag' akimaanisha kuwa kazi ya aina hii ni ya kisasa na vilevile akisikitikia kazi hiyo.

Vilevile Best and Kellner (1991) wanaonyesha Irving Howe katika kitabu chake *Mass Society and Postmodern Fiction* (1970) akisikitia kwa kufika tamati kwa kipindi cha usasa. Kinyume na hayo kipindi cha ubaadausasa husherekea kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi, wao huona kuwa ni ukombozi mkubwa sawia na ukombozi kutoka imani finyu zinazokandamiza. Best na Kellner wanadhihirisha hoja hii katika vitabu vya Leslie Fiedler, *The New Mutants* na *The Death of Avant-Garde Literature* (1971), zinazofurahia ukuaji wa sanaa ya utamaduni pendwa ambayo ilikuwa inafurahisha tofauti na sanaa ya juu na chini iliyokuwa imeshamiri katika kipindi cha usasa.

Tofauti nyingine baina ya ubaadausasa na usasa ni mtazamo kuhusu sanaa ya juu na sanaa ya chini. Usasa ulikuwa unakataa mchanganyiko baina ya sanaa ya juu na chini. Hii ilipelekea kuwepo kwa drama kama ya Samuel Beckett ambayo wakati wa kuigizwa ilifupishwa hadi dakika kumi na tatu, kuwepo kwa mwigizaji mmoja, kutokuwepo na mandhari wala lugha faafu. Kinyume na hii ubaadausasa hukataa utofautishaji huu wa sanaa. Wao huamini mchanganyiko wa elementi zote za kisanaa, kwa mfano mashairi ya waandishi kama Craig Raine na Christopher Reid yalikuwa na mchanganyiko ya elementi za taswira, misamiati na uzungumzaji nafsia.

Barret (1997) anasema kuwa wanausasa huamini kuwa nadharia huakisi maisha halisi ya mtu; urazini na hekima ni vyanzo vya ukweli. Tofauti na madai hayo, wanabaadausasa wanashuku imani hizi kuwa nadharia haiwezi kuakisi hali halisi ya maisha ya binadamu.

Vilevile urazini na hekima sio lazima zidhihirishe ukweli kwani ni ufasiri wa mtu binafsi na huathiriwa na utamaduni na lugha yake. Ili kudhihirisha hoja hii, Jacques Derrida (mwanaubadausasa) anasema hivi kuhusu dhana ya ukweli:



Fafanuzi zote za dunia, sayansi ikiwepo, ni hadithi au diskosi tu inayobuniwa na watu. Hatuwezi kufikia ukweli wowote, ila tunauzungumzia tu. Hakuna ukweli bali hizo ni diskosi au hadithi bunilizi (Barret 1997) (TY).

### **2.3.2 WAASISI WAKUU WA NADHARIA YA UBAADAUSASA**

Kabla hatujewaangalia waasisi wakuu wa nadharia ya ubaadausasa hatuna budi kumzungumzia mwananadharia wa Kijerumani Jiir Habermas. Kulingana na Barry (2002) mwananadharia huyu aliwasilisha makala iitwayo *Modernity - An incomplete project* (1980) ambayo ilikuwa msingi mkuu wa waasisi wa nadharia ya ubaadausasa. Kulingana na Habermas kipindi cha Usasa kilianza katika kipindi cha Mwamko (1660-1789) na bado kinaendelea. Ni wakati huu ambapo mwamko wa urazini, uasi wa tamaduni na sheria za dini zisizofaa ziliaminika zingesuluhisha matatizo ya kijamii. Mawazo hayo yaliendelezwa na wanafalsafa Kant kutoka Ujerumani, Voltaire na Diderot kutoka Ufaransa pamoja na Locke na Hume kutoka Uingereza. Ni mtazamo huu ndio Harbemas aliuita usasa. Kipindi hiki cha usasa kilisababisha majaribio ya mapinduzi ya Ufaransa (1789) na hivyo kuendelea kustawi. Kulingana na Habermas wanabaadaumuundo wa Kifaransa- Derrida na Foucault -walipinga mwamko huu wa usasa. Wanabaadaumuundo hawa walipinga dhana za usasa za urazini, ukweli, ubayana na ukuaji na hivyo basi kuonekana kudidimiza ustawi wa kipindi hiki.

#### **2.3.2.0 JEAN FRANCOIS LYOTARD**

Katika taaluma yake ya hapo awali Lyotard anaweza kuelezwa kuwa alikuwa mwanaumarx. Lyotard alikuwa mwanachama wa kikundi cha *Socialisme ou barbarie* kilichokuwa kinahakiki nadharia ya Umarx. Hata hivyo kikundi hiki ambacho makao yake yalikuwa Paris kilisambaratika mwaka wa 1960 na Lyotard alionekana kujitenga na imani za Kimarx. Katika mwaka wa 1974 Lyotard aliandika kitabu *Libidinal Economy* kilichopinga Umarx kwa kukosa kukidhi mahitaji ya binadamu; sababu mahitaji hayo

yalikuwa yanapiku uwezo wa nadharia hii (Sim 2001). Hapa ndipo tunaweza kusema ulikuwa mwanzo wa Lyotard kuanza azma yake kuu ya kupinga simulizi kuu na hivyo basi kupendelea ubaadausasa.

Kwa mujibu wa Barry (2002) dhana hii ya ubaadausasa ilitumika mwanzo mwaka wa 1930. Lakini hata hivyo matumizi ya sasa yalipata msukumo mkubwa kutokana na makala ya Lyotard aliyowasilisha mwaka wa 1979-*The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*.

Vilevile Lyotard alichapisha makala nyingine mwaka wa 1982: *Answering the Question: What is Postmodernism*. Ni katika makala hii alipojadili mtazamo wake kuhusu kipindi cha Mwamko kilichoendelezwa na Habermas. Lyotard alikataa maoni ya Habermas kuwa Kipindi cha Mwamko bado hakijakamilika; alikataa wito wake wa kutupiliwa mbali kwa majaribio. Alimwandikia Habermas hivi:

Nimesoma kuhusu mwanafalsafa (Habermas) anayetetea usasa. Lakini katika mwamko wa Ubaadausasa, nina imani (Lyotard) kuwa, nitatupilia mbali mwamko huu wa usasa ambao haujakamilika (Barry, 2002 akimnukuu Brooker, 1992:141) (TY).

Kulingana na Lyotard, kipindi hiki cha Mwamko kinachotetewa na Habermas, kimejaa simulizi kuu zinazopania kuwakandamiza na kuwapunja wanajamii. Lyotard aliutaja Ukristo, Umarx au itikadi za ukuaji wa Sayansi kama simulizi kuu mahususi ambazo zimesheheni udikteta na kuendeleza mamlaka ya watu wateule katika jamii. Simulizi hizi kuu haziaminiki tena na zinaendelezwa ili kuzuia tofauti, upingamizi na uwingi maana. Hii ilimpelekea Lyotard kufafanua maana ya ubaadausasa kama kutoaminika kwa simulizi kuu. Simulizi kuu za ukuaji na ukamilifu wa binadamu hazingeweza kutetewa tena na mahala pake panafaa pachukuliwe na simulizi ndogo ndogo. Simulizi hizi ndogo ndogo ni badilifu kulingana na muktadha, zinazotoa suluhu, zisizodumu milele. Simulizi ndogo ndogo ni msingi wa kusuluhisha matatizo maalum zinazokumba watu mahususi.

Kwa ufupi ubaadausasa udengua lengo kuu la kipindi cha Mwamko la ukamilifu wa historia.

### **2.3.2.1 JEAN BAUDRILLARD**

Kwa mujibu wa Sim (2001) Jean Baudrillard alizaliwa katika mji wa Reims nchini Ufaransa tarehe 9 Julai, 1929. Alianza taaluma yake kama profesa wa elimu katika shule za upili; alizamia ufundishaji wa sera za kijamii za Kijerumani na fasihi. Hata hivyo baadaye aliweza kusomea masomo ya Sosiolojia na Falsafa. Jean Baudrillard aliweza kuandika makala mengi yakiwemo: *The Mirror of Production in, Symbolic Exchange and Death, Simulacra na Simulations, Seduction, America, The Gulf War Did Not Take Place*. Hapo awali mwaasisi huyu alijulikana kama Mwanaumarx, lakini baada ya kuchapisha makala yake ya *The Mirror of Production in* (1973), alionekana akijitenga na Umarx kwa sababu ulikuwa na udhaifu mwingi kama ubepari uliokuwa umekithiri katika jamii.

Ni wakati huu ambapo Jean Baudrillard alijiunga na ubaadausasa. Nyenzo muhimu alizoendeleza za ubaadausasa ni uhusiano baina ya uhalisia na uonevu, athari za vyombo vya habari pamoja na matangazo ya biashara na changamoto za uwasilishaji

Baudrillard katika makala yake *The Mirror of Production in* (1973) anasema kuwa kwa kawaida tamaduni zinafaa kuleta maana na mtagusano katika jamii; jambo ambalo linawezekana kupitia matumizi ya ishara. Ishara hizi zinafanya kazi tu iwapo zitahusishwa moja kwa moja na watu na mazingira halisia. Hata hivyo kutokana na uuzaji wa bidhaa kwa minajili ya faida, matangazo ya biashara na matumizi ya vyombo vya habari, ishara hizi haziwakilishi uhalisia tena, bali uhusiano wao na uhalisi umekatizwa au kutiliwa chuku. Hivyo basi ishara hizi zimekuwa isharaselea; bila urejeleaji wa ukweli

halisia. Isharaselea hizi huwa hazina maana halisia kwa wanadamu; ni kutokana na dhana hii ndipo wanadamu wanatatisika kuelewa dunia yao ipasavyo.

Vilevile Barry (2002) anasema kuwa Baudrillard katika makala yake, *Simulcara and Simulation* (1981) anafafanua kuwa hapo awali palikuwa na ukamilifu ambapo ishara ilikuwa kiwakilishi kinachosimamia ukweli au uhalisi uliofichika. Jambo hili ni tofauti wakati huu wa ubaadausasa, huu umetokana na uigaji mwingi na kupelekea ishara kutokuwa na uhusiano wowote na uhalisi. Sababu hasa ni kutokana na athari za kiteknolojia ambayo yamesababisha kutokuwepo na mipaka kati ya hali halisi na ya kimawazo, ukweli na ndoto na vilevile maana ya juu na maana ya ndani. Athari hizi zinasababisha utamaduni wenye uhalisia uliotiliwa chuku. Inapofanyika hivyo ishara huchukuliwa kama ndio kitu halisi. Aidha, inapochukuliwa hivyo ishara hizi hukosa kuwakilisha ukweli halisia. Kwa hivyo katika enzi ya ubaadausasa inakuwa vigumu kutenganisha kati ya uhalisi na utohalisi.

### **2.3.2.2 FREDRICK JAMESON**

Kwa mujibu wa Ritgerotil (2006) na Best na Keller (1991) katika mwaka wa 1984 mwananadharia wa Kimarx Fredrick Jameson alijulikana kama mhakiki mkuu wa nadharia ya ubaadausasa. Hii ilitokana na uchapishaji wa kazi yake iitwayo *Postmodernism, or The Cultural Logic of Late Capitalism* (1991) ambayo ilichapishwa baadaye kama kitabu. Katika kazi hii, Jameson aliunganisha uhakiki wa ujumi wa sanaa na nadharia ya jamii na uchumi. Lengo lilikuwa ni kuonyesha kuwa utoaji wa ujumi wa kisanaa siku hizi umefungamanishwa na utoaji wa bidhaa za kiuchumi. Jameson alifafanua ubaadausasa kama nguvu za kitamaduni zinazoendeshwa na nguvu za kibebari za kimataifa. Best na Keller (1991) wakimnukuu Jameson 1984 na 1991 wanasema kuwa

ubaadausasa iliashiria kutamatika kwa kipindi cha usasa. Kipindi hiki cha ubaadausasa kilishamiri michanganyo ya sanaa ya juu na chini, matumizi ya mitindo ya uigaji wa vipande vya simulizi pamoja na uchopekaji wa vipande vya simulizi.

Jameson alichangia pakubwa katika ufafanuzi wa sifa mbalimbali za ubaadausasa. Alifafanua ubaadausasa kama mitindo mipya inayoselea na isiyokuwa na mizizi au vyanzo mahususi. Katika nakala yake *Postmodernism, or The Cultural Logic of Late Capitalism (1991)* Jameson alifafanua kupotea kwa historia halisi katika uandishi. Anasema kuwa riwaya za historia haziwezi kuwakilisha historia jinsi ilivyo, bali zinawakilisha mawazo yetu tu (Ritgerotil 2006 akimnukuu Jameson, 2001:79). Katika enzi hizi za ubaadausasa, historia yetu inawakilishwa sio kupitia yaliyomo kitabuni bali kupitia mitindo danganyifu na hivyo basi kuonyesha historia kwa njia isiyofaa. Jameson alidhihirisha ubadilikaji katika matumizi ya mitindo ya kisanaa. Kwa mfano, badala ya kubuni mitindo mipya ya kisanaa, waandishi huangalia nyuma na kuiga mitindo ya zamani iliyokufa kama uigaji wa vipande vya simulizi. Katika enzi za kibaadausasa mitindo mipya, ambayo ilikuwa nyenzo kuu ya usasa, imekuwa mitindo ya kawaida inayowakilisha dunia.

### **2.3.3 MATUMIZI YA NADHARIA YA UBAADAUSASA**

Mwamzandi (2013) anahoji kuwa ni jambo la kiada na lililokubalika kuzitumia nadharia kama msingi wa kuzisoma, kuzichambua na hatimaye kuzizungumzia kazi za fasihi. Ni kutokana na madai hayo nadharia ya ubaadausasa hutumiwa kuhakiki kazi za kifasihi za K20 na K21 kwa kuangalia maudhui, mitindo na mielekeo. Aidha, Mwamzandi katika makala yake anadhihirisha jinsi fasihi za kileo zinavyochukua hulka ya kuasisi nadharia ya ubaadausasa na kuzifanya kuwa kiini cha kazi hizo.

Gromov (2008) anasema kuwa miaka ya tisini ilishuhudia kuzuka kwa maandiko yaliyoathiriwa kwa kiasi na mbinu za usasabaadaye, miongoni mwao ubunaji wa visaasili na utumiaji wa uhalisia wa kimaajabu. Baadhi ya waandishi ambao wametumia mbinu hizi ni pamoja na Clara Momanyi, Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed Mohammed, Kyallo Wadi Wamitila na William Mkufya. Hadithi zao ni za kupendeza sana, na hata msomaji asiye na ujuzi anaweza kuzisoma-lakini kwake riwaya hizo zitaonekana kama visa au ngano tu. Kwa hivyo ili kupata ufahamikaji halisi wa riwaya hizo lazima kutumia nadharia ya ubaadausasa.

Kwa mujibu wa Barry (2002) wanabaadausasa huangalia kwa jicho pevu kazi za kinathari kwa sababu zinadhihirisha utohalisia (sifa ya ubaadausasa). Kazi za kinatharia zinadhihirisha michanganyo ya tanzu mbalimbali za fasihi kwa mfano riwaya ya upelelezi, kisaikolojia na tamthilia. Zaidi ya hayo nadharia ya ubaadausasa hutumiwa kuhakiki mitindo ya ubaadausasa iliyotumiwa katika kazi za fasihi kama mwingiliano matini, uigaji wa vipande vya simulizi, Simulizi ndogo ndogo na uchopekaji wa simulizi.

Kulingana na Khamis (2008) nadharia ya ubaadausasa hutumiwa kuhakiki kazi za kinadharia zilizo na vipengele ambavyo havimo katika kazi zilizotangulia za uhalisia. Kwa mfano riwaya zinazotumia usimulizi wa mikondo mingi: nafsi ya kwanza, nafsi ya tatu, hata nafsi ya pili, nafsi ya tatu katika nafsi ya kwanza. Usimulizi ulio na tabia ya kugeuka ghafla bila ya kuonekana kuvuka mstari wa ng'ambo nyingine za mitazamo.

### **2.3.4 MITINDO YA UBAADAUSASA KATIKA KAZI ZA FASIHI**

#### **2.3.4.0 USULI WA KUCHIPUKA KWA MITINDO YA NADHARIA YA UBAADAUSASA**

Kwa mujibu wa Best and Kellner (1991) tangu K19 kipindi cha usasa kilichukua mwelekeo mpya katika sanaa. Mitindo mipya ilianza kujitokeza. Vilevile madhumuni

mapya ya sanaa na msanii yalisisitizwa katika jamii. Kwa mfano mwaka wa 1850 mshairi Charles Baudelaire aliandika shairi la usasa lililokuwa linaakisi maisha halisi ya usasa; Arthur Rimband alidai kwamba sanaa lazima idhihirishe usasa na Ezra Pound alisisitiza sanaa lazima ifanywe kuwa mpya. Kwa ufupi sanaa ya kisasa ilisisitiza ubunifu, ugeni na maudhui kuakisi maisha jinsi yalivyo. Kwa kufanya hivyo usasa ulihimiza ukataaji wa mitindo ya zamani na kuisitiza ubunaji wa mitindo mipya.

Kipindi hiki cha usasa kilisisitiza swala la uhuru wa sanaa kutokana na dini, maadili na siasa na hivyo basi msanii wa sanaa kujihusisha na sanaa kwa ajili ya sanaa. Kutokana na imani hii, sanaa ilijitenga na taaluma zingine na hivyo basi kukosa kuwakilisha na kuigiza uhalisia wa maisha. Hii iliifanya sanaa kuwa wa hulka ya kujirejelea yenyewe kuliko kurejelea jamii au hata uhusiano wa msanii na jamii. Imani hii ilikuwa na athari hasi kwa sanaa kwani ilifanya sanaa kuwa ya kuwazika tu.

Best na Kellner (1991) wakimnukuu Huysen (1986) wanasema kuwa kufikia K20 sanaa ya usasa ilikuwa imefafanuliwa kama sanaa ya juu, tofauti na sanaa ya chini. Sanaa hii ya juu ilikuwa ya ubunifu wa hali ya juu na hata kutoeleweka kwa watu wa kawaida. Hii ni kwa sababu wasanii walianza kutumia lugha, maono na mitindo iliyokuwa inaeleweka na wao pekee. Kwa mfano riwaya za akina Eliot, Pound, Klee na Kandinsky zilizosomwa na watu wachache sana. Kwa ujumla wasanii wa kipindi cha usasa walijitenga na jamii na hii ilidhihirishwa katika kazi za fasihi.

Wasanii hawa walifaa kuwa na ubunifu wa hali ya juu, sawia na kazi zao. Kazi hizi zilifaa kutoa maono ya msanii kuhusu dunia yake, kubuni dhana, mtazamo na fikra mpya za kisanaa. Hivyo basi ilikuwa rahisi kutofautisha kazi za wasanii mbalimbali kama vile upakaji rangi wa Momet au Van Gogh, Usimulizi wa Kafka au Hemingway, nyimbo za

Schoenberg au Stravinsky, tamthilia za Pirandello au Brecht au majengo yaliyo na mtindo wa kimataifa.

Sanaa ilipofikia kiwango hiki cha juu, usasa ulianza kusambaratika. Kulikuwa na hisia kuwa sanaa ya juu imefika kikomo, kwani ugeni na ubunifu wa wasanii ulikuwa umefikia upeo wa juu kiasi cha kutowezekana kutunga kazi zingine. Kwa mfano upakaji rangi nyeupe kwa rangi nyeupe na mrusi Kasimir Malevich ulidhihirisha mwisho wa upakaji rangi na maandishi kama *literature of exhaustion* na John Barth kuonyesha mwisho wa fasihi (labda kutokana na mitindo iliyofuatwa na wanausasa). Ilionekana kuwa kilichobaki ni mwananadharia wa ubaadausasa kukusanya mitindo ya zamani na kuipanga upya. Kwa hivyo badala ya ugeni na ubunifu uliokuwa katika usasa, wanabaadausasa walithamini uigaji wa kazi zingine au unukuzi wa kazi zilizotungwa zamani. Wanabaadausasa pia hawakumthamini mwandishi au msanii kama walivyo wanausasa na hivyo basi kuubainisha ubaadausasa kama mwingiliano matini au unukuzi na ufafanuzi wa kazi zingine.

Kwa hivyo sanaa mpya ilianza kujitokeza kupitia matumizi ya mitindo ya ubaadausasa. Matumizi ya mitindo hii ya ubaadausasa ilijitokeza katika kazi kama riwaya za William Burroughs, nyimbo za John Cage na Merce Cunningham, upakaji rangi wa Andy Warhol na usanifu majengo wa Robert Venturi na Philip Johnson.


Mtindo mwingine wa ubaadausasa ulitokana na Lyotard aliyepinga simulizi kuu za Ukristo, ufunuo wa hekima, tamaduni, kaida za kisiasa, mifumo yote ya mamlaka, elimu na sayansi . Kwa mujibu wa Lyotard mifumo hii mikuu ya hekima ilikuwa haiaminiki tena na ilikuwa inaendelezwa ili kuzuia tofauti, upingamizi na uwingi maana. Fauka ya hayo simulizi hizi kuu hazikuwa zinasuluhisha matatizo ya binadamu. Kwa hivyo Lyotard



alipendekeza mtindo tofauti wa kusuluhisha matatizo ya kijamii-matumizi ya simulizi ndogondogo. Mtindo huu wa simulizi ndogo ndogo ni msingi wa kusuluhisha matatizo maalum yanayowakumba watu mahususi katika jamii (Barry 2002; Carter 2006). Katika sehemu ifuatayo tutaangalia kwa undani mitindo hii ya ubaadausasa iliyojitokeza katika fasihi.

Jedwali 2 lililoko ukurasa unaofuata linaonyesha kwa muhtasari jinsi fasihi ilivyobadilika kuanzia K19 hadi K21. Kati ya K19 na K20, fasihi hasa ilichukua mwelekeo wa kipindi cha usasa. Kipindi hiki kilikuwa kimeshamiri sifa zifuatazo: sanaa ilisisitiza ubunifu na ugeni wa kila msanii, sanaa kwa ajili ya sanaa, kuthamini mwandishi na matumizi ya simulizi kubwa. Ni kutokana na sifa hizi ndipo sanaa ilijulikana kama sanaa ya juu, sanaa ambayo ilijitenga na jamii na hivyo basi kusambaratika katika K20. Ni baada ya sanaa hii ya juu kusambaratika ndipo kipindi cha ubaadausasa kikaanza na hivyo basi fasihi ikajulikana kama fasihi ya kileo. Fasihi hii ya kileo ilishamiri sifa zifuatazo: Matumizi ya simulizi ndogo ndogo, kutothaminiwa kwa mwandishi na ukusanyaji wa mitindo ya zamani na kuipanga upya. Ni sifa hizi zilizochipua mitindo ya ubaadausasa katika fasihi.

**Jedwali 2: MITINDO YA UBAADAUSASA KATIKA FASIHI ILIYOBUNIWA BAADA YA KUSAMBARATIKA KWA SANAA YA JUU MNAMO K20**



**Chanzo:** Mtafiti b

### 2.3.4.1. SIMULIZI NDOGO NDOGO

Dhana hii ya simulizi ndogo ndogo inatokana na nadharia ya simulizi kuu inayohusishwa na Lyotard. Lyotard anasema kuwa simulizi kuu zinazodhaniwa kueleza maisha ya binadamu haziaminiki na huendelezwa tu ili kuzuia tofauti, upingamizi na uwingi maana (Barry 2002:86).

Kulingana na Wegesa na Macharia (2008) wahakiki wa ubaadasasa hukataa simulizi kuu na kupendelea Simulizi ndogo ndogo na vijihadithi vinavyoeleza vitendo vya jamii maalumu na wala si dunia nzima. Simulizi ndogo ndogo ni badilifu kimuktadha, badilifu

kiwakati, zenye natija na zisizodumu milele. Simulizi hizi za kibaadausasa si falsafa ya kilimwengu wala haudai kumiliki ukweli, urazini au uthabiti wowote.

Fauka ya hayo Wegesa na Macharia (2008) wameonyesha upingaji wa simulizi kuu za dini, utamaduni na sheria katika hali tatu tofauti nchini Kenya ambazo ni matanga, sekta ya uchukuzi wa umma (matatu) na kundi la Mungiki. Wamebainisha kuwa makundi haya matatu hupinga simulizi hizo kuu na badala yake kupendekeza simulizi ndogo ndogo zinazosuluhisha matatizo yao maalum.

Kwa mujibu wa Sim (2001) simulizi kuu hazina uhusiano wowote na historia halisi ya binadamu. Simulizi hizo ni kama za Umarx, dini na visasili. Simulizi hizi hazina suluhu maalumu; kwa mfano simulizi kuu ya Umarx ilisisitiza ukombozi wa binadamu kutoka minyororo ya ubepari lakini haikutimiza. Kwa hivyo simulizi hizi kuu zinafaa kutupiliwa mbali na pahali pao pachukuliwe na simulizi ndogo ndogo zilizo na suluhu kwa matatizo ya binadamu.

#### **2.4.4.2. UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI**

Kwa mujibu wa Best na Keller (1991) dhana hii inahusishwa na jinsi fasihi mamboleo inavyowasilishwa. Ni upingaji wa muundo maalum, mpangilio na mtiririko wa fasihi na badala yake kupendelea mitindo inayofafanuliwa na kutokuwepo kwa mpango, yenye vurugu na ubahatishaji, isiyo na mfululizo, isiyo wazi na iliyojaa michezo. Kwa mfano waimbaji John Cage na Mere Cunningham walitumia mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi. Waimbaji hawa walitumia ubahatishaji walipoimba nyimbo zisizo na mpangilio wowote kwa upande wa maudhui, sauti na tuni. Vilevile walidai kuwa wasikilizaji walikuwa na uhuru wa kujifasiria maana ya nyimbo hizo.

Barry (2002) alipokuwa akieleza maana ya ubaadausasa alifafanua kwa kutumia dhana hii ya uchopekaji wa vipande vya simulizi. Alisema kuwa ubaadausasa ni mtazamo usiofuata mfumo mmoja wa mawazo bali hutumia mtindo wa kuunganisha vipengele tofauti vya maandishi visivyo na uhusiano vilivyochukuliwa bila kutumia utaratibu maalumu. Ili kudhihirisha hoja hii Barry (2002) anamnukuu Eliots aliyetumia mtindo huu. Eliots alitumia mhimili huu alipoweka pamoja kolaji au vipande vya hadithi visivyokamilika. Vilevile Barry anaonyesha kuwa Dadaist (1917) alitumia mtindo huu kwa kutunga mashairi kwa kukutanisha sentensi zilizotolewa magazetini bila utaratibu maalumu. Kazi za kibaadausasa zinazotumia mtindo huu huwa hazina hitimisho maalumu na uchanganuzi wake hutegemea kipengele hiki (Barry 2002).

Sim (2001) anasema kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi ni ubadilishaji au ukiukaji wa ploti, wahusika, mandhari na maudhui katika kazi za fasihi. Kwa hivyo mtindo huu unasababisha mabadiliko katika tanzu za fasihi kutoka mtindo tuliokuwa tumeuzoea. Ni hapa ndipo Khamis (2008) anazungumzia kuhusu riwaya mpya ya Kiswahili iliyojaliwa miaka ya 1990. Anasema kuwa riwaya hizi zinakiuka takriban misingi yote ya kanuni za riwaya za uhalisia zilizotangulia. Ili kushadidia hoja hii Khamis anasema:

[Katika riwaya mpya] hakuna hadithi inayoshikamana kiwakati kama tuzijuavyo hadithi zilizoandikwa kwa mtindo wa uhalisia. Badala yake kuna vipande vya hadithi, matukio, vitukio na visa ambavyo vimevunjavunjwa maksudi na kukutanishwa mbali na mnyororo wa safari au utashi wa mhusika fulani kutaka kugundua au kutatua tatizo fulani. Hadithi, visa matukio haviaminiki katika mantiki ya maisha ya kawaida bali vinasimamia fantasia na mazingaombwe yaliyochanganyika na uhalisia wa aina fulani. Aidha, usimulizi wa hadithi unachukua mikondo mingi ambapo nafsi zote tatu zinatumiwa pamoja na usimulizi kugeuka na kuchukua mitazamo tofauti. Pia, hakuna sauti moja inayoongoza bali sauti na mitazamo ya mwandishi na wahusika huchanganyika. (Khamis 2008).

Maudhui huwa hayaeleweki kwa urahisi. Jonathan Baumbach alisema katika hadithi fupi *The Return of Service* (1979), ‘utasoma hadithi siku hizi na sio hadithi tena tulizozoea.’

Wakati mwingine matini huvunjwauvunjwa na nafasi huwachwa katikakati. Nafasi hizo

zinaweza kujalizwa kwa kuwekwa ishara, mada, nambari, nukuzi, picha, michoro au hata kuwachwa wazi. Sim anamnukuu Federman (1957) anayesema kuwa nafasi hizo zinaweza hata kujazwa na vitu ambavyo havina uhusiano na kazi husika. Mfano mzuri ni kazi iitwayo *Willie Masters' Lonesome Wife* (1967) na William Gass. Katika kazi hii mwandishi anatumia rangi na fonti tofauti tofauti.

Ritgerotil (2006) anaeleza mtindo wa uchopekaji wa simulizi kuwa unasababisha fasihi kuwa katika vipandevipande, wala hakuna mshikamano tuliokuwa tumeuzoea. Mawazo kama hayo yanatolewa na Sim (2001:127) anayesema uchopekaji wa simulzi usababisha fasihi kukosa ukamilifu na hitimisho kama sifa linalohusishwa na hadithi za zamani. Uchopekaji wa simulizi unafanya usimulizi kutofululiza na matukio kutapakaa kila pahali.

### **2.3.4.3 MWINGILIANO MATINI**

Kulingana na Barry (2002) sifa mojawapo wa kazi za kibaadausasa ni mwingiliano matini. Hali ya kazi za kifasihi kutegemeana na kurejeleana. Kwa mujibu wa Kehinde (2003) mtindo huu unahusishwa na nadharia ya mwingiliano matini iliyoanzishwa miaka ya 1960. Mihimili mikuu ya mwingiliano matini ilifafanuliwa na Northrop Fryes na Julia Kristeva. Julia Kristeva anafafanua maana ya mwingiliano matini hivi:

Matini yoyote ile ni mkusanyiko wa unukuzi, ufyonzaji au mgeuzo wa matini nyingine ya awali. Mkusanyiko huo uungana na kisha kuunda kazi jipya (TY).

Sawia na Julia Kristeva, Kehinde (2003) anamnukuu Terry Eagleton (1983) anayesema kazi za fasihi ni uandishi mpya wa kazi zilizoandikwa awali. Kwa hivyo kulingana na Eagleton kazi zote za fasihi tunazosoma sio mpya bali zilikuwa zimeandikwa. Mwingiliano matini ni ufafanuzi wa dhana zilizoandikwa kwa njia tofauti au dhana geni ili kuchukua nafasi za dhana zilizopitwa na wakati. Aghalabu, ufafanuzi wa M. H. Abrams ni mwafaka katika utafiti wetu:

Mwingiliano matini ni mmojawapo wa njia bunilizi za kutunga kazi za fasihi huku ukirejelea kazi zingine. Njia hizo ni pamoja na matumizi ya unukuzi, madondoo, vidokezo, sheria sawa na usimilishaji wa mitindo ya kazi awali (Kehinde 2003) (TY).

Mwingiliano matini vilevile unamaanisha mwachano baina ya matini na msomaji.

Umberto Eco anasema kuwa sio kweli kusema kuwa matini zinaandikwa na mwandishi bali matini hujiunda zenyewe. Kwa hivyo hakuna matini inayojisimamia bali inategemea matini mengine.

Mwingiliano matini imejitokeza katika fasihi simulizi za Afrika. Hii ni kwa sababu fasihi simulizi ni mali ya jamii na hivyo basi ni ya kila mtu tofauti na fasihi andishi. Fasihi simulizi hupitishwa kwa njia ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Finnegan 1970:36)

Vilevile waandishi wa Afrika hutumia mwingiliano matini. Hii ni kwa sababu tamaduni zinafanana katika jamii za dunia na hii inawafanya kurejelea kazi za tamaduni zingine. Pia wanadamu kwa ujumla wana shida za kiuchumi, kisiasa na kijamii zinazofanana na hivyo kazi zao za fasihi kukaribiana. Kwa ujumla fasihi yoyote huchibuka kutoka fasihi nyingine na si kutoka ombwe tupu. Hivyo basi waandishi hurejelea maudhui na mitindo za waandishi wengine, hasa katika enzi hii ya utandawazi na uwingi tamaduni (Kehinde 2003 akimnukuu Biodun Jeyifo, 1988: 277). Waandishi wa Afrika wanaweza kurejelea ama kazi za wengine, kazi zao wenyewe (walizoandika awali) au fasihi simulizi. Kwa mfano Chinua Achebe katika *Arrow of God* anarejelea drama za matambiko (*Egwugwu - Masquerade*) za Kiafrika, methali na sherehe za kitamaduni (*Akwu Nro*). Ni kutokana na mwingiliano matini hii ya mazingira na tamaduni mbalimbali za fasihi simulizi, Chinua Achebe anaboresha kazi yake. Urejeleaji wa waandishi wengine unadhihirishwa kupitia Ngugi wa Thiongo *A Grain of Wheat* ambaye maudhui makuu ya Usaliti na Udhulumu yanafanana na maudhui ya kitabu cha mwandishi Conrad *Under Western Eyes*. Mifanano

hii ya maudhui katika riwaya hizi mbili inadhihirisha shida za binadamu zinafanana na hazitegemei tamaduni, jiografia wala tabaka.

Walibora (2012) anaoyesha mwingiliano matini katika riwaya zake za *Siku Njema* na *Kidagaa Kimemwozea*. Walibora alirejelea riwaya yake ya awali ya *Siku Njema* pale aliposhabisha tabia za Mzee Kazikwisha na Mtemi Nasaba Bora (uk.128). Katika *Kidagaa Kimemwozea* Mtemi Nasaba Bora anamwambia Amani amchimbie kaburi ili azikwe afapo. Sawia na hayo, Mzee Kazikwisha katika *Siku Njema* anampa mhusika mkuu Kongowea maagizo yayo hayo (uk. 100).

Kwa mujibu wa Anton Pokrivčák mwingiliano matini unaweza kuundwa katika fasihi kupitia njia zifuatazo: urejeleaji, dokezo, unukuzi , urudiaji wa maneno ya wengine, wizi wa maandishi au mawazo ya mtu, kolaji na mbinu inayohusisha matumizi ya uandishi upya wa matini ya awali kwa kuweka mandhari tofauti kitamaduni na kilugha.

Umuhimu wa mwingiliano matini ni kwa wanahistoria na wahakiki wa fasihi. Kutokana na mtindo huu wanaweza kufafanua uhusiano uliopo baina ya waandishi mbalimbali na fasihi zao. Kwa kufanya hivi fasihi itaweza kueleweka kama tendo la kibinadamu lililoko na majukumu katika jamii.

#### **2.3.4.4 UIGAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI**

Kama tulivyotanguliza hapo awali, imani za kipindi cha usasa zilisababisha kutokea kwa sanaa ya juu iliyosisitiza ubunifu na ugeni wa kila msanii. Kwa hivyo ilifika wakati ambapo ubunifu ulidhaniwa umekwisha na kufika tamati kwa sanaa. Ni hapa ndipo mtindo huu ulibuniwa na wanabaadausasa ili kuepukana na kufa kwa sanaa. Kwa mujibu wa Best na Keller (1991) wanaubaadausasa walizitisha dhana za ubunifu na ugeni katika

kazi za sanaa na badala yake kubuni mtindo wa uigaji wa kazi zingine pamoja na sifa zao. Miongoni mwa sifa hizo ni uigaji wa kazi zingine pamoja na mitindo yao. Kwa mfano Robert Rauschenberg alikutanisha matini kutoka magazeti na picha mbalimbali ili kuunda kazi mpya na wasanii kama Andy Warhol, Sherrie Levine, Cindy Sherman, Braque na Picasso kukutanisha nyimbo mbalimbali za zamani ili kuunda nyimbo mpya.

Kulingana na Ritgerotil (2006) mtindo huu ni uigaji wa kazi zingine au mitindo iliyotumika katika kazi hizo. Jameson katika makala yake *Postmodernism* anafafanua mtindo huu kuwa ni msingi mkuu wa kazi za kifasihi. Jameson anaiita mbinu hii *parody* wazi; uigaji bila tashtiti yoyote inayodhihirika katika *parody*. Kazi za kisanaa za kibaadausasa zinachukua haki miliki za waandishi wa zamani na kuiga kama kazi mipya za kibaadausasa. Hapo awali mtindo huu ulikuwa kama wizi lakini katika kipindi cha ubaadausasa umekubalika. Vilevile Rigerotil (2006) anasema kuwa, mtindo huu umetumiwa na filamu ya *The Simpsons*. Matukio mengi ya filamu ya *The Simpsons* imeiga kazi zingine kama vitabu, sinema na matukio ya kihistoria.

Kwa mujibu wa Sim (2001) mitindo hii ni kuchanganya tanzu na mitindo mbalimbali katika kazi za fasihi. Ilitokana na kuvunjika moyo kuwa kila kitu kimeshabuniwa na kimeshafanywa, Fredrick Jameson anasema katika kitabu chake *Postmodernism and Consumer Society (1983)*:

Waandishi na waimbaji wa ubaadausasa hawawezi kubuni mitindo mipya....ni kidogo tu kinawezekana; sababu ni kuwa imeshabuniwa tayari. Kwa hivyo badala ya kuandika kwa mitindo bunilizi wao ukutanisha mitindo iliyopo katika fasihi na kufanya kuwa kazi zao asilia (Sim 2001) (TY).

Sim anatoa mifano ya waandishi wa kibaadausasa ambao wametumia mtindo huu. Kwa mfano *The Hawkline Monster* (1974) na Richard Brautigan, *Yellow Back Radio Broke-Down* (1969) na Ishmael Reed, *The Place of Dead Roads* (1984) na William Burroughs.



Vilevile Childs na Fowler (2006) wanahoji kuwa kazi zinazotumia mtindo huu huwa zimeundwa kwa upande mkubwa na maneno, virai, sentensi, aya, mizani na onyesho kutoka kazi zingine. Mtindo huu hufanya kazi husika kuonekana kama zilinukuliwa kutoka kazi za watu wengine.

## **2.4 HITIMISHO**

Sura hii imejadili vipengele vya ubaadausasa katika muktadha wa tasnifu hii. Vipindi mbalimbali vya historia ya dunia hadi kufikia kipindi cha ubaadausasa vilijadiliwa kwa kina. Tulifafanua kuwa kipindi cha ubaadausasa kilichipuka kutokana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kisiasa na kisayansi katika jamii. Ni kutokana na mabadiliko hayo ndipo wataalamu walizua nadharia ya ubaadausasa ili kuelezea jamii hiyo.

Kwa upande mwingine, tulifafanua dhana ya nadharia ya ubaadausasa kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali na tofauti baina ya vipindi vya usasa na vipindi vya ubaadausasa. Fauka ya hayo tulijadili waasisi wakuu wa nadharia ya ubaadausasa wakiwemo Lyotard, Baudrillard na Jameson. Zaidi ya hayo tuliangalia kwa undani matumizi ya nadharia ya ubaadausasa katika fasihi.

Katika sehemu ya mwisho, tuliangalia mitindo ya ubaadausasa katika kazi za fasihi. Ni hapa ndipo tulijadili kuwa mitindo hii ilichipuka baada ya wanausasa kulekeza imani zao za sanaa ya juu. Hii ilipelekea kubuniwa kwa mitindo ya ubaadausasa tuliyojadili kwa kina: simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi.

## **SURA YA TATU**

### **SIMULIZI NDOGO NDOGO NA UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI KATIKA NYIMBO ZA KIKALENJIN**

#### **3.0 UTANGULIZI**

Sura hii imechanganua nyimbo za Kikalenjin za K21 kwa kuzingatia mihimili ya simulizi ndogo ndogo na uchopekaji wa vipande vya simulizi. Katika kufanya hivyo sura hii imetimiza lengo la pili kwenye tasnifu hii. Kwa mujibu wa Carter (2006) na Barry (2002) simulizi ndogo ndogo ni mhimili unayohusishwa na mfaransa Francis Lyotard. Lyotard alibeua simulizi kuu zilizokuwa zinakandamiza na kupendelea simulizi ndogo ndogo. Kwa hivyo simulizi ndogo ndogo ni msingi wa kusuluhisha matatizo maalum yanayowakumba watu mahususi katika jamii.

Kulingana na Lewis (2001) uchopekaji wa vipande vya simulizi ni upinduaji wa nyenzo ambazo zilikuwa zimezoeleka za akina Plato na Aristotle, katika uwasilishwaji wa kazi za sanaa. Nyenzo hizo ni pamoja na ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Katika Ploti, hakuna mantiki katika mpangilio wa matukio na visa. Mintarafu ya kazi za kibaadausasa, wahusika na mandhari hubadilika ghafla, maudhui huwa changamano na sio rahisi kuyaeleza juu yake.

### **3.1 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA SIMULIZI NDOGO NDOGO**

Kama nilivyotanguliza hapo awali, dhana hii ya simulizi ndogo ndogo imewekwa msingi imara na Mfaransa Francois Lyotard. Lyotard alipinga matumizi ya simulizi kubwa zilizokuwa zinakandamiza maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu simulizi kuu hazina uhusiano wowote na historia halisi. Kwa hivyo, Lyotard alipendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo zinazosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha. Simulizi hizi ndogo huzingatia maslahi ya watu binafsi na kufanya simulizi zao kukubalika. Aidha, ni katika simulizi ndogo ndogo ambapo watu hueleza mitazamo yao kuhusu mambo yao halisi (Carter 2006; Barry 2002).

Katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21, maudhui hujitokeza kwa kuangalia jinsi simulizi kuu zinavyopingwa; na mahala pake kuchukuliwa na simulizi ndogo ndogo. Katika uchanganuzi wetu wa nyimbo hizi, maoni ya wataalamu wafuatao yalifaa utafiti huu: Mikhail Bakhtin, Michel Foucault, Deleuze, Felix Guattari na Louis Althusser. Bakhtin alisema kuwa lugha yoyote ile lazima itumike katika jamii mahususi. Nyimbo ambazo zilichanganuliwa katika utafiti huu zimetumia lugha ya Kikalenjin inayohusishwa na jamii ya Kikalenjin. Foucault katika utafiti wake alidhihirisha jinsi mamlaka kuu inavyoweza kuwatenga punguani, wagonjwa, maskini, wahalifu na

wapinga desturi. Diskosi yoyote ile, kama asemavyo Foucault, haitenganishwi na mamlaka kwa sababu ni kama njia ya uongozi katika taasisi yoyote. Diskosi hii huamua jinsi ya kuzungumza, njia muafaka ya ukweli, nani anafaa kuongea na ni wapi panafaa paongewe. Katika uchanganuzi wetu tuliangalia jinsi mamlaka kuu zilivyoundwa na kuwatenga watu wengine na jinsi inavyokataliwa katika simulizi ndogo ndogo.

Maoni ya Deleuze na Guattari yalifaa uchanganuzi huu. Deleuze na Guattari waliangalia jinsi tamaduni mbalimbali zilivyochanganyigana na kuunda tamaduni nyingine tofauti. Ni katika muktadha huu ambapo tuliangalia jinsi nyimbo za Kikalenjin zilivyodhihirisha mgongano kati ya tamaduni kongwe na za juu na kisha utamaduni wa ubaadausasa ambao unaelekea kukinzana na ule wa kijadi.

Louis Althusser alidhihirisha jinsi mamlaka makuu yanavyoundwa katika jamii. Ni katika mamlaka haya ambapo imani za simulizi kuu zinaendelezwa. Maoni ya Louis Althusser yalituwezesha kuchanganua nyimbo za Kikalenjin katika mamlaka makuu manne (Wegesa na Machariah 2008):

1. Dini
2. Taasisi za binadamu
3. Elimu
4. Kaida za siasa

Sehemu zinazofuata zinaangazia namna nyimbo teule zinavyoelekea kupinga waziwazi mamlaka makuu ya kijamii ambayo tangu jadi yamekuwa yakienziwa na kuthaminiwa na wanajamii. Katika kufanya hivyo, sehemu hii itatosheleza lengo la pili la tasnifu hii la

kuchanganua kipengele cha simulizi ndogo ndogo katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21.

### 3.1.1 DINI

Dini ni mojawapo ya simulizi kuu zilizopingwa na Lyotard (Barry 2002). Lee (2009) akimnukuu Ingraffia anasema kuwa katika kipindi cha usasa, dini imekuwa ikienziwa na wanadamu na kuchukuliwa kama chemichemi ya ukweli. Mtazamo huu umebadilika katika kipindi cha ubaadausasa mintarafu ya sababu zifuatazo:

- Katika dunia ya ubaadausasa hakuna ukweli kamili au ukweli wa Bibilia, na hata ukweli huo hauna uhusiano na uhalisia. Kwa hivyo mafunzo ya dini hayaaminiki tena.
- Imani za dini katika dunia ya kibaadausasa zinakataaliwa. Hii ni kwa sababu imani za dini kama maandiko matakatifu, maombi, ushuhuda, maungano, historia ya kanisa na mikutano ya kanisa zinatiliwa shaka. Fauka ya hayo, matini ya Bibilia hayaaminiki hasa kwa sababu Lyotard katika *Postmodern Condition* alisema nadharia na utekelezi wa ufasiri wake haiaminiki. Zaidi ya hayo, Lyotard alikataa mfumo wa hekima wa makubaliano.
- Vile vile katika dunia ya ubaadausasa mtazamo wa aina moja umechukuliwa na mitazamo ya aina nyingi. Kwa hivyo imani za dini za aina moja haziruhusiwi bali kila mtu ana ruhusa za kuwa na mitazamo yake.

Upingaji wa simulizi kuu ya dini katika nyimbo za Kikalenjin za K21 ulidhihirika kupitia wimbo wa Kipkurui Ngeny *Pastor (Mhubiri)*. Wimbo huu ni mfano maalum wa namna nyimbo zinavyoweza kubeua kanuni za kidini hasa inapotokea kuwa waliopewa mamlaka

ya dini hutenda mambo ambayo ni kinyume na misingi ya dini. Uteuzi wa mada wa wimbo huu *Pastor (Mhubiri)* unaashiria mamlaka mkubwa sana katika dini. Matarajio yetu ni kuwa wimbo huu utazungumzia vitendo vyema vilivyotendwa na mhubiri. Lakini kama wimbo unavyodhihirisha mhubiri huyu anatenda kinyume na matarajio yetu. Ni kutokana na vitendo hivi viovu wimbo huu unasawiri, ndipo taswira ya ubaadausasa unajengwa, yaani upingaji wa dini na hivyo basi kupendekeza njia mbadala.

Katika mfano huu wa wimbo wa Kipkurui Ngeny *Pastor (Mhubiri)* simulizi kuu ya dini imesawiriwa kupitia mhubiri aliyekuwa akiwadhulumu wafuasi wake: kwani mhubiri huyu anasingizia mkutano kwa wafuasi wake bila kuwajulisha waume zao kama inavyojitokeza katika mistari ya 2, 3 na 4:

**MA**

2. Kiagwon pastor kutil tuiyet kocho konyu!
3. Kiagwon pastor kutil tuiyet kocho konyu!
4. Ak komamwoo, sarishet!

**MP**

**Nilishangaa mhubiri anapangia mkutano kwangu!**  
**Nilishangaa mhubiri anapangia mkutano kwangu!**  
**Na alikuwa hajaniambia, huo ni unyang'anyi!**

Katika mistari hii mhubiri anaelekea kutumia mamlaka yake visivyo kwani anautisha mkutano kwa mwanamke bila kumjulisha bwana yake. Na hii inamfanya mhubiri huyu kuonekana kama mnyanganyi (mistari 4). Lakini hata hivyo kuuitisha mkutano iwapo kuna dharura unaruhusiwa, japo mhubiri huyu anaitisha mikutano mingi na kuja kushiriki kwa 'mambo mengine'. Hili linadhihirika katika mistari ya 9, 10 na 11:

**MA**

9. Mayaa sine kebwa tuyet
  10. Lakini yaa ngebwa ngalek alek
  11. Mameche kuchang'a tuyosiek
- 'Mambo mengine' yaliyotajwa katika mistari wa 10 ni yale yanayokiuka mafundisho ya

**MP**

**Si vibaya wakija mkutano**  
**Ni vibaya wakija mambo mengine**  
**Sio vizuri kuwa na mikutano mingi**

dini. Kwani baada ya mhubiri huyu kuusingizia mkutano kwa mmojawao wa mfuasi

wake, anaenda kukaa na mke wa mtu hadi saa sita za usiku na kisha kusikika wakiongea kwa furaha katika zizi la ng'ombe. Tazama mistari ya 19 na 20.

**MA**

19. Ako mie saa sita nebo kemoi  
20. Akase bik nyenyungusot ak komakwany

**MP**

- Ilifika saa sita za usiku**  
**Nasikia watu wakinong'onezana na hawafiki**

Kutokana na wimbo huu, bila shaka mhubiri huyu alikuwa anawanyanyasa wafuasi wake. Kwanza ni kuchagua wake za watu bila ya idhini za waume zao. Haheshimu ndoa. Pili mikutano hii ni mingi mno na kuwafanya mke na mume wasipate wasaa wa kuendesha mambo yao nyumbani. Mstari wa 25 unaonyesha jinsi mwimbaji anavyolalamikia usumbufu wa mhubiri huyu:

25. Ak kikuima pasto anun

**Mhubiri huyu amenisumbua sana**

Wimbo huu unadhihirisha kuwa lazima watu wakubaliana na kile asemacho mhubiri. Mhubiri anapoitisha mikutano, watu wanakubaliana naye bila pingamizi. Hii ni kwa sababu tangu kale watu wameamini mamlaka ya dini. Dini hahitaji maswali au kusaili kinachosemwa na viongozi wake. Na hii inafanya watu wahudhurie mikutano aliyoitisha bila pingamizi kwa mtawalia: angalia mstari wa 5.

**MA**

5. Kingotar tuiyet, kole mie lagat nebo kwonyit

**MP**

- Alipomaliza mkutano huo, akasema kesho yake**  
**kunamkutano mwingine wa akina mama pekee**

Hii ni dhana iliyoelezwa na Lyotard kuwa katika simulizi kuu, watu hushurutishwa kukubaliana na mamlaka kuu (Ritgerotil 2006). Ni mamlaka ya aina hii ambayo Lyotard anayapinga katika nadharia yake ya simulizi kuu. Kwa hivyo ni kupitia huu wimbo huu ambapo dini (simulizi kuu) inapingwa. Wanabaadausasa wanasema kuwa iwapo watu wataasi dini na watumie urazini na umantiki hali hii (mhubiri kudanganya) haingetokea na hivyo basi matatizo ya kijamii kuweza kusuluhishwa (Barry 2002).

Dini vile vile imedhihirishwa kama simulizi kuu kupitia wanawake ambao walikuwa wanaenda mkutanoni. Wanawake ambao walidanganywa na mhubiri wamedhihirishwa

kama watu wasioelewa dunia yao hasa kutokana na wao kuamini dini (simulizi kuu). Imani yao katika dini imewafanya kuwa na mtazamo finyu wa maisha na hata kukosa kuwajibikia familia zao kwani jukumu la kulisha watoto wanawaachia waume zao kama inavyobainika katika mstari wa 14:

**MA**

14. Ak koleche sibai lakok awe tuiyet

**MP**

**Na akaniambia niwalishe watoto**

Imani hizi katika dini zinawafanya waumini wadanganywe kwa urahisi na mhubiri. Kwa hivyo imani zao katika dini haiwasaidii bali inawakandamiza.

Wimbo huu unamdhihirisha mhubiri kama mtu mdanganyifu, mnyang'anyi, mzinifu na muongo huku wanawake (wafuasi wake) wakisawiriwa kama wajinga katika dini. Katika kufanya hivyo, wimbo huu ni mfano mwafaka wa upingaji wa simulizi kuu kuhusu dini. Hata maombi, ambayo kwa kawaida hutarajiwa yalete afueni maishani yanadhihakiwa kwa kuwa mhubiri anayeyatoa si mtumishi halisi wa Mungu kama anavyodai. Mistari ya 24, 36 na 37 inasema:

**MA**

24. Kingaitu kubere Bwana asibiwe

36. Ako tinye saet ake nebere simbarara! Simbarara!

37. Akole kasae tamirmiyet

**MP**

**Nilifika anasema Bwana asifiwe**

**Na anaomba simbarara! Simbarara!**

**Na anadai anaongozwa na roho mtakatifu**

Hapa, mhubiri anadhihirishwa kama mhusika asiyeleweka. Katika mstari wa 36 mhubiri anasawiriwa kububujikwa na maneno yasiyo na maana yoyote huku akidai anaongozwa na Roho Mtakatifu (mstari wa 37). Katika mstari wa 36, maneno hayo 'simbarara!', 'simbarara!' yanadhihirisha maombi hayaaminiki katika enzi ya ubaadausasa sawia na nguvu za Roho Mtakatifu. Wimbo huu unaonyesha kuwa imani katika dini haina maana hasa katika jamii ya kibaadausasa, iliyo na uwingi tamaduni na teknolojia. Katika dunia ya kisasa huwezi kuwa na mtazamo mmoja wa dini na kuwacha mitazamo mingine.

### 3.1.2 TAASISI ZA BINADAMU



Kwa mujibu wa North (1990), taasisi za binadamu ni mfumo wa kijamii unaotawala maisha ya binadamu. Mfumo huo unadhibiti tabia za wanajamii na huhusisha sheria ambazo binadamu hana budi kuziheshimu. Baadhi ya taasisi hizi ni ndoa na familia, dini, elimu, mifumo ya sheria, haki na jeshi, mashirika ya hospitali, mawasiliano na haki za binadamu. Kwa mujibu wa wanabaadausasa, taasisi hizi za kibinadamu ni visawa vya kipindi cha usasa. Hii ni kwa sababu taasisi hizi zinajitokeza kama simulizi kuu zinazokandamiza maisha ya binadamu. Kama nilivyotanguliza hapo awali, taasisi hizi za binadamu zilibuniwa kwa madhumuni ya kusuluhisha matatizo ya binadamu, lakini zilisababisha mateso na mahangaiko mengi sana. Chambilecho Karl Marx, kile ambacho kilikuwa kimeganda kimeyeyuka na kuwa hewa. Kwa hivyo kazi za kibaadausasa zinadhihirisha jinsi taasisi hizi za binadamu zinavyopingwa ili angalau njia mbadala hubuniwe (Bertens 1995). Kwa hivyo katika utafiti huu tuliangalia jinsi wimbo *Meyetegei Kiisoman (Nilidhani umesoma)* na Scholar Chepkorir unavyodhihirisha dhana hii.

Upingaji wa taasisi ya binadamu umedhihirishwa kupitia wimbo huu wa Kikalenjin: *Meyetegei Kiisoman (Nilidhani umesoma)* na Scholar Chepkorir. Wimbo huu unadhihirisha jinsi kijana alivyopinga taasisi zote zilizokuwa zinadhaniwa ni nyenzo muhimu ya maisha ya binadamu.

Kwa vyovyote vile imekuwa jambo la kiada vijana kunasihwa kuheshimu taasisi zote za binadamu duniani: shule, ndoa, dini, elimu, sheria na wazazi. Kulinga na Lyotard hizi ni simulizi kuu ambazo zinaleta ukandamizi wa binadamu na zinafaa kupingwa kwa vyovyote vile (Barry 2002; Carter 2006). Fasihi za kibadausasa zinadhihirisha upingaji wa taasisi hizi zilizozoeleka kama polisi, sheria, kanisa na elimu (Wegesa na Macharia

2008). Ni kupitia wimbo huu wa Chepkorir ambapo kijana huyu anadhihirisha upingamizi wa taasisi hizi zote za binadamu. Tazama mistari ya 7, 8, 9, 10 na 11.

**MA**

7. Kikimitei sukul, koraa kisererte
8. Kinamin mistake eng sukul
9. Keonun inyo kaa
10. Kinyikealda koraa tugaa
11. Keliban tukuk ab sukul

**MP**

- Ukiwa shuleni, hucusoma**  
**Ulifanya makosa shuleni**  
**Ulifukuzwa kuja nyumbani**  
**Lakini tena uliuziwa ng'ombe**  
**Ili wagharamie mali ya shule**

Wimbo huu unazungumzia jinsi wazazi wanavyogharamikia elimu ya watoto wao. Katika muktadha huu, wazazi waliuza ng'ombe ili mtoto wao apate elimu. Ingawa hivyo kijana huyu hakusoma alipofika shuleni kwani alifanya makosa yaliyosababisha afukuzwe shuleni. Kutokana na mkasa huo, wazazi wake kijana huyu waliuza tena ng'ombe wao. Badala ya kuthamini hisani anayotendewa na wazazi, kijana huyu alimbaka msichana wa kidato cha pili. Jambo linalomfanya apelekwe mahakamani. Baba wa kijana huyu hachoki na anagharamia faini kama wimbo unavyozidi kueleza:

**MA**

14. Ak nget lekwet ab form two
15. Itururu eng sukul, kenamin ak keratin
16. Koluban baba ngung

**MP**

- Halafu ukabaka msichana wa kidato cha pili**  
**Ulishikwa na ukafungwa**  
**Lakini baba yako aligharamia faini**

Hata hivyo alionewa huruma na akapelekwa na wazazi wake katika chuo kikuu. Na alipokuwa katika chuo kikuu aliiba na alishikwa na kupigwa. Baba yake alimpeleka hospitalini na kugharamia bili ya hospitali. Mistari ya 17, 18,19 na 20:

**MA**

17. Kikomi maiwech alak kecho
18. Kendain college
19. Iwe imande eng college ak ichorsee bet
20. Keberit keomisanin, konyait baba

**MP**

- Ulionewa huruma**  
**Na ukapelekwa chuoni**  
**Ulipokuwa chuoni tena ukaiba**  
**Ulishikwa na kupigwa, ukatibiwa na babako**

Kijana huyu alifunguliwa biashara nyumbani ili aweze kumudu familia yake. Lakini hata hivyo alianza kulewa chakari na kuanza kufilisisha duka lile. Mistari ya 21, 22 na 23:

**MA**

21. Kemutung inyo kaa, akinyoo chekeosung ak
22. Ak kenamun biashara kele siribe lekukuk
23. Inam ibukitate, iwe iker tuket

**MP**

- Ulipoletwa nyumbani ulionewa huruma**  
**Ulifunguliwa biashara wakidhani utajimudu na familia yako**  
**Ulianza kulewa, na ukapora duka**

Kijana huyu alipoishiwa alitoroka wazaziwe pamoja na familia yake. Familia yake iliteseka sana. Mistari ya 24, 25, 26 na 27:

**MA**

- 24. Ooh! Kikaisiwang itorokan eng gaa
- 25. Ibakachi babangung
- 26. kwondongung ak lekuk
- 27. Kosiririch ak saratiach eng kaa

**MP**

- Ooh! Ulipoishiwa na pesa, ukatoroka**
- Na ukawaacha wazazi wako**
- Bibi yako na watoto wako**
- Familia yako wakateseka**

Kwa mukhtasari kijana huyu aliwapinga wazazi wake japo aligharamiwa kila kitu

kuanzia karo ya shule, faini, bili ya hospitali na hata kufunguliwa biashara. Alikaidi elimu kwani hakusoma bali aliiba chuoni na hivyo kufungwa. Vilevile alikaidi tamaduni za jamii kwa kubaka msichana wa kidato cha pili. Alipinga taasisi ya ndoa kwa kuwacha familia yake na kutoroka.

Kama vile tulikuwa tumejadili hapo awali, hizi ni baadhi ya simulizi kuu zinazopingwa na Lyotard. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa upingaji wa simulizi kuu katika wimbo huu wa Chepkorir ni sawia na upingaji ulioendelezwa na Lyotard; hasa kwa sababu katika wimbo mzima kijana huyu amepinga taasisi zote za binadamu. Kulingana na Sim (2001) upingaji huu unaitwa upingaji wa kaida na iliendelezwa na mfalsafa mjerumani anayeitwa Friedrich Nietzsche aliyependekeza uchunguzi wa imani zote za binadamu. Hii ni kutokana na imani kuwa iwapo watu watapinga taasisi gandamifu na watumie urazini na umantiki hali hii ingeleta suluhisho kwa matatizo ya kijamii (Barry 2002).

### **3.1.3 ELIMU**

Elimu imefafanuliwa kama mchakato wa upashaji wa maarifa, ustadhi, mielekeo na maadili kwa ajili ya kufungamanisha mtu na jamii yake. Elimu ni maisha na huanza mtu azaliwapo hadi afapo. Kulingana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni, elimu inajumuisha mpango mahususi wa mawasiliano kwa lengo la kufundisha. Mpango huu ujumuisha mfumo wa elimu unaowekwa na serikali (Mukudi

2004). Kwa hivyo, elimu ni mojawapo wa mfumo wa maisha uliotawala maisha ya watu katika karne kadhaa zilizopita. Wanabaadausasa upinga matumizi ya mfumo huu wa maisha. Wao hudai kuwa mfumo huu unakandamiza maisha ya binadamu. Kwa mujibu wa Lyotard mfumo huo wa maisha ni sawa na simulizi kuu na zinapaswa kupingwa na mahala pake pachukuliwe na simulizi ndogo ndogo zinazoakisi maisha halisi ya binadamu (Barry 2002). Katika wimbo ufuatao tuliangalia jinsi simulizi kuu ya elimu ilivyopingwa na mahala pake pakachukuliwa na simulizi ndogo ndogo: *Kiomongu Subui (Nilitoka Asubuhi)* na Cyrus Langat

Katika muktadha wa kibaadausasa elimu ni simulizi kuu inayosababisha ukandamizaji wa binadamu. Kama vile wimbo huu wa Langat umedhihirisha elimu imesababisha matatizo chungu nzima sio tu kwa wasomi bali pia kwa wafadhili au wazaziwe. Tazama mistari ya 11 hadi 17:

**MA**

11. Okass amwawak sikik chu
12. Motohaltee tukukwak
13. Kasarii makumii kasit
14. Rabishek chekemeche,
15. Matos Kegilchikee somanet
16. Mamikie naakasee engclass
17. Ibwoo bak seretet

**MP**

- Msikize wazazi niwaambie**  
**Msiuze mali yenu**  
**Nyakati hizi hakuna kazi**  
**Pesa ndiyo tunahitaji**  
**Sio lazima ujikaze masomoni**  
**Na huelewi darasani**  
**Kwani italetta umaskini zaidi**

Elimu kulingana na wimbo huu wa Langat itasababisha umaskini wa hali ya juu. Iwapo wazazi watauza ng'ombe na mashamba yao kwa ajili ya masomo basi wataweza kuteseka zaidi hasa ikichukuliwa kuwa siku hizi hakuna kazi.

Vile vile elimu hii itasababisha wazaziwe kuwa wagonjwa hasa kutokana na wao kuuza mashamba yao ili kukusomesha kama inavyodhihirika katika mistari ya 26 hadi 32.

**MA**

26. Ongee bakakte baishek
27. Keekachi mbarenikwai

**MP**

- Tuwachane na wazee**  
**Tuwapatie mashamba yao**

28. Meche sikuim mianto
29. Akukichang koraa tugaa
30. Kiraa sikumandae eng sugul
31. Koraa komekasee eng class
32. Ohh ibu bak seretet

**Wataanza kuwa wagonjwa  
Na mifugo walikuwa wengi  
Halafu humalizi shule  
Na hauelewi darasani  
Inaleta umaskini**

Hapa, elimu itasababisha madhara badala ya faida. Hii ni kwa sababu wazazi kwa madhumuni ya kufadhili elimu watauza mashamba na ng'ombe wao na hivyo basi kuwafilisisha. Ni ufilisikishaji huu ndio unaowasababishia umaskini. Hiki ni kinyume na matarajio yao kuwa elimu ingewafaidi. Hii inaoana na kile Lyotard alijadili katika makala yake ya *Postmodern Condition*. Lyotard alisema kuwa elimu ni mfumo wa maisha wa kipindi cha kisasa na ulidaniwa na wanausasa kama Habermas ungesuluhisha matatizo ya kijamii. Madai hayo yaligeuka na kuwa kinyume chambilecho wimbo huu wa Cyrus Langat *Kiomongu Subui (Nilitoka Asubuhi)*. Ni kutokana na mahangaiko hayo ndiposa Lyotard alipendekeza simulizi ndogo ndogo zinazohakisi hali halisi ya maisha na hivyo basi kuleta suluhu.

Kulingana na Wegesa na Macharia (2008) kipindi cha usasa kilikuwa kinaficha ukweli halisia wa maisha na hivyo basi kupendelea simulizi kuu kama elimu zinazozuia utofauti. Ndiposa kijana huyu alipokuwa akitaka kuasi elimu alionekana kama amepotoka na akaitiwa *bamwai* Chumba ili aje amshauri asiache shule. Mistari ya 8, 9 na 10:

- MA**
8. Kobirchi simit bamwai, kolechi konyo Chumba
  9. konyokutikang lakwek, kokakubakach sugul
  10. Sikutachikee tianda, nataa kotalentainyu

**MP**

**Akampigia simu bamwai Chumba aje  
Amshauri mtoto wake kwa sababu  
alikuwa anataka kuacha shule  
Halafu aanze kuimba, ambayo ni  
talanta yake**

Hapa, kijana huyu alipokataa elimu, wazaziwe walimwona kuwa amekuwa mkorofi na hivyo basi akaitiwa mshauri ili aje kumshauri arudi shule. Kijana huyu alikuwa amekataa elimu ili aweze kuanza kuimba. Alikuwa anapenda uimbaji kwa sababu ulikuwa talanta yake.

Kulingana na Carter (2006) na Barry (2002) simulizi hizi kuu zitajidengua na kutafuta njia mbadala. Kwani kijana huyu aliweza kuingia taaluma ya uimbaji uliokuwa na manufaa kwake. Hata hivyo kijana huyu hakueleweka kutokana na imani za jamii katika elimu. Imani iliyolazimisha kila mtu kufuata bila pingamizi. Ni imani hizi Lyotard alikataa katika makala yake ya *postmodern Condition*. Mfumo huu wa elimu unachukua mawazo ya wale “waliodhaniwa” kuwa wanahekima katika jamii na kuwadunisha wengine kama kijana huyu (wanaodaniwa hawana hekima). Ni kutokana na mfumo huu ndipo simulizi kuu zinaundwa katika jamii. Simulizi hizi kuu zinatenga watu wengine katika jamii na hivyo basi kukosa kusikizwa na kuonekana kama ‘wakorofi’ wakikataa kufuata mfumo huo. Hii ilipelekea kijana huyu kuonekana kupotoka alipokataa kwenda shuleni; na mama yake kumwita mshauri ili amshauri. Ni kutokana na hali hii ambapo Lyotard alipendekeza mfumo tofauti wa ushirikiano ambao hutajumuisha kila mtu bila kujali umri, dini, siasa au hata elimu. Kwa hivyo kupitia mfumo huu ndipo wahusika kama kijana huyu watasikizwa licha ya elimu yao.

### **3.1.4 KAIDA ZA KISIASA**

Kwa mujibu wa Ernesto (1988:33) siasa za kipindi cha usasa zilikuwa na kaida za kusuluhisha matatizo yaliyokumba mwanadamu kwa ujumla. Walihimiza uhuru, majadiliano, makubaliano, usawa na haki kwa watu wote. Hata hivyo kaida hizi zilipingwa na wanabaadausasa kwa kuwa zilikuwa simulizi kuu zisizokidhi mahitaji ya watu mahususi na zinaficha ukweli. Hili limesababisha kukataliwa kwa mwamko wa kimataifa unaoahidi ukombozi na badala yake vikundi mahususi kubuniwa ili kutetea maslahi ya kibinafsi.

Kulingana na Sim (2001) wanabaadausasa wanashuku kaida hizi za kisiasa. Wao huona kuwa kaida hizi hazina maana katika maisha na zinafaa kutupiliwa mbali. Barry (2002) anasema kuwa iwapo watu wataasi kaida hizi na watumie urazini na umantiki hali hii ingeweza kuleta suluhisho kwa matatizo ya kijamii. Katika wimbo wa Jackline Memo *Osoruech Eng Mau (Mtuokoe Mau)* tunaona jinsi kaida hizi za kisiasa zilivyoleta mahangaiko katika maisha ya binadamu na kisha kupingwa ili mahala pake pachukuliwe na simulizi ndogo ndogo zinazoweza kuleta suluhisho.

Kutokana na wimbo huu wa Memo ni dhahiri kwamba raia wanateseka kutokana na kaida za kisiasa. Kaida hizo zilifanya watu kufurushwa kutoka msitu wa Mau na kukosa mahala pa kuishi. Mistari ya 9 hadi 12 inasema:

**MA**

9. Kikeonach kila okilel nee!
10. Kikoyalilcha biik cha chemitei Mau
11. Rirech cha ak kandoi, kirirchi oh!
12. Osoruech biik cha chemita mau

**MP**

- Wamekuwa wakifukuzwa kila siku.**  
**Watu ambao wanaishi Mau wameteseka**  
**Tunawalilia viongozi oh!**  
**Muwaokoe watu wetu wanaoishi Mau**

Katika mistari hii, inabainika kuwa watu ambao wanaishi msitu wa Mau wanateseka sana. Hii ni kwa sababu serikali iliwafurusha wakaaji hao kwa madhumuni ya kuhifadhi mazingira. Katika harakati hizo wakaaji wa Sekemiat, Siaraleon, Kaptai na Binech walifurushwa kama wimbo unavyoendelea kusema kwenye mistari ifuatayo:

**MA**

15. Yalilta yee oh, kandoi yaliltosh
16. Biik cho chemitei Sekemiat
23. Yaliltosh yee oh, kandoi yaliltosh
24. Biik cho chemitei Binech
31. Siaraleon, kandoi kirirchinok nkoo?
32. Omo kerech, kandoi kibendi ano?
39. Chemitei Kaptai, kandoi koyaltosh

**MP**

- Watu ambao wanaishi upande wa**  
**Sekemiat wanateseka**  
**Watu ambao wanaishi Binech wanateseka**  
**Viongozi tunawalilia**  
**Watu ambao wanaishi upande wa**  
**Siaraleon wanateseka, viongozi tutaenda wapi?**  
**Watu walioko Kaptai wanateseka**

Sheria hizo za kisiasa zilifanya watu ambao walikuwa wanaishi upande wa Sekemiat, Siaraleon, Kaptai na Binech kuteseka kwa kukosa pahala pa kuishi. Sheria hizi za kisiasa

ni simulizi kuu zinazojaribu kueleza ukuaji na ukamilifu wa binadamu. Asili ya sheria hizi zilikuwa za kimataifa zinazojaribu kuhifadhi mazingira kutokana na ongezeko la joto duniani. Hata hivyo juhudi za serikali za kutekeleza sheria hizi, zilisababisha matatizo mengi kwa wakahaji wa msitu wa Mau.

### **3.2 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA UCHOPEKAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI**

Kama nilivyotanguliza hapo awali, uchopekaji wa vipande vya simulizi ni upinduaji wa nyenzo ambazo zilikuwa zimependekezwa na akina Plato na Aristotle. Nyenzo hizo ni pamoja na ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Plato na Aristotle walidai kuwa ploti lazima iwe yenye muumano na muungano kuanzia mwanzo hadi mwisho, yaani vitendo katika ploti viwe na mwanzo, kati na mwisho vilivyokamilifu. Hata hivyo, kama inavyodaiwa na wanabaadausasa, imani hizo zimepitwa na wakati. Wanabaadausasa hupendelea njia tofauti ya kuwasilisha kazi ya sanaa ili kukidhi mahitaji ya hadhira lengwa. Ni uwasilishwaji huu ndio ulizua mhimili huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi. Katika mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi, kazi za kibaadausasa hazina mantiki katika mpangilio wa matukio na visa. Vilevile wahusika na mandhari hubadilika ghafla, maudhui huwa changamano na sio rahisi kuyaeleza juu yake (Lewis 2001; Tilak 1993).

Tulichanganua mhimili huu wa ubaadausasa katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Katika kufanya hivyo sehemu hii imekidhi lengo la pili la tasnifu hii la kuchanganua kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Kwanza, wimbo ulio na mada *Ibinu Kunur (Kizazi Kitovu)* na Millicent Jerotich, umetumia mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi kwa kuwasilisha jamii



nzima . Hii ni kwa sababu wimbo huu umetumiwa kusawiri maisha ya jamii nzima ya Kikalenjin; kuanzia watoto, wazazi, vijana hadi watu wazima. Vile vile wimbo huu umesawiri uovu wa aina tofauti tofauti uliokithiri katika jamii. Katika sehemu ya kwanza, wimbo huu unakashifu wazazi dhidi ya kuwa na tabia ambazo hazifai katika jamii zikiwemo kuparamia jikoni na mama mzazi. Wimbo huu unanza hivi, mistari wa 3 na 4:

**MA**

3. Kiaro baba Faith Komaut chepkubet ak kamit ye,  
koko yaa ye? Amungwae, aibu! Kwisha!

**MP**

**Nilimwona baba Faith akipigania jikoni na mamake nini hii? aibu! kwisha!**

4. Kiaro baba Faith Komaut chepkubet ak kamit ye,  
koko yaa ye? Amungwae, aibu! Kwisha!

**Nilimwona baba Faith akipigania jikoni na mamake nini hii? Aibu! Kwisha!**

Vilevile wimbo huu unakashifu mababu dhidi ya fitina, kwani fitina hii itasababisha mporomoko wa jamii. Mistari 7 na 8 inadokeza hivi:

**MA**

7. Iyaru koku konami fitina ak karu apwerit  
kutoit kebesho, aelewi rika!
8. Iyaru koku konami fitina ak karu apwerit  
kutoit kebesho, aelewi rika!

**MP**

**Utapata babu akifanya fitina Hadi wake wa nduguze wanakosana bure, haelewi rika!**

**Utapata babu akifanya fitina Hadi wake wa nduguze wanakosana bure, haelewi rika!**

Pia, wimbo huu umetumiwa kusawiri wasichana walio na tabia mbaya ya kuvaa nguo fupi. Mistari ya 11 na 12:

**MA**

11. Iyaru tiibik chailachi ngoriak cha nwaken,  
akole fashion funika uchi!
12. Iyaru tiibik chailachi ngoriak cha nwaken,  
akole fashion funika uchi!

**MP**

**Wasichana wanavaa nguo fupi ati ni mtindo wa kisasa, funika uchi!**

**Wasichana wanavaa nguo fupi ati ni mtindo wa kisasa, funika uchi!**

Aidha, wimbo huu umesawiri jamii iliyo na vijana ambao hawatekelezi wajibu wa ndoa bali wanaenda kulala mjini. Mistari ya 15 na 16:

**MA**

15. Murenik kutuka, obakach ruando centre kerke  
ak kokai chesebe, mayai akili kwisha!
16. Murenik kutuka, obakach ruando centre kerke  
ak kokai chesebe, mayai akili kwisha!

**MP**

**Vijana pevukeni, wacheni kwenda kulala mjini tabia hiyo ni sawa na kuku anayelalia mayai, akili kwisha!**

**Vijana pevukeni, wacheni kwenda kulala mjini tabia hiyo ni sawa na kuku anayelalia mayai, akili kwisha!**

Fauka ya hayo, wimbo huu umeonyesha jamii iliyo na itikadi ya uganga. Itikadi kuwa kuna dawa zinazoweza kuwatuliza wazee wanaofanya mapenzi nje ya ndoa. Mistari ya 19 na 20:

**MA**

19. Sikarun kelechets kionde TMM makitinye cha lee

kwanyik ap Kalenjin, shows denied

20. Sikarun kelechets kionde TMM makitinye cha lee

kwanyik ap Kalenjin, shows denied

**MP**

**Halafu tutaambiwa kuwa tumewapatia  
Dawa ya TMM (Tuliza Mzee Mkorofi)**

**Wanawake wa Kalenjin hatuna hiyo  
dawa, tunakataa madai hayo**

**Halafu tutaambiwa kuwa tumewapatia  
Dawa ya TMM (Tuliza Mzee Mkorofi)**

**wanawake wa Kalenjin hatuna hiyo  
dawa, tunakataa madai hayo**

Jamii iliyo na watu ambao hawafanya kazi ila kunywa pombe tu imesawiriwa katika wimbo huu. Mistari ya 23 na 24:

**MA**

23. Iwendi iyoru jito nee ngete asubuhi ak kuyee  
Maiyek kotomakungetke, bure kabisa!

24. Iwendi iyoru jito nee ngete asubuhi ak kuyee  
Maiyek kotomakungetke, bure kabisa!

**MP**

**Utapata mtu anaamka asubuhi na kwenda  
kunywa pombe hadi hajijui, bure kabisa!**

**Utapata mtu anaamka asubuhi na kwenda  
kunywa pombe hadi hajijui, bure kabisa!**

Hatimaye, Jamii iliyo na hali ya juu ya uasherati imesawiriwa kwani watu hutongozana mijini. Mistari ya 27 na 28.

**MA**

27. Iwendi town iyoru koinange altaeke biika  
borwee kwai, aibu kwisha

28. Iwendi town iyoru koinange altaeke biika  
borwee kwai, aibu kwisha

**MP**

**Ukienda mjini utapata watu wanashiriki  
katika usherati, aibu kwisha!**

**Ukienda mjini utapata watu wanashiriki  
katika usherati, aibu kwisha!**

Kwa muhtasari wimbo huu unadhihirisha mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi kwani unazungumzia mambo mengi kuhusu jamii nzima. Humo, twapata vipande vingi vya simulizi vinavyohusu watoto, wazazi, vijana, wasichana na kisha vipande vinavyosawiri uovu uliokithiri mjini na vijijini. Ni kama kwamba wimbo umechopeka ‘vijihadithi’ saba visivyomuwala kwa pamoja. Ni dhana hii iliyozungumziwa na Best na Keller (1991) walipomnukuu Jameson (1984) kuwa wanabaadausasa husawiri maisha mamboleo kwa matumizi ya vijihadithi vingi visivyoona na visivyo na mandhari mahususi. Maisha ya kisasa, kama ulivyo wimbo huu,

hayana hadithi iliyokamilika kiusimulizi. Badala yake, maisha ya kisasa yamejaa vijihadithi vilivyochopekwa hapa na pale.

Kipengele hiki cha uchopekaji wa vipande vya simulizi kinakinzana na kile Aristotle na Plato walikuwa wamependekeza kuwa lazima kazi za kisanaa ziwe na muumano na muungano kuanzia mwanzo hadi mwisho. Vilevile Aristotle alikataa uwingi wa matukio katika kazi za kisanaa. Aristotle alisawasisa kazi za kisanaa na viungo vya mnyama na kwamba lazima viuhusiane na kuwa haitawezekana kutoa kiungo kimoja bila kusasabisha maafa (Tilak 1993). Wimbo huu wa Millicent Jerotich *Ibinu Kunur (Kizazi Kitovu)* ni wa kisasa na hivyo basi kutupilia mbali imani hizo. Wimbo huu hauna muumano na muungano na mna matukio mengi ambayo hayahusiani. Inawezekana kutoa au hata kuongeza baadhi ya matukio bila kuathiri wimbo wenyewe.

Kulingana na Best na Keller (1991) Foucault anakiri kuwa jamii ya kibaadausasa ina uwingi wa mfumo wa hekima na hivyo basi kuhitaji matumizi ya usawiri ndogo ndogo. Usawiri huu hufanywa kupitia mtindo wa Uchopekaji wa vipande vya simulizi. Kwa hivyo matumizi ya mtindo huu huwezesha waimbaji wa Kikalenjin kusawiri hali halisi ya kijamii ya kibaadausasa ya Kikalenjin. Kwa hivyo kupitia mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi mwimbaji Millicent Jerotich aliweza kuonyesha maovu ya uasherati, uzembe, ufitina, na itikadi zilizopitwa na wakati yaliyokithiri miongoni mwa watoto, vijana, wasichana na wazee yote kwa pamoja.

Pili, mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya hadithi unajitokeza katika wimbo wa Cyrus Lagat ulio na mada *Kiomongu Subui (Nilitoka asubuhi)*. Katika utangulizi wa wimbo huu hakuna uhusiano mkubwa sana na wimbo wenyewe.

#### MA

1. Ooh! asaa Isimba aah kaa otkee
2. Meche siku tingwak, wee menye Kabisimba

#### MP

**Ooh! Huyu ni Isimba anataka kujiendeleza  
Anataka kuanza kuwaambia, anaishi**

**Kabisimba  
anataka kumdunga chui**

3. Che mekuruit kimagetit  
Mistari ya 1, 2, na 3 katika wimbo huu inazungumzia kuhusu Isimba ambaye anaishi Kabisimba na anataka kuendelea kwa kuimba. Vilevile anataka kumdunga chui. Mistari hii haina uhusiano na wimbo wenyewe unaohusu mwimbaji aliyekataa kwenda shule na kuanza kuimba. Mfano mwingine ni wimbo wa Diana Musila Chelele *Sugardaddy (Wazazi Bandia)*.

**MA**

1. Akole ah! Akole ah!
2. Mie barak kotit kotabe engweng dustin(shindwe)
3. tukuk chematileke kipkok
4. Kicham chichi anan kicham ngoroik

**MP**

**Akole ah! Akole ah!  
wasichana wadogo ambao wana  
uhusiano na wazee ni wengi  
wanapenda (wazee) kwa sababu  
ya kununuliwa nguo**

5. Kicham chichi anan kicham rabishek

**pamoja na kupewa pesa**

Mstari wa 1, hauna uhusiano wowote na wimbo huu hasa kwa sababu matamshi hayo haileti maana yoyote inayooana na maudhui ya wimbo huu ya wazee wanaodhulumu wasichana wadogo. Hayo ni sawia na maoni ya Ritgerotil (2006) ya kuwa kazi za kibaadausasa katika matukio au maelezo ya kwanza huwa haina uhusiano na matukio mengine, dhana ambayo inajidhihirisha katika nyimbo hizi. Utangulizi wa aina hii unaathiri wimbo vipi?

Kwa mujibu wa Mwamzandi (2013) fasihi mamboleo zina ugumu kwa hadhira lengwa hasa kutokana na mitindo mamboleo inayotumiwa kuiwasilisha. Msikilizaji sharti asikilize kwa umakinifu na kukubali kuzugwa pale inapobidi. Sanaa nzuri ni ile itakayomlazimisha msikilizaji kusaili ishara tofauti tofauti zilizo kwa wimbo na kisha kuzihusisha ishara hizo na muktadha wa maisha yake halisi. Hatimaye, ufaafu wa sanaa huamuliwa na namna itakavyomtumikia yule anayelengwa. Hivyo basi utangulizi huo kuwa na maana kwa msikilizaji.

Tatu, mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi unadhihirika katika nyimbo za Kikalenjin za K21 kupitia michanganyo ya vijitanzu. Michanganyo ya vijitanzu ni ile itakayojumuisha mbinu za kuelezea dunia ya sasa iliyojaa miujiza na mambo mengi ambayo hayawezi kueleweka kwa njia iliyo rahisi. Vijitanzu ambavyo vimeonekana kutumiwa na waimbaji wengi wa Kikalenjin ni utumaji wa Salamu na mazungumzo ya simu. Utumaji wa salamu ni sifa mojawapo inayojitokeza katika nyimbo za Kikalenjin na unahusishwa na ubaadausasa. Sababu ni kuwa njia hii huvuruga maudhui ya wimbo husika na mpangilio wa wimbo uliozoeleka. Mfano wa wimbo uliotumia mtindo huu wa utumaji wa salamu ni wimbo wa Paul Subembe Lagat *Club City*:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
24. Club city bar ooh	<b>Kilabu cha Club City ooh!</b>
25. Chorwenyu nemita Boomet	<b>Rafiki yangu kilicho Boomet</b>
26. Kuu mambo yote kabisa	<b>Ni mambo yote kabisa</b>
27. Ak kotache taik	<b>Na kinakaribisha wageni</b>
28. Akokatwa Belie	<b>Unimsalimie Belie</b>
29. Ako ng'imeche parking nebo garit, kokararan	<b>Hata ukitaka maegesho ya magari, ni mazuri</b>
30. Kuribun komei garing'ung kotiwe komei	<b>Watakuchungia gari lako hadi uende vizuri</b>

Mstari wa 28, *Akokatwa Belie (Unimsalimie Belie)* ni ujumbe uliotolewa na mwimbaji ili mtu anayeitwa Belie asalamiwe. Nyimbo ambazo zilitumia mtindo huu wa utumaji salamu ni pamoja na Cyrus Langat *Kiomongu Subui (Nilitoka Subui)* mstari wa 7, Mika Maritim *Katabugan (Shida)* mistari ya 83 hadi 86 na Kipkurui Ngeny *Pastor (Mhubiri)* mistari ya 41 hadi 69. Hii ni mtindo uliosawia na ufafanuzi wa Best na Keller (1991) wanaosema kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi upinga mfufulizo wa fasihi (wimbo) na badala yake kupendelea mitindo isio na mpangilio. Aidha, Lewis (2001:128) anasema kuwa ni jukumu la wasikilizaji kuunganisha vipande hivyo ili kupata maana. Katika wimbo uu huu wa Paul Subembe Lagat *Club City*; mazungumzo ya simu yametumiwa vilevile. Tazama mistari ya 76 hadi 87:

**MA**

76. Kuu bikap baishek tugul ak restaurant
77. Ntomo bitu toloo oyee
78. Alakini mamwai kit neyaa
79. Okimit baishet
80. Til ooh Makiche sio obir,
81. Kawek ii?
82. Halo?
83. Yes service neba Club City ii sir
84. Koboiboyet eng service nekikonuu
85. Ak koraa eeh
86. Ngosukan biik chebunn Nairobi
87. Kumakosanii tuguk chekalat

**MP**

**Watu wote wa vilabu na hoteli  
Kusiwe na msukosuko  
Lakini hata hivyo sitaongea vibaya  
Fanyeni kazi  
Kata simu Makiche halafu nikupigie,  
Unaona nini?  
Halo?  
Ndiyo, huduma ya Club City bwana  
Ni furaha kwa huduma yao wanayotoa  
Na pia eeh!  
Watu wanaotoka Nairobi wakishuka  
Hawatakosa vyakula vilivyotiwa rangi**

Hapa, mwimbaji anazungumza na mhusika wa kiubunifu anayeitwa Makiche (mstari wa

80). Mwimbaji anamjulisha mhusika huyu kuhusu huduma zinazopatikana katika kilabu kitwacho *Club City*. Kilabu hiki kinapatikana mjini Bomet na panauuzwa vinywaji na vyakula. Zaidi ya hayo mwimbaji huyu anamjulisha kuwa abiria wanaotoka Nairobi wakishuka hawatakosa vyakula vilivyotiwa rangi (mstari wa 87). Ni mabadiliko hayo ya matumizi ya teknolojia ndio yanahusishwa na mtindo huu wa ubaadausasa. Mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi usawiri jamii ya kibaadausasa jinsi ilivyo kwa kutumia mazungumzo ya simu. Mawazo hayo yanashadidiana na Best na Keller (1991) wanaosema kuwa matumizi ya teknolojia yalisababisha kuvunjavunja tamaduni, dhana inayojitokeza katika wimbo huu.

Nne, mtindo huu wa uchopekaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo za Kikalenjin za K21 zinaonekana kupitia miundo ya nyimbo. Mtindo wa uchopekaji wa vipande vya simulizi huhusisha ukiukaji wa ploti uliozoeleka (Lewis 2001:127) wa akina Plato na Aristote. Aristotle alipendekeza kazi ya kisanaa kuwa na utangulizi, kati na hitimisho. Utangulizi, kazi ya sanaa lazima iwe na mwanzo unaoweza kueleweka bila kutegemea chanzo kingine. Kati, kazi ya sanaa ni sharti ioane na vitendo tangulizi na vitendo vitakavyofuata baadaye. Mwisho au tamati, kazi ya sanaa ni lazima ioane na utangulizi na kati, na kumalizika kwa furaha (Tilak 1993). Hivyo basi, katika fasihi za mamboleo,

mtindo uliozoelekeka wa fasihi kumalizika kwa furaha ili kujenga maudhui fulani hubezwa kwa kutumia majadiliano pale wahusika wanapojadiliana kuhusu yale wamejifunza katika nyimbo. Katika kuchanganua dhana hii tulitumia mfano huu wa wimbo wa Bamwai Yegon *Toyon Beek (Maji ni ya Kila Mtu)*. Wimbo wenyewe umegawanyika katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza (mistari ya 1 hadi 60) mwimbaji anajadili kuhusu imani za jadi kuwa mwanamke ni wa jamii nzima. Wimbo unadokezwa hivi:

**MA**

1. Kikamwaa baishek kule
2. Iman toyon beek
3. ak kora ayan
4. Ikiyee tugul eeh
5. shika shika shika
6. Kikamwaa baishek kule
7. Iman toyon beek
8. ak kora ayan
9. Ikiyee tugul eeh
10. ibut ibut kebut ibak

**MP**

**Wazee walisema kwamba  
Ni ukweli maji ni ya kila mtu  
Na nilikuwa karibu nikubali  
Wote tunakunywa eeh  
Shika shika shika  
Wazee walisema kwamba  
Ni ukweli maji ni ya kila mtu  
Na nilikuwa karibu nikubali  
Wote tunakunywa eeh  
Chuna chuna tuchune basi**

Hapa, mwimbaji anazungumzia jinsi wazee walipendekeza kuwa wanawake ni wa jamii nzima. Wanaposema kuwa maji ni ya kila mtu wanamaanisha kuwa mwanamume anaweza kuzini na mwanamke yeyote. Kwa ufupi kila mwanamume anaweza ‘kuchuna’, mwanamke yeyote, chambilecho mstari wa 10. Hata hivyo mwimbaji anatupilia mbali imani hizo kuwa hazifai katika dunia ya nyakati hizi:

**MA**

48. Lakini makukasiri is
49. Kikeng nekaba baishek
50. Lakini kasari kukiit tioniki nebele kutit

**MP**

**Lakini si nyakati hizi  
Ilikuwa nyakati za wazee wetu  
Lakini nyakati hizi majitu ya mdomo yamefika**

Katika mistari hii, mwimbaji anasema kuwa imani za kuzini na mwanamke yeyote hazifai nyakati hizi. Sababu anayotoa ni kuwa nyakati hizi majitu ya mdomo yamefika. Anachomaanisha mwimbaji ni kuwa katika dunia ya kisasa magonjwa ya zinaa yamezuka.

Katika sehemu ya pili (mistari ya 61 hadi 88) wimbo unachukua mwelekeo wa majadiliano. Hapa mhusika anayeitwa Joseph arap Teso anajadiliana na mwimbaji yale waliyojifunza katika wimbo huo. Wanajadiliana hivi:

**MA**

61. Joseph arap Teso, akasee
62. Makaechintosh beek kasari
63. Kabere mie straw makiheng
64. Komi sumuk kora
65. Amu beek cheikulu eng teret kochunto kora
66. Melen ngibaishe straw komatinyin kutit
67. Kabare makumeche kutiny glassit nekae chito
68. Mhh ano kiro tero neeto imuchi  
koroche ak kung'uti
69. Ikul akinye, akonamin karasta akolal kutit
70. Kikuwalak oh,
71. Menget soo?
72. Kitomoo anai
73. Nae ibak
74. Kakul aketugul terenyi
75. Ak kwam chitugul maingenyi
76. Kaekass anun, Kanyabro eng
77. Kapketet komenye Kaptirmit mie stage ooh
78. Kialel anee anerech kole
79. Baishek eeh ima toyoi beek
80. Kiyee tugul eeh
81. Kiker kochorwe Kipsonai kokete Tinai
82. Ak kochohajike Kisumu ooh
83. Kerke kira Sikibo ak sigirok itiaribik tugul koraa
84. An kii Bamwai kiabere kikule maikuete
85. Beek ab kimagetich?
86. Kikass kole mie korenyu beek ab kimagetok?
87. Metebbe mondoi
88. Ak korko mondoi

**MP**

- Joseph arap Teso, ninasikia**  
**Usinywe maji ya mtu nyakati hizi**  
**Nilidhani unaweza kunywa na *straw***  
**Kuna sumu vilevile**  
**Kwa sababu maji unayokunywa ni yale**  
**yale yaliyo mtungini**  
**Usidhani ukitumia *straw* haiwezi**  
**gusana na mdomo wako**  
**Nilidhani hufai kuguswa na gilasi**  
**uliyonywea maji**  
**Vilevile mtu anaweza kunywa kutoka mtungi**  
**huo na kutemea mate**  
**Halafu wewe unywe na ushikwe na**  
**kansa ya mdomo**  
**Dunia imebadilika oh**  
**Hujui yaani?**  
**Nilikuwa sijajua**  
**Jua basi**  
**Kila mtu anywe kutoka mtungi wake**  
**Na kila mtu ale asali iliyoko kwenye mzinga wake**  
**Umesikia Kanyabro huko?**  
**Kapketet akiishi huko Kaptirmit katika Stage**  
**Mimi nilitaka kukasirika**  
**Wazee wakasema maji ni ya kila mtu**  
**Tunakunywa wote**  
**Ukiona mto Kipsonai ukitiririka kuanzia Tinai**  
**Hadi Kisumu ooh**  
**Ni sawa na Punda**  
**Binamu nilidhani walisema hawakatai**  
**Maji ya chui?**  
**Umesikia maji ya chui yanapatikana kwangu?**  
**Uliza *Mondo***  
**Na bibi wa *Mondo***

Kulingana na majadiliano hayo, mwimbaji anazungumza na mhusika ambaye anaitwa

Joseph arap Teso (mistari wa 61). Mwimbaji anamwambia Joseph arap Teso asifanye mapenzi na mtu ambaye si mpenzi wake nyakati hizi, hasa kwa sababu ya kuzuka kwa magonjwa ya zinaa (mistari wa 62). Naye Joseph arap Teso anauliza kama anaweza kutumia kondomu (*straw*) wakati wa kujamiiana (mistari 63). Mwimbaji anamkataza kwa sababu sio kinga kamili dhidi ya magonjwa ya zinaa. Hii ni kwa sababu kondomu



inaweza kupasuka wakati wa kujamiiana na hivyo basi kusababisha kuambukizwa magonjwa ya zinaa kama UKIMWI. Mwimbaji anasisitiza kuwa suluhisho kamili ni kuwa na uaminifu kwa mpenzi mmoja (mistari 75). Katika mistari ya 84 hadi 88 majadiliano kuhusu umuhimu wa kuwa na uaminifu kwa mpenzi mmoja yanamazilika kwa matumizi ya mtindo wa tashtiti. Joseph arap Teso anauliza kuwa alidhani hawakatai maji isiyo ya mtu (chui) (mistari 86), lakini mwimbaji anajibu ikiwa amesikia kama kuna maji isiyo ya mtu. Funzo ni kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja (usinywe maji ya mtu mwengine).

Sifa nyingine ya uchopekaji wa vipande vya simulizi na ambayo inajitokeza katika nyimbo teule ni ile ya ukosefu wa hitimisho maalum. Mtindo huu ulidhihirika katika wimbo wa Mika Maritim *Katabugan (Shida)* unaochukua mwelekeo wa Dadaist (1917) aliyetunga mashairi kwa kukutanisha sentensi zilizotolewa magazetini bila utaratibu maalumu (Barry 2002), Mwimbaji huyu, kama alivyofanya Dadaist, alikutanisha vijihadithi vitatu tofautitofauti kwa pamoja. Katika sehemu ya kwanza anatumia jinsi alivyopitia baiskeli (mistari ya 5 na 6), kupatana na mtu na kondoo kukimbia kuelekea mlimani (11 hadi 17), na mwishowe kupatana na afisa wa kilimo (mistari ya 58 hadi 61). Wimbo huu unakosa hitimisho maalum na katika uchanganuzi wetu tulizingatia kipengele hicho.

- |   |  |
|---|--|
| <b>MA</b>   | <b>MP</b>  |
| 5. Kianget besho eng Nyahururu kiabunati baskilit | <b>Niliamka wakati mmoja huko Nyahururu na kusafiri kwa baiskeli</b> |
| 6. kuchus baskilit yu                             | <b>Baiskeli yangu ilipata pancha</b>                                 |

Katika mistari hii ya 5 na 6, mwimbaji anatumia kuwa aliamka wakati mmoja asubuhi na kusafiri kwa baiskeli. Alipokuwa akisafiri baiskeli yake ikaharibika.

11. Kicho chi chokolekitio
12. Koleche taabu gani?
13. Kiatonon ak alubjan
14. Alache amune sijuba ilache itabugan?

**mtu akaja karibu nami.  
Akaniuliza nilikuwa na taabu gani?  
Nilisimama na kukasirika  
Mbona ananitusi kwa kuniambia taabu  
gani?  
Nani mwenye shida baiskeli au mimi?  
kondoo alikimbia  
kuelekea mlimani**

15. Ane nekataabugan anan katabugan baiskelilit
16. Kolaban kechiryet gei kwua
17. Ngerita eng tulwet

Hapa, mwimbaji anatuambia mtu alikuja na kumwuliza alikuwa na shida gani. Mwimbaji hajetuambia huyu mtu alitoka wapi? Alikuwa akifanya nini? Kasha kondoo alikimbia kuelekea mlimani. Huyu kondoo alitoka wapi? Moja kwa moja mwimbaji anatuelekeza yale yaliyofanyika katika sehemu za Longisa Bomet:

58. Sikoekenchebaboishe eng koling ba
59. Longisa, eng Bomet
60. Kikulechi kimite ak Mambet
61. Kinete chi neba agriculture

**Hii ni sawa na yale ambayo  
Yalifanyika huko Longisa Bomet  
Tukiwa na rafiki yangu Mambet  
Wakati ambapo wazee walikuwa  
Wakifunzwa na afisa wa kilimo**

Katika mistari hii, mwimbaji anatusawiria kuhusu mafunzo ya kilimo huko Longisa Bomet. Mafunzo hayo yalikuwa yakiendelezwa na afisa wa kilimo. Hata hivyo mafunzo hayo hayana uhusiano na sehemu iliyotangulia, kupitia baiskeli na kukutana na mtu na kondoo.

Lewis (2001:127) anasema kuwa wanabaadausasa hushuku ukamilifu na mahitimisho yanayohusishwa na hadithi za zamani za kina Plato na Aristotle. Wanabaadausasa hupendelea matumizi ya mahitimisho mengi na hukataa hitimisho la aina moja. Dhana hii inadhihirika katika wimbo huu kutokana na ukosefu wa kuwepo kwa hitimisho la aina moja. Kwa mfano mwimbaji huyu alipokuwa akipitia baiskeli yake na kupata pancha, alifanya nini? Baiskeli yake ilichukuliwa na nani? Yule mtu aliyekutana naye alifanya nini baadaye? Kwa hivyo kutokana na wimbo huu ni dhahiri kwamba kuna uwezekano wa mahitimisho kadha wa kadha ambayo wasilikizaji wangeweza kuyatoa. Lakini je, mahitimisho hayo yana umuhimu gani kwa hadhira lengwa?

Best na Keller (1991) wakimnukuu Nietzsche (1967:326) katika mtazamo wake anasema kuwa hakuna ukweli wa dunia bali tulionayo ni ufasiri wake tu. Kwa hivyo dunia ina fasiri nyingi sana ambayo uwasilishwa kupitia mtindo wa uchopekaji wa vipande vya simulizi. Fasiri hizi hutunenepesha kiakili na kihakima kuhusu dunia yetu. Ni hapa ndipo nyimbo za Kikalenjin huwa haina hitimisho maalum na hazilengi kuhodhi ukweli kama zilivyo simulizi za jadi za akina Plato na Aristotle ambao wanazungumzia ngano kuu za wafalme kama kina Edipode. Nyimbo za Kikalenjin zina mawezekano chungu nzima na hivyo basi kuzipatia wasikilizaji jukumu la kujitafsiria maana ya wimbo wenyewe. Hii ni muhimu kwani itakidhi mahitaji ya kila msikizaji kutegemea imani na filofosofia anazotumia katika maisha yake. Kwa hivyo wimbo wa Mika Maritim *Shida (Katabugan)* una mahitimisho mengi na hivyo basi kutosheleza mahitaji ya wasikilizaji mbalimbali. Hatimaye, kulingana na Lewis (2001:127), kazi za kibaadausasa zinavunjwavunjwa na nafasi huachwa katikati. Nafasi hizo zinaweza kujalizwa kwa kuwekewa ishara za maneno mbalimbali, mada, nambari, unukuzi, picha, michoro au hata kuachwa tu. Katika utafiti huu tulitumia wimbo wa Faith Chepkurui *South Afrika (Afrika Kusini)* ili kudhihirisha jinsi waimbaji wanavyotenganisha ‘vijihadithi’ vyao kwa kutumia ishara mbalimbali za maneno. Ishara hizi ziliwawezesha kusawiri dunia ya kibaadausasa iliyojaa mambo mengi. Katika wimbo wa Faith Chepkurui mwimbaji huyu ameziba nafasi hizo kwa kutumia ishara za maneno, tazama mistari ya 10 na 15:

### MA

1. I my people
2. Thank you for the support
3. You are giving to us as the musicians
4. I congratulate my mentor Chelele,
5. The biginner of the south African beats
6. In our region
7. It has changed our style and fashion
8. Even to, dancing upcoming dotcom generation

### MP

- Nyinyi watu wangu**  
**Ninawashukuru kwa usaidizi wenu**  
**Mnayotupatia sisi waimbaji**  
**Ninampongeza mnasih wangu Chelele**  
**Mwanzilishi wa mitindo mamboleo kutoka Afrika**  
**Kusini**  
**Katika sehemu yetu**  
**Imebadilisha mitindo yetu**  
**Katika uchezaji wa muziki wetu**

9. This is Therui band
10. Pamba sana wapi nduru, aya! Aya!  
Sawa! Sawa!
11. Diana Chelele neketing tingiza
12. Tunishek chebo South Afrika
13. Ikastai ano nedurundoo
14. Taman chamakse ak Dj Kipro
15. Iyee iyee lee lee
16. Kongoi Chelele amu kinetech tunishek
17. Ab South Afrika
18. Ndemaieye tostomo kenai tunishek
19. Ab South Afrika

- Hii ni bendi ya Therui**  
**Pamba sana wapi nduru, aya! Aya!**  
**Sawa! Sawa!**  
**Diana Chelele ndiye aliimba *tingiza***  
**Mitindo mamboleo kutoka Afrika Kusini**  
**Unasikiaje mitindo hiyo**  
**Ni nzuri sana na Dj Kipro**  
**Iyee iyee lee lee**  
**Asante Chelele kwa kutufundisha mitindo hii**  
**Kutoka Afrika Kusini**  
**Kama si wewe hatungekuwa tumejua mitindo hii**  
**Kutoka Afrika Kusini**

Mwimbaji huyu ametumia mstari huu wa 10 ili kujalizia pengo baina ya mistari ya 9 na

11. Hii ni kwa sababu mwimbaji huyu katika mistari ya 1 hadi 9 alikuwa anajadili hoja tofauti na ya kuanzia mistari ya 11. Katika mistari ya 1 hadi 9 mwimbaji alikuwa anashukuru mashabiki wake kwa usaidizi wao kwa waimbaji (mstari 2). Fauka ya hayo anamtambua mwimbaji anayeitwa Diana Chelele kwa kuwa mwanzilishi wa muziki mamboleo kutoka Afrika Kusini (mstari 5). Hii ni tofauti na hoja inayopatikana kuanzia mistari wa 11. Katika mstari huu mwimbaji anamtaja Diana Chelele moja kwa moja kuwa yeye ndiye aliimba nyimbo za *tingiza* ambazo ni muziki mamboleo kutoka Afrika Kusini. Zaidi ya hayo anasema kuwa muziki huo ni mzuri sana na unachezwa na Dj Kipro. Kutokana na maelezo hayo ni bayana kuwa mstari wa 10 ulitumiwa na mwimbaji makusudi kujalizia nafasi hiyo. Mstari huu ulimwezesha mwimbaji kuwasilisha hoja zake japo mstari wenyewe hauchangii hoja hizo moja kwa moja. Pia katika wimbo uu huu wa Chepkurui mstari wa 15 ulitumiwa na mwimbaji ili kujalizia pengo baina ya hoja za mistari ya 11-14 na 16-19. Kama nilivyotanguliza katika mistari ya 11-14, mwimbaji anamtaja moja kwa moja Diana Chelele kuwa yeye ndiye aliimba nyimbo za *tingiza* ambazo ni muziki mamboleo kutoka Afrika Kusini. Zaidi ya hayo anasema kuwa mitindo hiyo ni nzuri sana na inachezwa na Dj Kipro. Hoja hii ni tofauti na ile ya mistari ya 16-19 inayotoa shukrani kwa Diana Chelele kwa kuwafundisha muziki mamboleo kutoka

Afrika Kusini. Vilevile anasema kuwa kama haingekuwa Diana Chelele kuleta mitindo hiyo hawangekuwa wameijua. Kwa hivyo mstari wa 15 ulitumiwa na mwimbaji kwa lengo la kujalizia nafasi hiyo. Mstari huu ulimwezesha mwimbaji kuwasilisha hoja zake barabara. Kama nilivyotanguliza kuwa wimbo huu ni wa kibaadausasa na mwimbaji alitumia ishara hizi za maneno ili kutenganisha hoja au ‘vijihadithi’ vyake katika mistari ya 24, 35, 44, 53 na 63. Kama asemavyo Lewis (2001) mtindo huu unagawa kazi katika vijihadithi mbalimbali vilivyowazi na visivyokamilika. Kwa hivyo matumizi ya ishara hizi za maneno zimeuwezesha mwimbaji kusawiri hoja nyingi kuhusu mwimbaji Diana Chelele. Vilevile mtindo huu kulingana na Lewis udhoofisha maudhui katika fasihi hadi ni vigumu kuelewa inazungumzia nini. Wimbo huu wa Chepkurui unasawiri mambo mengi sana kuhusu Diana Chelele na huwa vigumu kueleza kwa ufupi kile kitu kinachozungumzia.

### **3.3. HITIMISHO**

Katika sura hii ya tatu tumechanganua kwa kina vipengele vya simulizi ndogo ndogo na uchopekaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Katika uchanganuzi wa kipengele cha simulizi ndogo ndogo, tulichanganua nyimbo kwa kuzingatia mamlaka makuu manne ya dini, elimu, taasisi za binadamu na kaida za kisiasa. Ni katika mamlaka haya ndipo tulibainisha jinsi imani za simulizi kuu zilivyoendelezwa. Vilevile tulidhihirisha jinsi mamlaka haya yalivyokandamiza maisha ya binadamu na hivyo basi kubuniwa kwa simulizi ndogo ndogo. Simulizi hizi ndogo ndogo zilipendekezwa na Lyotard kama suluhu kamili kwa matatizo ya kisasa ya kibinadamu.

Kipengele cha uchopekaji wa vipande vya simulizi kimejitokeza kikionyesha jinsi kipengele hiki kinavyopindua nyenzo ambazo zilikuwa zimependekezwa na akina Plato na Aristotle. Tulibainisha jinsi nyimbo za Kikalenjin za K21 zinavyochopeka vijihadithi vingi visivyomuwala pamoja. Halikadhalika nyimbo zilizo na tangulizi zisizooana na wimbo wenyewe, nyimbo zilizochanganya tanzu kwa kutumia utumaji wa Salamu na mazungumzo ya simu na kuwa na ukosefu wa hitimisho maalum pamoja na ploti isiyo na muumano na muungano. Hatimaye tulibainisha jinsi nyimbo za kibaadausasa zinavyovunjwawunjwa na nafasi huachwa katikati. Nafasi hizo hujalizwa kwa kutumia ishara mbalimbali za maneno.

## **SURA YA NNE**

### **MWINGILIANO MATINI NA UIGAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI KATIKA NYIMBO ZA KIKALENJIN**

#### **4.0 UTANGULIZI**

Sura hii imehakiki nyimbo teule za Kikalenjin kwa kuangalia mihimili ya mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi. Katika kufanya hivyo, sura hii imetimiza lengo la tatu la tasnifu hii. Katika sehemu ya kwanza tumechanganua nyimbo zinazodhihirisha kipengele cha mwingiliano matini. Hii imefuatwa na sehemu ya pili tuliyo changanua kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi.

Kwa mujibu wa Child na Fowler (2006) mwingiliano matini ni dhana inayotumiwa kuelezea matini yoyote yawe nyimbo, riwaya, au hata filamu yanayorejelea matini mengine ambayo kwa njia moja au nyingine huchangia utunzaji na maana ya matini hayo. Katika sura hii tuliangalia namna nyimbo za Kikalenjin zilivyorejelea matini za awali na hivyo basi kuchangia utunzi na uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo hizo. Kati

ya mambo tuliyoangalia ni pamoja na urejeleaji wa simulizi za jadi za Kikalenjin, methali, tasbihi, Bibilia na Katiba ya Kenya. Aidha, tulibainisha jinsi nyimbo za Kikalenjin zinavyorejelea nyimbo nyingine.

Kwa upande mwingine kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi kinarejelea kazi zozote zilizoundwa kwa upande mkubwa na maneno, virai, sentensi, mistari, aya, mizani, na hata onyesho kutoka kazi nyingine (Child na Fowler, 2006). Aidha, kipengele hiki huhusisha uigaji wa ploti na mitindo ya kazi za waandishi wengine. Uigaji wa vipande vya simulizi hufanya kazi husika kuonekana kama zilionukuliwa kutoka kazi za watu wengine. Katika sura hii tumechanganua nyimbo za waimbaji mbalimbali zilizodhihirisha mistari na ploti zilizofanana. Aidha, tulichanganua nyimbo za waimbaji waliotumia mitindo ya kisengere nyuma na utumaji wa salamu kwa mashabiki.

#### **4.1 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA MWINGILIANO MATINI**

Katika sehemu hii tumechanganua nyimbo za Kikalenjin za K21 kwa kuangalia mielekeo miwili. Mwelekeo wa kwanza unahusu mwingiliano matini wa nyimbo za Kikalenjin na tanzu zingine. Tanzu hizo tulizoangalia ni pamoja na simulizi za jadi za Kikalenjin, methali, tasbihi, Bibilia na Katiba ya Kenya. Katika sehemu ya pili tumeangalia jinsi mwingiliano matini unavyojitokeza wakati nyimbo mahususi za Kikalenjin zinaporejelea nyimbo nyingine.

Kwa mujibu wa Fairclough (1992) Julia Kristeva ndiye anayedhaniwa kuwa mtaalamu wa kwanza aliyebuni dhana hii ya mwingiliano matini. Kulingana na Kristeva matini yoyote yale ni unukuzi, ufafanuzi na urejeleaji wa matini mengine ya awali. Kwa hivyo mwingiliano matini ni dhana inayotumiwa kuelezea matini yoyote yawe nyimbo, riwaya, au hata filamu yanavyorejelea matini mengine. Mtindo huu wa mwingiliano matini

ulichipuka baada ya wanausasa kulekeza ubunifu na upekee wa kila msanii (mwandishi). Chimbuko la wingimatini kama dhana unatokana na imani za wanabaadausasa walioshikilia kuwa mfumo wa lugha umekuwepo tangu kale, na hivyo basi chochote tunachokisema huwa tayari kimeshasemwa na wale waliotutangulia. Hivyo basi matini yoyote huwa mkusanyiko wa matini ya awali kuanzia kiwango cha virai hadi utanzu mzima.

Ijapokuwa dhana hii ya mwingiliano matini ina misingi yake katika muktadha wa Kimagharibi, sio mgeni katika fasihi za Kiafrika. Miongoni mwa sifa zingine, fasihi za Kiafrika hazimilikiwi na watu binafsi, yaani ni mali ya jamii. Fauka ya hayo, hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Finnegan 1970). Fasihi za Kiafrika zinahusishwa na mwingiliano matini, hasa kutokana na sababu zifuatazo:

- Kwanza, utamaduni ni sawa miongoni mwa watu wa Afrika, kwa hivyo kazi zao zinaelekea kufanana.
- Pili, shida na changamoto za binadamu zinafanana duniani nzima na hivyo basi kazi zao zinafanana au zinajadili maudhui sawa.
- Fasihi haitokani na ombwe tupu. Fasihi huibuliwa kutoka fasihi zingine.

Ni kutokana na sababu hizo ambapo tunaweza kuziangalia nyimbo za kileo za Kikalenjin kama mfano madhubuti unaodhihirisha dhana hii ya mwingiliano matini kutokana na kurejelea simulizi za jadi za Wakalenjin. Katika kufanya hivyo, sura hii inazingatia madhumuni mahususi ya utafiti ya kuchanganua kipengele cha mwingiliano matini katika nyimbo teule za Kikalenjin.

Fairclough (1992) amemnuuu John Fiske ambaye anatofautisha aina mbili za mwingiliano matini: matini wima na matini mlalo. Mwingiliano matini wima ukiwa ni



urejeleaji wa matini kutoka tanzu tofauti, kwa mfano nyimbo kwa Biblia huku mwingiliano matini mlalo ni urejeleaji wa matini kutoka tanzu sawa, mfano nyimbo kwa nyimbo nyingine. Kutokana na maoni hayo ya Fiske, tumechanganua nyimbo za Kikalenjin kama zinavyojitokeza hapa chini:

#### **4.1.0 UREJELEAJI WA SIMULIZI ZA JADI ZA KIKALENJIN**

Kulingana na Nwachukwu-Agbada (2000:122) mwingiliano matini wima hujitokeza pale fasihi mamboleo zinaporejelea vijitanzu mbalimbali vya fasihi simulizi, tamaduni, mila na desturi za jamii. Miongoni mwa vipera hivyo ni visasili, hekaya, methali, hurafa, ngano na imani katika uchawi na ushirikina. Katika utafiti huu tuligundua kuwa nyimbo zilirejelea simulizi za jamii ya Kikalenjin. Simulizi ni mojawapo wa tanzu kuu ya fasihi simulizi za Kikalenjin. Tanzu zingine ni nyimbo, methali na vitendawili. Simulizi hizi zilikuwa na sifa mbalimbali. Kati ya sifa hizo ni kuwa zilikuwa na mianzio maalum. Kwa mfano, *En kasarta age kimi chi... (Hapo zamani za kale palikuwa na mtu...)*, *Kitun (anan yetun) ko kimi Kiplengwet ak Muryat... (Hapo zamani palikuwa na sungura na panya...)*. Wahusika wakuu katika simulizi walikuwa wanyama. Aidha, simulizi zilikuwa mali ya jamii na hivyo basi kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na zilikuwa zina maadili kwa wanajamii (Chesanai 1991). Uchanganuzi wa wimbo wa Bamwai Yegon *Toyon Beek (Maji ni ya kila mtu)* umebainisha kuwa umerejelea simulizi maalum ya jamii ya Kikalenjin. Simulizi iliyorejelewa ni *Toyon beek, beek ap Kimaketit anan Kocheptibi (maji ni ya kila mtu na hayafai kuhodhiwa)*. Kwa mujibu wa Chesanai (1985) simulizi hii ni ya zamani sana na ilikuwa inatumiwa na jamii kuhimiza ushirikiano na umoja katika jamii. Kwa mfano wanawake hawakuwa wanahodhiwa na mtu yeyote. Mwanamume angeweza kujitosheleza kimapenzi na mwanamke yeyote. Hata hivyo,

kama asemavyo Chesanai, simulizi hii imepitwa na wakati na inafaa kutupiliwa mbali katika dunia ya kibaadausasa.

Wimbo wa Bamwai Yegon *Toyon Beek (Maji ni ya kila mtu)* unarejelea ngano hii ya *Toyon beek, beek ap Kimaketit anan Kocheptibi (maji ni ya kila mtu na hayafai kuhodhiwa)*. Hii inadhihirishwa na mada ya wimbo, *toyon beek (maji ni ya kila mtu)*. Kama wimbo unavyobainisha, simulizi hii ni ya jadi sana, hasa pale wimbo unaposema kwenye mstari wa 1 ‘wazee walisema’. Matumizi ya wakati uliopita (LI) katika neno ‘walisema’ unaonyesha sifa mojawapo ya simulizi ya ‘hapo zamani paliondokea...’. Katika mstari wa 2, wimbo huu unafafanua simulizi hii moja kwa moja kuwa *iman toyon beek (ni ukweli maji ni ya kila mtu)*.

**MA**

1. Kikamwaa baishek kule
2. iman toyon beek

**MP**

**wazee walisema kwamba  
ni ukweli maji ni ya kila mtu**

Katika mistari hii, wimbo wa Yegon unadhihirisha kuwa simulizi hii ilikuwa inaendeleza imani kuwa mwanamke si wa mtu yeyote, bali ni wa jamii nzima (mistari ya 1 na 2). Fauka ya hayo, imani hizo ziliendelezwa pale wazee walipodai kuwa maji hayo hayawezi kumalizika. Tazama mstari wa 19:

**MA**

19. kikale matar matar

**MP**

**walisema hatamaliza hatamaliza**

Katika mstari wa 13 hadi 18, mwimbaji anatuambia alikuwa ameo na akasafiri. Aliporudi, rafiki yake alikuwa amefanya mapenzi na bibi yake. Alipowauliza wazee, akaambiwa kuwa maji ni ya kila mtu na hayataisha (mwanamke ni wa kila mtu na hawezi kumilikiwa na mume mmoja):

**MA**

13. awe safari kuhee chorwa nyu
14. ibut ibut kebut ibak
15. kikabal besho kisima
16. kutakomon beek
17. arute weyan

**MP**

**Nilienda safari na rafiki yangu akanywa maji yangu  
Chuna chuna tuchune basi  
Nilichimba siku moja kisima  
Hadi maji yakatoka  
Nikalala mahali**

18. kuhee chorwa nenyu

**Rafiki yangu akanywa**

Hapa, mwimbaji anatuambia kuwa alikuwa ameo (mistari 15 na 16). Baada ya kuoa alienda safari (mistari 13). Alipokuwa safarini rafiki yake akazini na bibi yake. Matumizi ya uradidi katika mistari wa 14 unasisitiza imani za simulizi hii ya Kikalenjin. Imani zinazokubali kuwa mwanamke si wa kumilikiwa na mume mmoja bali ni wa jamii nzima. Kama asemavyo Chesnai kuwa simulizi hii imepitwa na wakati na inafaa kutupiliwa mbali, Jeyifo (1988:277) naye anafafanua katika muktadha wa mwingiliano matini, kuwa kazi za kibaadausasa zinarekebisha kazi za awali na kuziboresha kwa kutupilia mbali imani potovu. Wimbo wa Yegon unabainisha hoja hii, pale anaposema:

**MA**

- 35. marani betushechu wee
- 36. makehe tugul
- 37. kuit korasta nebele kutit
- 38. swele kutit, swele bak swele bak

**MP**

- Lakini si nyakati hizi**
- Hatunywi wote**
- Kumefika saratani ya mdomo**
- Choma mdomo, choma basi choma basi**

Hapa, mwimbaji anadhihirisha kuwa imani zilizoendelezwa na simulizi hii ya kufanya mapenzi na mwanamke yeyote zimepitwa na wakati. Katika mistari wa 35, Yegon anasema kuwa nyakati hizo zimepitwa na wakati. Hii ni kwa sababu katika dunia hii ya kibaadausasa kumefika saratani ya mdomo, inayochoma mdomo. Hapa saratani ya mdomo imetumiwa kwa maana ya magonjwa ya zinaa kama vile UKIMWI. Ule msisitizo unaopatikana katika mistari wa 38 umetumiwa kama tahadhari ya hatari inayoweza kumsibu yule ambaye hatajikinga katika nyakati za hivi leo zilizojaa magonjwa ya zinaa ya kila aina.

#### **4.1.1 UREJELEAJI WA METHALI**

Wimbo wa Yegon una mwingiliano matini na methali za jamii ya Wakalenjin. Kulingana na Chesaina (1991) methali za jamii hutumiwa na wazee kupitisha ujumbe kwa lugha ya mkato ili kuwaelekeza vijana na kutatua shida za kijamii. Nyenzo muhimu pia katika methali za Kikalenjin ni lugha inayotumiwa. Lugha inayotumiwa katika

methali za Kikalenjin ni lugha ya kijazanda. Sababu ya kutumia lugha ya kijazanda ni kuweza kupitisha ujumbe kwa njia wazi bila kukirihisha hisia. Yegon alitumia methali ya Kikalenjin kuwahimiza wanaume kutoshiriki katika mapenzi na wanawake wengi:

**MA**

75. Ak kwam chitugul maingenyi

**MP**

**Na kila mtu ale asali iliyoko kwenye mzinga wake**

Hapa, mstari huu wa 75 ni methali ya Kikalenjin. Mstari huu *ak kwam chitugul maingenyi (na kila mtu ale asali iliyoko kwenye mzinga wake)* ni methali iliyo na maana ya wazi na maana ya ndani. Maana ya wazi ni kuwa kila mtu ale asali aliyorina kutoka kwa mzinga wake. Maana batini ni kuwa kila mwanamume anafaa awe mwaminifu kwa mkewe wa ndoa bila ya kuzini. Hivyo basi neno *maingenyi (mzinga)* limetumiwa kijazanda. Neno hili linamaanisha mwanamke na limetumiwa ili kupitisha ujumbe bila kukirihisha hisia za watu au wanajamii.

Halikadhalika, mwingiliano matini unajitokeza nyimbo teule za Kikalenjin zinaporejelea methali za Waswahili. Methali za Waswahili ni msemo wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahususi, unaokumbukika na unaokusudiwa kuelekeza, kuadibu, kusuta na kushauri (Wamitila 2003). Uchanganuzi wa wimbo wa Diana Chelele *Sugardaddy (Wazazi Bandia)* unadhihirisha madai hayo unaporejelea methali ya Waswahili katika mistari ya 24 na 25:

**MA**

24. Kimakekenu kele tendet ore tab garit ab mat

25. Ak kobune garit ab mat ak kolai masikek

**MP**

**Hawakusema uongo njia ya reli ni nyembamba**

**Lakini gari moshi linapita na linabeba mizigo**

Mistari hii imeundwa kutokana na methali ya Kiswahili inayosema- *usione wembamba wa reli gari moshi linapita*. Kutokana na methali hii mwimbaji ameweza kusawiri ujumbe wa wimbo wake sawasawa. Madhumuni ya Chelele kutumia methali hii katika wimbo wake *Sugardaddy (Wazazi Bandia)* ni kutuonyesha jinsi wasichana wadogo

wanavyokubali kuhusiana na wazee wakubwa na hivyo basi kudhulumiwa kimapenzi na kutumiwa kama vyombo vya burudani. Cheroni anadokeza hivi:

**MA**

2. Tibik chemengech chechamsot ak baishek
3. Tukuk chematileke (kipkok)!
4. Kicham chichi anan kicham ngoroik?
5. Kicham chichi anan kicham rabishek?
8. Beste korot nekikobok kelek!
9. Darling korot nekiko yatyatek(sikiriyet)!
10. Aiktwek doubling eng keyisyek
11. Iyos kora akot kosir babanguk

**MP**

**Wasichana wadogo wanaohusina na wazee Bure kabisa!**  
**Mnawapenda au ni kwa ajili ya kununuliwa nguo?**  
**Mnawapenda au ni kwa ajili ya kupewa pesa?**  
**Hati ni rafiki, kijizee ambacho meno yameisha!**  
**Tena kimeishiwa na nguvu!**  
**Tena umri chake kinazidi wako maradufu**  
**Zaidi ya hayo ni jizee kuliko babako mzazi**

Hapa, Chelele anashangaa ni kwa nini wasichana wadogo wanahusiana na wazee ambao hawana meno na hata nguvu zimewaishia. Vilevile umri wao ni zaidi ya baba mzazi. Wasichana hawa wadogo wanakubali kuhusiana na wazee wanaowazidi kwa umri kwa sababu ya kununuliwa nguo na kupewa pesa. Wasichana hawa wadogo wanapokubali kuhusiana na wazee hawa, wanadhulumiwa mintarafu ya mistari ifuatayo:

**MA**

18. Kuwek iche cheitururu eng sukul
19. Ikaji rabishek kosir sikik

**MP**

**Kinyume chake vizee hivi huwatorosha shuleni**  
**Na kuwapa pesa nyingi**

Katika mistari hii, wasichana hawa wanatorosha shuleni na kupotoshwa kwa kupewa pesa nyingi. Fauka ya hayo wasichana hawa hupelekwa sehemu za burudani kama inavyofafanuliwa na mistari ifuatayo:

**MA**

39. Nendeitetei bar Langat
40. Ibere komite tuiyet ab sikik
41. Boiyot ake tukul ak lakwet (babies)

**MP**

**Na ukienda sehemu za burudani**  
**Utadhani kumekuwa na mkutano wa wazazi**  
**Kwani kila kizee kina kisichana kidogo**

Mwimbaji anasema kuwa katika sehemu za burudani kila mzee ameandamana na msichana mdogo. Sehemu za burudani zinajulikana kwa unywaji wa pombe. Bila shaka wasichana hawa wadogo walikuwa wakilewa. Ikumbukwe wasichana hao ni wadogo na kwa hali halisi hawafai kwenda sehemu hizi za burudani ila wanafaa kuwa shuleni

wakisoma. Huu ni upeo wa juu jinsi wasichana wadogo wanavyodhulumiwa na wazee. Isitoshe, mwimbaji anatusawiria jinsi wazee huwapotosha wasichana hawa kwa kuwapeleka *pool*:

**MA**

53. Kwanza intaitetai poolit(chegeng ibak)
54. Kabanganget ak ngetik
55. Natakeitikani weru kwai
56. Kwek icheke neineti kobir kiratek

**MP**

- Ukienda *pool* utawapata wale wazee**  
**Wanaketi na vijana wadogo**  
**Badala ya kuwashauru vijana**  
**Wanakuwa wao ndio wapotoshaji wakuu**

Hapa, *Pool* katika muktadha huu ni sehemu ambazo watu waliopotoka kimaadili hupatikana. Sehemu hizi hutapata vijana ambao hushiriki katika matumizi ya dawa za kulevya, uasherati na uwizi. Kwa hivyo wasichana wanapopelekwa katika sehemu hizi bila shaka mwishowe hupotoka. Badala ya wazee kuwashauri wasichana hawa, wao ndio viongozi katika sehemu hizo. Aidha, wazee huwapotosha zaidi wasichana kwa kuwapeleka katika mabwawa ya kuogelea. Jambo hili linadhihirika katika mistari ifuatayo:

**MA**

66. Maajabu nteitei swimit
67. Large sizes chemit bek arit (Mungu)
68. Sikomok koyu asista, kotalkang(ngoo aiyenta)
69. Jeso kerkee ak makaita
70. So, tekista cheto ngunan?
71. Kweshion mark

**MP**

- Ukienda bwawa la kuogea utajionea maajabu**  
**Wale majizee na visichana vidogo vinaogelea**  
**Na baadaye kuota jua na kubarizi**  
**Ni sawia na ushetani**  
**Je, huo ni heshima?**  
**Ndio ninawauliza**

Mwimbaji anatusawiria jinsi wazee wanavyotumia wasichana kama vyombo vya kujiburudisha. Wazee hawa wanaogelea pamoja na wasichana wadogo ambao wangukuwa wanasoma shuleni. Mwimbaji anasawasisha matendo hayo na ushetani, yaani vitendo vilivyopita uhalisia. Ni kutokana na matendo hayo ambayo labda ukifiria unadhani hayawezeke, yaani gari moshi kupitia njia nyembamba. Mwimbaji hivyo basi aliirejelea methali, usione wembamba wa reli gari moshi linapita, kuonyesha jinsi wasichana wadogo (reli) wanavyotumiwa na wazee (gari moshi).

Mwingiliano matini katika nyimbo za Kikalenjin za K21 vilevile ulijitokeza kupitia urejeleaji wa tashbihi. Kulingana na Ntarangwi (2004) tasbihi ni istilahi ambayo hutumiwa kufananisha vitu viwili au zaidi. Huhusisha matumizi ya maneno kama yafuatayo: vile, sawa, na, kana kwamba, kama na mithili ya. Uchanganuzi wa wimbo wa Charles Tanui *Sungura* ulidhihirisha kipengele hiki cha mwingiliano matini. Tanui alilinganisha tabia za wanawake na ujanja wa sungura. Simulizi nyingi za Kikalenjin zinamsawiri sungura kama mnyama mjanja sana. Kwa hivyo Tanui aliuimba katika wimbo wake kuwa wanawake ni wajanja kama sungura:

**MA**

5. Ujanja netindoi kwonyichu
6. Uno ba kiplengwet
7. Ukoraaa kabisa!

**MP**

**Ujanja wa hawa wanawake  
Ni kama wa sungura  
Ukoraaa kabisa!**

Tanui anaeleza kwa kina kisa kilichompata ili kubainisha waziwazi ujanja huu wa wanawake. Anasema kuwa alimtongoza mwanamke kwa maneno machache na akakubaliana naye. Alimwambia kuwa hana bwana jinsi inavyodhihirika katika mistari ifuatayo:

**MA**

8. Kikungalal ngalek somok
9. Kulecha matinye boiyot

**MP**

**Tuliongee maneno machache  
Akaniambia hana bwana**

Baada ya mwanamke huyu kuahidi kuwa hana bwana (jambo ambalo lilikuwa uongo), wanaandamana na yeye hadi kwake:

**MA**

14. Komutaa kanyin rwonit
15. Saa sita anun nebo kemoi

**MP**

**Akanipeleka usingizi kwake  
Ikafika saa sita ya usiku**

Walipofika kwake saa sita ya usiku, bwana yake alifika na kubisha mlango:

**MA**

19. Chekukwerakwer kurget
20. Akany kukwerakwer kurget

**MP**

**Akaja na kubisha mlango  
Nami nikangoja abishe mlango**

Mlango ulipobishwa mwimbaji alistuka sana na kuona kuwa kutatokea mapigano makali sana baina yao juu ya mwanamke huyu:

23. Kuwalwa kulee kakemee
24. Alee ooh kakemee!

**Huyu mwanamke akaniambia tumepatikana  
Nikasema ooh tumepatikana!**

25. Ujanja netindoi kwonyichu  
 26. Uno ba kiplengwet

**Ujanja wa hawa wanawake  
 Ni kama wa sungura**

Kumbuka kwamba mwanamke huyu alikuwa amemdanganya mwimbaji kwamba hana bwana; ilhali sasa anasema katika mstari wa 23 kuwa wamepatikana. Madai haya ya mwanamke huyu yanamfanya mwimbaji kustuka sana (mstari 24). Ni matendo hayo ya mwanamke huyu kumdanganya kuwa hana bwana ndiyo yanamfanya mwimbaji kuwaona wanawake kuwa wajanja kama sungura. Kwa hivyo kuna mwingiliano matini baina ya wimbo huu wa Tanui na tashbihi hii ya mjanja kama sungura. Ni kutokana na tashbihi hii, mwimbaji Tanui anauimba wimbo wake wa *Sungura*, chambilecho Terry Eagleton (1983), mwingiliano matini uhusisha ufafanuzi wa dhana zilizozoeleka. Mwimbaji anatomia tasbihi iliyozoeleka na kuuimba wimbo wake.

Kwa ujumla matumizi ya simulizi, methali na tasbihi katika nyimbo za Kikalenjin zilikoleza ubunaji na utungaji wa waimbaji. Vilevile unadhihirisha kuwa jamii ya Kikalenjin imejawa na fasihi simulizi, mila na tamaduni. Kama asemavyo Bill Ashcroft na wenzake (1989:64) matumizi ya simulizi, methali na tasbihi katika nyimbo yadhihirisha kuwa jamii za Kiafrika zimejawa na fasihi simulizi.

#### **4.1.3 UREJELEAJI WA BIBILIA TAKATIFU**

Nyimbo za Kikalenjin za K21 zilirejelea Kitabu cha Uzima au Biblia takatifu. Kulingana na Riches (2000) bibilia ni mkusanyiko wa matini yanayochukuliwa kuwa matakatifu na Wakristo. Bibilia hii imegawanyika mara mbili: matini ya agano la kale na agano jipya. Matini ya agano la kale ni thelathini na tisa nayo agano jipya ina matini ishirini na saba. Kwa ujumla bibilia imeundwa na matini sitini na sita. Bibilia hii inaaminika iliandikwa hapo zamani sana na watu waliopata ufunuo kutoka kwa Mungu. Katika utafiti wetu



tuligundua kuwa wimbo wa Joel Kimetto uitwao *Kichigili (Kuchunguza)* umetumia mwingiliano matini mlalo katika kurejelea bibilia: Wimbo huu umerejelea bibilia katika kitabu cha Waamuzi, mstari wa 7 unaposema:

**MA**

7. Soman Kirwakik we eng taman ak loo
8. Koitatab akwan we ak itestai
9. Kinerech Samson oh kobel ingalut
10. woi korom chamyet we bele emet
11. Ripek chamyet neku hasaret
12. Kass ak po Samson ak Delila
13. Kinget Samson kung'anta sirii
14. Kebol konyekyik wee korat chamnyet

**MP**

**Ukisoma Biblia Waamuzi mlango wa 16  
Mstari wa nne na kuendelea  
Kwa hamaki Samsoni kachoma ghala  
Woi upendo ni hatari unachoma  
Jiepushe na upendo uletao hasara  
Twasikia juu ya Samsoni na Delila  
Samsoni alidanganywa akatoa siri  
Akang'olewa macho, upendo hauna  
macho**

Hapa, mwimbaji alikirejelea kitabu cha Bibilia cha Waamuzi mlango wa kumi na sita, mstari wa nne (Waamuzi 16:4). Kitabu cha Waamuzi ni miongoni mwa vitabu 39 vya Bibilia ya Kikristo katika Agano la Kale. Kitabu hiki ni cha saba baada ya Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu la Torati na Yoshua. Katika kitabu hiki uhusiano wa kimapenzi kati ya Samson na Delila unazungumziwa. Delila alimrahi Samson kumwambia nini inampatia nguvu. Japo Samson alimdanganya mara tatu, alimwambia ukweli mwishowe. Samson alimwambia Delila kuwa nywele zake zikinyolewa nguvu zitamwishia. Delila alifanya jinsi alivyoambiwa na nguvu zilimwishia Samson. Hii ilimpelekea Samson kushikwa na Wafilipino na kung'olewa macho. Kwa hivyo uhusiano huo ulikuwa hatari kwani Samson aliweza kuangamia mwishowe kwa kutolewa macho. Urejeleaji huo ulifaa wimbo huu kwa sababu mwimbaji aliweza kuonyesha kwamba uhusiano wa kimapenzi unaweza kuleta maangamizi, jinsi anavyoendelea kueleza katika mstari wa 15. Katika mstari huu, mwimbaji ananukuu na kufafanua kitabu cha Hesabu mlango wa 15 na 16:

**MA**

15. Kaitosik 15 ak16 kinget korotat nekibar
16. Biik elfuche chechang mami nekikas
17. Ntakimami chito nakiker ntakikobuku biik

**MP**

**Ukisoma Hesabu 15 na 16 kuna kitu kiliangamiza  
Maelfu ya watu na hakikuziwa  
Kama hakungekuwa na mtu aliyekizuia watu wote  
wangekufa**

18. Kerger ak ukimwi nikikutar biik **Ni sawa na ukimwi unaoangamiza watu**  
 Hapa, mwimbaji anatumia kuwa katika kitabu hiki cha Biblia kuna kitu  
 kilichoangamiza watu. Ukisoma kitabu cha Hesabu mlango wa 15 na 16 tunaambiwa  
 Wanaisraeli walikuwa wameupinga uongozi wa Musa na Aaron. Musa na Aaron  
 walikuwa watumishi wa Mungu. Wapingamizi hawa waliongozwa na Korah, Dathan na  
 Abiram. Musa aliomba Mungu awaangamize wapingamizi hao. Mungu alikubali maombi  
 yake na kuwaangamiza wote wakiwemo zaidi ya Wanaisraeli 250. Wanaisraeli  
 hawakufurahia maangamizo hayo na waliandamana tena ili kuupinga uongozi wa Musa  
 na Aaron. Mungu alikasirika na kuahidi Musa na Aaron kuwa angewaangamiza  
 Wanaisraeli wote. Musa aliwaonea huruma na kuomba Mungu asiwaangamize tena.  
 Lakini hata hivyo, Mungu alianza kuwaangamiza Wanaisraeli mara moja na Musa  
 alimtuma Aaron aingilie kati kabla wajeangamizwa wote. Kabla Aaron hajeingilia kati,  
 zaidi ya watu 14, 700 walikuwa wameangamia (Thomas 2006). Urejeleaji huu ulifaa kwa  
 kuwa mwimbaji aliweza kuthibitisha kuangamia kwa watu wengi sana (mstari 16) na  
 hivyo basi kukifananisha na ugonjwa wa UKIMWI (mstari 18). Fauka ya hayo,  
 mwimbaji huyu, Joel Kimetto, katika wimbo wake alikirejelea kitabu cha Wakorinto wa  
 kwanza, mlango wa sita, mstari wa kumi na tano hadi ishirini (1 Wakorinto 6:15-20):

**MA**

24. Soman Korintoit kurkat nebo loo koito  
 ab taman ak mut testai ak tubtem  
 25. Nei le borta ng'ung ko ekalut ab Jehovah

**MP**

**Soma Wakorinto wa kwanza mlango wa  
 Sita mstari wa kumi na tano hadi ishirini  
 Jua kwamba mwili wako ni nyumba ya  
 Mungu**

Katika mistari hii, mwimbaji alikirejelea kitabu cha Wakorinto wa kwanza, mlango wa  
 sita, mstari wa kumi na tano hadi ishirini. Katika kitabu hiki Wakristo wanasihwa  
 wasishiriki katika uasherati. Hii ni kwa sababu miili yao ni nyumba ya Mungu na iwapo  
 watahiriki katika uasherati watakuwa wanaharibu nyumba ya Mungu. Kwa kurejelea  
 matini hii mwimbaji anataka kuwashawishi watu kutoshiriki ili wasiambukizwe ugonjwa

wa UKIMWI. Kwa ujumla urejeleaji wa Bibilia unaoana na hoja aliyoeleza Ronald Barthes katika kitabu chake *The Death of Author* kuwa kila matini ni unukuzi wa matini ya awali na kisha kutapakazwa ndani mwake.

(<http://www2.iath.virginia.edu/elab/hfl0278.html> 02/10/2013 10.00a.m).

#### 4.1.4 UREJELEAJI WA KATIBA YA KENYA

Mwingiliano matini mlalo pia ulijitokeza pale nyimbo za Kikalenjin ziliporejelea Katiba ya Kenya. Katiba ya Kenya ni sheria kuu ya taifa. Katiba ni kielelezo kinachotumiwa na serikali kuongoza nchi. Aidha, inafafanua uhusiano kati ya serikali na wananchi. Katiba mpya ya Kenya ilifanywa kuwa sheria tarehe 27 Agosti 2010 na kuchukua nafasi ya katiba ya zamani iliyotumiwa tangia mwaka wa 1963. Katiba ya Kenya imeundwa na sura kumi na nane na vifungu 264 vinavyozungumzia mambo mbalimbali (Katiba ya Kenya 2010). Mwimbaji Geoffrey Kipkurui aliirejelea Katiba ya Kenya katika wimbo wake *Onae Katiba (Mjue Katiba)*. Mada ya wimbo huu inamaanisha kuwa Wakenya na hasa Wakalenjin wanafaa kuelimishwa kuhusu katiba mpya ya Kenya. Mwimbaji huyu anawasihi Wakalenjin waelewe kuhusu Katiba ili nchi iendelee mbele:

##### MA

1. Kalenjin ogosun
2. Onae katiba nelel
3. Sikwa tai emet

##### MP

**Wakalenjin muamke  
Mjue Katiba Mpya  
Halafu nchi iendelee**

Katika mistari hii, mwimbaji anawaambia wakalenjin wajue na waelewe kuhusu Katiba Mpya ili nchi iendelee. Japo mwimbaji huyu amezungumzia kuhusu katiba kwa ujumla, upelelezi wa ndani unaonyesha kuwa amerejelea sura ya nne ya Katiba ya Kenya iliyochapishwa tarehe 6/05/2010. Kwa ujumla sura ya nne ya Katiba inahusu haki za binadamu. Hebu angalia mistari ya 6 na 7:

##### MA

6. Omwachi bikcha kule katiba koribe bika tugul
7. Iheshimi haki nebo chitugul

##### MP

**Muwaambie katiba inatunza watu wote  
Katiba inaheshimu haki za kila mtu**

Katika mistari hii ya 6 na 7, mwimbaji amezungumzia kuhusu katiba. Anasema kuwa katiba inatunza na kuheshimu haki za kila mtu. Haki za kila mtu zimezungumziwa kwa kina katika katiba ya Kenya, sura ya nne. Miongoni mwa haki hizo ni haki ya kuishi, usawa na uhuru dhidi ya kubaguliwa, hadhi ya binadamu na uhuru wa usalama wa mtu.

Katika mistari ya 12 hadi 13 Kipkurui amezungumzia haki ya kuishi:

MA	MP
12. Kalenjin onae kule katiba koribe sabantab chito	<b>Wakalenjin mjue katiba inatunza uhai wetu</b>
13. Amuak ale sabantab chito kutou eng moit ab mamayi	<b>Ninawaambia uhai uanza mimba itungwapo</b>
17. Meyanat keturur matinwaek wacha!	<b>Uavyaji mimba haukubaliki wacha!</b>
21. Kandoikcha onet bikcha kule nya ngeturur lakok	<b>Viongozi wetu muafunze watu uavyaji ni mbaya</b>
22. Kerke ak kebaris ak komeani Mungu	<b>Ni sawa na kuuwa na Mungu anakataa</b>

Hapa, mwimbaji anawafahamisha Wakalenjin waelewe kwamba katiba inatunza uhai.

Aidha, anawaambia kuwa uhai uanza mimba itungwapo. Ili kuhifadhi uhai, katiba inakataza uavyaji mimba na ni jukumu la kila kiongozi kuwafunza watu wake. Fauka ya hayo anasema kuwa Mungu hakubali uavyaji mimba. Sehemu hii imenukuliwa kutoka Katiba ya Kenya sura ya nne, kifungu cha 26 ambacho nimekinukuu hapa jinsi ilivyo kwenye Katiba:

**Haki ya kuishi kifungu cha 26:**

- a) Kila mtu ana haki ya kuishi
- b) Maisha ya mtu huanza baada ya kutunga mimba
- c) Mtu hatauawa kimaksudi, isipokuwa kwa kiwango kinachoidhinishwa na Katiba hii au kwa sheria nyingine iliyoandikwa
- d) Uavyaji mimba hauruhusiwi, isipokuwa kwa maoni ya mtaalamu wa masuala ya kiafya, kuna haja ya matibabu ya dharura, au maisha au afya ya mama imo hatarini au kwa kuidhinishwa na sheria nyingine iliyoandikwa (Katiba ya Kenya 2010, msisitizo wangu).

Nadhani mwimbaji Kipkurui amezitumia sehemu za Katiba nilizopikia mistari katika wimbo wake. Hii ni kwa sababu katika wimbo wake mstari wa 12, amesema kuwa katiba inatunza uhai wetu, jambo ambalo linathibitishwa na kifungu hiki cha 26 cha Katiba mstari wa (a) kinachozungumzia kuhusu haki za kuishi. Vilevile Kipkurui katika wimbo wake amezungumzia kuhusu uanzapo wa uhai katika mstari wa 13, jambo ambalo

linadhihirika katika Katiba ya Kenya mstari wa (b) unaoesema kuwa maisha ya mtu huanza atungwapo mimba. Aidha, Kipkurui katika mstari wa 17 amekataza uavyaji wa mimba jambo ambalo linathibitishwa kwenye Katiba mstari wa (d) unaoesema uavyaji mimba hauruhusiwi.

Fauka ya hayo, wimbo wa Kipkurui unaendelea kufafanua Katiba ya Kenya. Katika mistari ya 31 hadi 34, upelelezi wa ndani unabainisha kuwa kifungu kinachozungumziwa ni cha 39 cha Katiba ya Kenya. Mistari hii inadokezwa hivi:

**MA**

- 31. Bikab ab Kenya onae kulel katiba nelel
- 32. Kuanjini chitugul komen alotugul in Kenya jua!
- 33. Kandoikcha eng Rift Valley ondochi bikcha
- 34. Ak koonet katiba nelel ak kerib sikwatai emet

**MP**

**Watu wa Kenya mjue kwamba  
Kila mkenya anaruhusiwa kuishi popote  
nchini  
Viongozi wa Bonde la Ufa muongoze  
watu  
Na muwafunze katiba mpya ili nchi  
iendelee**

Kama mistari inavyojidokeza, Kipkurui anawarai viongozi wa Bonde la ufa kuwaongoza watu. Yeye anaona kuwa watu wakifunzwa kuhusu katiba nchi itaweza kuendelea mbele. Anawaambia watu wa Kenya wajue kwamba kila mtu ana haki ya kuishi popote nchini. Nadhani Kipkurui amenukuu kifungu cha 39 cha Katiba kwenye wimbo wake. Vilevile nimekinukuu kifungu hiki jinsi kilivyo kwenye Katiba ya Kenya ili kuonyesha kinagaubaga jinsi unukuzi huu ulivyofanywa:

**Uhuru wa kutembea na makaazi kifungu cha 39:**

- a) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutembea.
- b) Kila mtu ana haki ya kuondoka nchini Kenya
- c) Kila mwananchi ana haki ya kuingia, kubaki na kuishi kokote nchini Kenya (Katiba ya Kenya 2010, msisitizo wangu)

Kama inavyobainika katika kifungu hiki cha 39, mstari wa (c) unazungumzia kuhusu haki ya kuishi kokote nchini Kenya. Mstari huu unaona na kile Kipkurui amesema katika wimbo wake mstari wa 32 kuwa kila mwananchi anaruhusiwa kuishi popote nchini Kenya. Kwa ujumla kuna mwingiliano matini baina ya wimbo wa Kipkurui na Katiba ya Kenya. Hii ni kwa sababu Kipkurui ameweza kunukuu baadhi ya vifungu vya Katiba ya

Kenya katika wimbo *Onae Katiba (Mjue Katiba)* na kuvifanya viwe vyake. Hii inathibitisha kile M. H. Abram (1981:200) alisema katika ufafanuzi wa mwingiliano matini kuwa kazi zozote zinazodhihirisha kipengele cha mwingiliano matini uhusisha unukuzi wa kazi tangulizi.

#### **4.1.5 UREJELEAJI WA NYIMBO NYINGINE**

Mwingiliano matini hutokea sio tu kwa kazi za kifasihi kurejelea kazi au tanzu zingine bali pia kwa nyimbo nyingine (Ritgerotil 2006). Katika sehemu hii nimetoa mifano mahsusi inayobainisha jinsi nyimbo teule zinavyofanya unukuzi au urejelezi wa moja kwa moja kutoka nyimbo nyingine. Katika muktadha huu, nyimbo teule zinaelekea kuafiki kuwepo kwa nyimbo zilizotangulia na ambazo zimeathiri mwelekeo zinazozichukua. Hapa tumetoa mifano maalum inayoendeleza sifa hii ya mwingiliano matini mlalo.

Kwanza, kuna mwingiliano matini baina ya wimbo wa Sheila Cherotio, *kwondap transmara (bibi kutoka transmara)* na ule wa msanii Kotombululdo uitwao *meyat kutit (usiongee vibaya)*. Wimbo wa *Kotombululdo (meyat kutit)* unalenga kurekebisha usawiri mbaya kuhusu eneo na wanawake wa Transmara. Usawiri huo mbaya ulikuwa umefanywa na wimbo wa awali wa Cherotio. Cherotio anadai kwamba wanawake wa Transmara wako nyuma sio tu kimaendeleo bali hata katika starehe. Wanawake hao, asemavyo Cherotio, hawana nidhamu za kimaisha na hawajui kustarehe. Kwa ufupi anawaona kama wasiopevuka:

#### **MA**

25. Mainget chebechebe
26. Mainget breakfast

#### **MP**

- Hawajui starehe**  
**Hajui kiamsha kinywa**

Usawiri wa kina kuhusu mwanamke wa Transmara umejitokeza kuanzia mistari ya 65 hadi 80:

**MA**

65. Nee rahisi nee ya
66. Ingikaji elfut
67. Uyoo tindae ten thousand
68. Kwo Chebunyaa Monday Jumatatu
69. Komaalee ngwaitab ngwek
70. Wendii kwal sundet
71. Nebo moit eng teta
72. Nebo tati bob eng Chepkuyuk
73. Nebo eng ngwek
74. Aya, ak kwo kwal sukarit robo
75. Ak kunget nekintanaitah chaik
76. Machanik koraa kwendi cha kipimani
77. Cha ba kakit cha ba 27 shilings
78. Eng ngeba tililinta koraa
79. Ngele kakiilkee, ko makali
80. Mwete kelyek ak kuilee subunit

**MP**

- Ambaye ni rahisi sana (mwanamke wa Transmara)**
- Ukimpatia shilingi elfu moja**  
**Ni kama ana shilingi elfu kumi**  
**Anaenda Jumatatu soko ya Chebunyaa**  
**Hawezi kununua mafuta ya mboga**  
**Bali anaenda kununua mafuta**  
**Yaliyoko matumbo ya ng'ombe**  
**Ya shilingi thelatini huko Chepkuyuk**  
**Na kuja kutumia kwenye mboga**  
**Tena anaenda kununua sukari robo**  
**Na anajua jinsi ya kuweka**  
**Pia majani ananunua ya kupima**  
**Yaliyofungwa karatasini na kuuzwa shilingi 27**  
**Na tukienda kwa usafi**  
**Tukisema tunajipaka mafuta, sio ghali**  
**Anaoga na kujipaka povu la sabuni**

Hapa, mwanamke wa Transmara amesawiriwa kuwa ni rahisi sana na asiyejua namna ya kuzitumia fedha kama inavyotarajiwa kwa mwanamke wa kisasa. Akipewa elfu moja ni kama amepewa shilingi elfu kumi. Hii ni kwa sababu hana gharama nyingi. Hununua vitu vya bei rahisi. Kwa mfano badala ya kununua mafuta ya kupikia mboga, yeye hununua nyama ya ng'ombe iliyonona na kugandiana mafuta ambayo anayatumia kupikia. Vilevile ananunua sukari na majani vya vijipaketi vidogo na anapoweka kwenye chai huweka kidogo sana. Katika mistari wa 80, mwanamke wa Transmara anasawiriwa kuwa hata hawajipaki mafuta bali wanajipaka povu la sabuni. Hatimaye, mwanamke wa Transmara amesawiriwa kuwa hawezi hata kupiga mswaki:

**MA**

101. Lemasite akot kelek

Katika mistari hii, mwanamke wa Transmara amesawiriwa kuwa hawapigi mswaki. Hii inadhihirisha kuwa meno yao yatakuwa yakinuka.

**MP**

- Hawezi hata kupiga mswaki**

Kwa ujumla wanawake wa Transmara wamesawiriwa na Cherotio kama wanawake wasiopevuka, wajinga, wasiojua mitindo na mambo ya kisasa kwa haraka, wasiojua starehe, mafukara na waliokosa mwelekeo wa kimaisha.

Wimbo wa Kotombululdo *Meyat Kutit (usiongee Vibaya)* uliimbwa ili kurekebisha usawiri hasi wa wanawake wa Transmara, kama unavyosema katika mistari ya 8 hadi 17:

**MA**

8. Meyat kutit
9. Ingalale Transmara neamenye
10. Kiakass ain eng station
11. Ongalale Transmara
12. Kiakass ake nelenate
13. Transmara komi kwonyik cheseretos
14. Lileke mwaitab teta, mondai koreik
15. Kiakass ake nelenate
16. Transmara komi kwonyik cheileke mwaitab teta
17. Mochezanee, we!

**MP**

- Usiongee vibaya**  
**Kuhusu Transmara, mahala ninapoishi**  
**Nilisikia kwa stesheni juzi**  
**Wakiongee kuhusu Transmara**  
**Nilisikia mwengine akisema**  
**Transmara kuna wanawake mafukara**  
**Wanajipaka mafuta ya ng'ombe na hawana nguo**  
**Nilisikia mwengine akisema**  
**Transmara wanawake wanajipaka mafuta ya**  
**ng'ombe**  
**Msiwachezee, we!**

Hapa, Kotombululdo anamuonya mwimbaji aliyewasawiri vibaya wanawake wa

Transmara. Ingawa Kotombululdo hajamtaja Cherotio kwa jina, unukuzi wa maneno uliomo ndani ya wimbo wake unaashiria hivyo. Anadai kuwa alisikia katika stesheni (stesheni hapa imetumiwa kumaanisha kusikia wimbo wa Cherotio *Kwondap Transmara*) akiongee kuhusu wanawake wa Transmara kuwa ni mafukara, wasiojipaka mafuta safi ila kutumia mapovu ya sabuni na kuwa hawana nguo. Katika mistari wa 17 anawaambia wakome kabisa. Sahihisho hili linalotolewa na Kotombululdo kwa Cherotio ni sawia na lile la riwaya ya Chinua Achebe *Things Fall Apart* inayorekebisha usawiri hasi wa Waafrika kama wajinga – jambo linaloendelezwa na riwaya ya Joseph Conrad *Heart of Darkness* (Emenyomu 2002).

Katika utafiti huu, tuligundua kuwa Kotombululdo alikuwa anadengua wimbo wa Cherotio ili kuwaambia walimwengu kuwa wanawake wa Transmara ni wazuri. Tazama mistari ifuatayo:

**MA**

55. Nkoker chito uyo mabanganat
56. Koit kole nyaa alinta
57. Transmara moitab moait

**MP**

- Mtu ukisikia unadhani hawajajipanga**  
**Watahesabu kuwa huko ni kubaya**  
**Transmara mahala pa wanawake**



Kotombuludo anasema kuwa watu wakisikia wimbo wa awali (wa Cherotio) bila shaka wataadhani kuwa wanawake wa Transmara ni wabaya (Mstari 56). Anasema kuwa Transmara ni pahala pa wanawake wazuri na hii inampelekea kuimba wimbo wake:

**MA**

27. Transmara emet neemey
28. Mie minutik
29. Miten tukaa chekoron
30. Miten lakok chesomansot

**MP**

- Transmara ni pahala pazuri**  
**Kuna nafaka**  
**Kuna ng'ombe wazuri**  
**Kuna watoto wanaosoma**

Katika mistari hii, Kotombuludo anasema kuwa Transmara ni pahala pazuri penye chakula, ng'ombe na hata elimu ya kisasa kinyume na madai yaliyomo katika wimbo wa Cherotio. Kwa ujumla wimbo huu wa Kotombuludo uliimbwa ili kunadhifisha wimbo wa awali wa Cherotio na hivyo basi kujaza nafasi zilizoachwa na kurekebisha usawiri mbaya wa wanawake wa Transmara. Hii inashadidia kile Michel Foucault alisema kuwa kazi yoyote ile ya kisanaa ni urejelezi wa matini mengine ya awali ([Foucault 1974: 23](#)).

Fauka ya hayo mwingiliano matini unajitokeza baina ya nyimbo za *Meus Kwondo* (*Msipigie Wanawake Kelele*) wa Joyce Chemutai na ule wa Sheila Cherotich uitwao *Meus murenik* (*Msipigie wanaume kelele*). Chemutai katika wimbo wake *Meus Kwondo* (*Msipigie Wanawake Kelele*) anapendekeza kwa kina jinsi wanaume wanavyofaa kuwatunza wanawake au wake zao. Chemutai anaanza hivi wimbo wake:

**MA**

2. Meus kwanyit murenik, wacha
3. Meus Kwando nebo kot mama toto,
4. cham i bak

**MP**

- Wanaume msiwapigie kelele wanawake wenu**  
**Usimpigie kelele mama watoto wako nyumbani**  
**Mpende sana**

Katika mistari hii, Chemutai anawasihi wanaume wawatonze wanawake wao vizuri kwa kuwapenda badala ya kuwapigia kelele. Wimbo huu unaenda hatua moja mbele na kuyataja mahitaji ambayo wanaume wanafaa kuwatimizia wake zao. Baadhi ya mahitaji yaliyoorodheshwa ni kama yafuatayo:

**MA**

5. Mama toto koyalo irib kotililit
8. Aljii tukuk chemache, mama toto, ngoriet
9. Korat medit ak konee kuu chebabich

**MP**

- Lazima umchunge mama watoto awe safi**  
**Mnununulie vitu anavyohitaji kama nguo**  
**Asuke nywele kama wengine**

11. Ak kimutate kokertat
14. Akimwachinii, amukase matibirabir
18. Aljii bendo aku nee, nyamchom

**Na umtembeze atalii**  
**Ongea naye , usimpigepige mkeo**  
**Bibi yako umnunulie nyama choma**

Hapa, Chelele anawaambia wanaume kwa undani mahitaji ambayo wanawake wanayataka. Miongoni mwa mahitaji hayo ni nguo, wasukwe nywele, watembezwe na wapewe vyakula kama nyama choma. Aidha, wimbo huu unasisitiza kuwa mwanamume lazima amtunze bibi yake awe safi ili apendeze kwake na mbele ya watu. Aidha, Chelele anataka mwanamume asimpige mwanamke bali azungumze naye kwa maelewano. Wimbo huu unasema kuwa iwapo mwanamume hatamtunza bibi yake basi hatakuwa mwenye kupendeza kwake, au atafute wanawake wengine atakaozini nao:

- MA**  
 24. Rip kotililit, simesubate chebabich chakikerip

**MP**  
**Umchunge awe safi ili usianze mpango wa kando**

Ni kutokana na wimbo huu uliowalenga wanaume ndipo Sheila Cherotich alipouimba wimbo wake wa *meus murenik (Msipigie wanaume kelele)*. Wimbo huu unawalenga wanawake. Ingawa wimbo huu uliimbwa na mwanamke, unawatetea wanaume ambao kwa sababu moja au nyingine wanadhulumiwa na wanawake. Usawa wa kijinsia unaosisitizwa mwanzoni mwa wimbo huu unadokeza haja ya kuwepo kwa utulivu nyumbani na hasa kwa wanawake wanaowapigia waume zao kelele:

- MA**  
 1. Kwonyit ku murenik  
 2. Kwonyit ku murenik  
 3. Kwonyit kwonyit meus murenik

**MP**  
**Wanaume ni sawa na wanawake**  
**Wanaume ni sawa na wanawake**  
**Wanawake msiwapigie wanaume kelele**

Hapa, Cherotich anasema kuwa wanaume ni sawa na wanawake. Huenda rai hii imetolewa kutokana na hali halisi ambapo wapo baadhi ya wanawake ambao wanawanyanyasa na kuwadhulumu waume zao. Wimbo huu ni matini pingamizi inayodengua taasubi za kiume katika wimbo wa awali wa Joyce Chemutai. Kama

wanavyotunzwa na wanaume nao wanafaa kutunzwa na kuheshimiwa. Cherotich anatoa sababu kadhaa ambazo anaona zinafaa zizingatiwe mintarafu ya wanaume:

**MA**

- 4. Metit ap kaa
- 7. Sikeamshe ache kumurenik
- 10. Kusomanso lakok kumurenik
- 15. Ya kisete luket kumurenik

**MP**

- Wao ni viongozi wa familia**
- Wanaume ndio wanaotulisha**
- Wanaume wanatusomeshea watoto**
- Wao ndio wanaotulinda**

Hapa, Cherotich anasema kuwa wanawake wanafaa kuwalinda na kuwatunza wananaume kwa sababu wao ndio viongozi wa familia, huwapa ulinzi, hulisha familia na kuwasomesha watoto. Madai hayo ni kama majibu kutoka wanaume kwa wanawake; kuwa wanaume hutekeleza majukumu muhimu katika jamii na hivyo basi wanafaa kutunzwa. Pindi hayo yanapozingatiwa, matokeo yatakuwa ni jamii yenye masikizano kama wimbo unavyozidi kueleza:

**MA**

- 23. Ongerib murenik sikuribech cheee

**MP**

- Tuwachunge wanaume halafu watuchunge**

Katika mstari huu, inadhihirika kuwa Cherotich anapendekeza kuwa wanawake wanapata mahitaji yao ya kimsingi ikiwa wanaume watapewa haki zao. Kwa muktasari nyimbo hizi mbili za Chemutai na Cherotich zinaonyesha kipengele cha mwingiliano matini. Zote zinajadili kuhusu maswala ya wanawake na wanaume katika jamii. Mjadiliano huo unazua fikra kuwa jinsia zote ni sawa na wanafaa kuishi kwa maelewano.

#### **4.2 UCHANGANUZI WA KIPENGELE CHA UIGAJI WA VIPANDE VYA SIMULIZI**

Kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi kilibuniwa baada ya sanaa ya juu kusambaratika, sanaa ya juu ilikuwa inasisitiza ugeni na upekee wa kila msanii. Sanaa hii ilisambaratika kwa sababu wasanii walifika upeo wa juu kiasi cha kutoweza kutunga kazi zingine zilizoonekana tofauti. Kwa hivyo msanii wa kibaadausasa aliona heri kukusanya mitindo ya zamani na kuipanga upya. Hivyo basi badala ya ugeni na upekee uliokuwa katika usasa, wanabadausasa walithamini uigaji wa vipande vya simulizi au unukuzi wa

kazi zilizotungwa awali (Best and Kellner 1991). Kutokana na mafafanuzi hayo, kazi zozote zinazotumia mtindo huu wa uigaji wa vipande vya simulizi huwa zimeundwa kwa upande mkubwa na maneno, virai, sentensi, mistari, aya, mizani na hata maonyesho kutoka kazi zingine. Mtindo huu hufanya kazi husika kuonekana kama zilizonukuliwa kutoka kazi za watu wengine (Childs na Fowler 2006). Mtindo huu ulikuwa unaonekana kama uwizi hapo awali. Kwa hivi sasa umekubalika kama mtindo mmojawapo wa kuwasilishia kazi ya sanaa. Hivyo basi katika nyimbo za Kikalenjin za K21 waimbaji wameweza kuiga kazi za waimbaji wengine na kuzifanya ziwe zao. Katika sehemu hii nimetoa nyimbo teule zinazodhihirisha kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi. Katika kufanya hivyo, sura hii inazingatia madhumuni mahususi ya utafiti ya kuchanganua kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin.

Kwa mujibu wa mwanafasihi Kimani Njogu (2006:2) fasihi simulizi ya kileo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya binadamu, kwani ndani yake kuna masimulizi, maigizo, tathmini za mazingira na mahusiano ya kijamii. Ni kwa sababu hii nyimbo za kileo za Kikalenjin ziliweza kuakisi mateso ya watu waliofurushwa kwenye msitu wa Mau. Waimbaji Jackline Memo na Joyce Cheptoo waliimba nyimbo za *Osoruech Eng Mau (Mtuokoe Katika Mau)* na *Rirek en Mau (Mateso Katika Mau)* mtawalia; ili kuonyesha jinsi watu walivyoteseka katika msitu wa Mau. Uchanganuzi wa nyimbo hizi za Memo na Cheptoo zilidhihirisha kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi.

Nyimbo hizi mbili zinaonyesha kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi kupitia ploti sawa. Kulingana na Tilak (1995) ploti ni mfululizo wa vitushi katika kazi za sanaa kuanzia mwanzo hadi mwisho. Aidha, Ntarangwi (2004) anasema kuwa ploti ni uchaguzi

wa vijisehemu vinavyojenga hadithi kwa njia ambayo yatoa mfuatano na usababishano ili hatimaye kujenga kitu kamilifu. Uchanganuzi wa ploti za nyimbo za Memo na Cheptoo zinadhihirisha kuwa zinaigana. Mwanzo wa nyimbo hizi ni pale watu walipofurushwa Mau na serikali tawala ili kuhifadhi msitu wa Mau: Memo anasema hivi katika mistari ifuatayo:

MA	MP
50. Kikase kila kandoi ang taarifa	<b>Tunasikia kila siku kwenye taarifa kuwa</b>
51. Meche serikali keon biik cha chemitei Mau	<b>Serikali inataka kufurusha watu walioko msitu wa Mau</b>

Mistari hii inatueleza kinagaubaga kuwa wenyeji walikuwa wameambiwa kuwa watafurushwa kutoka msitu wa Mau na serikali. Mawazo yayo hayo yanaendelezwa na mwimbaji Cheptoo *Rirek en Mau (Mateso Katika Mau)* katika mistari wa pili:

MA	MP
2. Kieon serikali biikcha chemiten eng	<b>Serikali ilifurusha watu wetu walioko msitu wa Mau</b>

Watu hawa walipofukuzwa kutoka msitu wa Mau waliteseka sana. Mateso hayo yaliendelezwa na mwimbaji Memo katika wimbo wake *Osoruech Eng Mau (Mtuokoe Katika Mau)*:

MA	MP
15. Yalilta yee oh, kandoi yaliltosh	<b>Watu ambao wanaishi upande wa</b>
16. biik cho chemitei Sekemiat	<b>Sekemiat wanateseka</b>
23. Yaliltosh yee oh, Binech yaliltosh	<b>Watu ambao wanaishi Binech wanateseka</b>
39. Chemitei Kaptai, kandoi koyaltosh	<b>Watu walioko Kaptai wanateseka</b>

Katika mistari hii, Memo anatusawiria jinsi watu walivyoteseka katika sehemu mbalimbali. Anatuambia kuwa watu waliokuwa wakiishi Sekemiat, Binech na Kaptai wanateseka. Sawia na hayo mwimbaji Cheptoo anatuambia katika wimbo wake *Rirek en Mau (Mateso Katika Mau)*:

MA	MP
6. Rirek! Rirek! Rirek! Rirek!	<b>Mateso! Mateso! Mateso! Mateso!</b>
15. Oker biikcha komenye sakech	<b>Watu wetu hawana makao</b>
16. Eng Sekemiat ak Binech	<b>Huko Sekemiat na Binech</b>
17. Kaptai ngorirak Mungu	<b>Watu wa Kaptai Mungu hawaonee huruma</b>

Kama Memo, Cheptoo anatuambia kuwa watu ambao walifurushwa kutoka msitu wa Mau wanateseka. Hii ni kwa sababu watu hao hawana makao. Watu hawa ni wale walioko Sekemiat, Binech na Kaptai. Usawiri wa mateso yanayokumba watu walioko sehemu sawa za Sekemiat, Binech na Kaptai ni dhihirisho kuwa waimbaji Memo na Cheptoo waliigana au kutumia mtindo huu wa uigaji wa vipande vya simulizi.

Kutokana na mateso hayo, waimbaji Memo na Cheptoo wanajaribu kutafuta suluhisho kutoka kwa viongozi. Wanawarai viongozi kuwatetea watu hao. Wanadai kuwa walichaguliwa ili kuwasaidia watu lakini sio kuwatesa. Memo katika wimbo wake anasema hivi:

**MA**

- 45. Rirech cha ak kandoi, kirirchi oh!
- 46. Osoruech biik cha chemita mau
- 47. Emet nee koo
- 48. Pendi ano bikcha?
- 49. Ochengi nawech onebendi

**MP**

- Tunawalilia viongozi oh!**
- Muwaokoe watu wetu wanaoishi Mau**
- Nchi yetu ni kubwa**
- Watu wetu wataenda wapi?**
- Mtafutie watu wetu mahali**

Hapa, Memo anawarai viongozi kuwaokoa watu ambao wanateseka kwa kukosa makao. Japo watu hawa walifurushwa kutoka msitu wa Mau, Memo anasema kuwa nchi yetu ni kubwa. Hivyo basi watu hawa watafutiwe makao mahala kwingine. Mapendekezo sawia na hayo yanatolewa na Cheptoo katika mistari ifuatayo:

**MA**

- 48. Lakini alenee kandoik kabisa
- 49. Maunoo kabisa ongeriree sabanuek ak biik
- 50. Engenai nekintai tun icheket

**MP**

- Lakini nawaambia viongozi wetu**
- Haifai hivyo tuonee huruma watu wetu**
- Tuwatafutie makao**

Cheptoo anasema kuwa watu hawafai kuteseka. Sawia na Memo, anapendekeza viongozi kuwatafutia watu hawa makao mbadalia kuliko kuwawacha wateseke. Waimbaji hawa kwa pamoja kutoa mapendekezo ya suluhisho zinazolingana ni mfano wa kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi. Hii ni kwa sababu katika dunia ya kibaadausasa haiwezekani kubuni sanaa mpya bali wasanii huibiana mawazo na kufanya yawe mawazo

yao mahususi (Jameson 1984) Japo nyimbo za Cheptoo na Memo zinamfanano mkubwa tukizingatia ploti zao, ni nyimbo mbili ambazo zinajisimamia. Hivyo basi, kupitia kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi waimbaji hawa waliweza kuimba nyimbo zao tofauti.

Winszewski (2008) akimnukuu Jameson (1984) anahoji kuwa waimbaji wa ubaadausasa hawawezi kubuni mitindo mipya.....ni kidogo tu kinawezekana; sababu ni kuwa imeshabuniwa tayari. Kwa hivyo badala ya kuimba kwa mitindo bunilizi waimbaji wa kibaadausasa ukutanisha mitindo iliyopo katika fasihi na kufanya kuwa kazi zao asilia. Madai haya yalidhihirika tulipochanganua nyimbo za Philip Yegon *Ezekiel Kemboi* na Kipkemei Tulwet *Emily Jepchumba*. Hii ni kwa sababu wimbo wa Yegon *Ezekiel Kemboi* uliiga wimbo wa Tulwet *Emily Jepchumba*. Kwa mukhtasari wimbo wa Yegon *Ezekiel Kemboi* ni wimbo ulioimbwa ili kumsifu mwanariadha mashuhuru kutoka Marakwet anayeitwa Ezekiel Kemboi. Ezekiel Kemboi ni mwanariadha aliyefunja rekodi mbalimbali za riadha ya kuruka viunzi ya mita 1500. Baada ya mwanariadha huyu kushinda rekodi yoyote ile, imekuwa desturi yake kunengua mwili wake huko akiimba wimbo wa Tulwet *Emily Jepchumba*. Wimbo huu wa Tulwet ni wimbo wa kimapenzi unaomsifu mpenzi wake anayeitwa Emily Jepchumba. Mwimbaji Yegon alipokuwa akiuimba wimbo wake wa kumsifu *Ezekiel Kemboi* aliurejelea wimbo huo wa Tulwet *Emily Jepchumba* aliyekuwa akimsifu mpenzi wake Emily Jepchumba kuanzia mistari ya 32:

**MA**

- 27. Abwatin Ezekiel Kemboi
- 28. Eng kilabati eng South Korea
- 29. Kitar ilabati
- 30. Ibwat tiendo
- 31. Ak itien kole
- 32. Emily Jepchumba lakwani baa keiyo
- 33. Iamune mama eeh

**MP**

- Ninakumbuka Ezekiel Kemboi**
- Ulipokuwa ukikimbia huko Korea Kusini**
- Ulipomaliza kukimbia**
- Ukakumbuka wimbo**
- Na ukaimba hivi**
- Emily Jepchumba msichana kutoka Keiyo**
- Habari mama eeh**

34. Achamin Jepchumba  
35. Achamin sweety

**Ninakupenda Jepchumba**  
**Ninakupenda mpenzi**

Katika mistari hii, mwimbaji Yegon anasema kuwa mwanariadha huyu anayeitwa Ezekiel Kemboi, alipomaliza kukimbia huko Korea kusini alikumbuka wimbo wa kimapenzi wa Tulwet *Emily Jepchumba* na hivyo basi kuanza kuimba. Ni hapa ndipo Yegon aliuga wimbo wa Tulwet *Emily Jepchumba* kutoka mistari ya 1, 2, 3 na 4 kama inavyodhihirika hapa:

**MA**

1. Emily Jepchumba lakwani baa keiyo  
2. Iamune mama eeh  
3. Achamin Jepchumba  
4. Achamin sweety

**MP**

**Emily Jepchumba msichana kutoka Keiyo**  
**Habari mama eeh**  
**Ninakupenda Jepchumba**  
**Ninakupenda mpenzi**

Yegon anatuambia aliiga mistari hii kwa sababu mwanariadha Ezekiel Kemboi aliuimba wimbo wa Tulwet *Emily Jepchumba* kwa sababu bibi yake anaitwa Emily Jepchumba kama inavyobainika katika mistari ya 49:

**MA**

48. Ibaibaitu ooh kabisa amu  
49. Chepyoseng'ung kekure Emily Jepchumba

**MP**

**Una furaha ooh kwa sababu**  
**Bibi yako anaitwa Emily Jepchumba**

Aidha, mistari wa 50, 51, 52, 53 na 54 katika wimbo huu wa Yegon *Ezekiel Kemboi* umeigwa kutoka wimbo wa Tulwet *Emily Jepchumba*.

**MA**

50. Oolin ng'won ko Keiyo  
51. Oolin nyoo ko Bomet  
52. Loo missing Jepchumba  
53. Emily Jepchumba lakwani baa keiyo  
54. Iamune mama eeh

**MP**

**Kwenu ni huko Keiyo**  
**Kwetu ni huko Bomet**  
**Maeneo hayo ni mbali**  
**Emily Jepchumba msichana kutoka Keiyo**  
**Habari mama eeh**

Hapa, mistari hii imetwaliwa moja kwa moja kutoka wimbo wa Tulwet *Emily Jepchumba* katika mistari ya 5,6,7,8 na 9.

**MA**

5. Oolin ng'won ko Keiyo  
6. Oolin nyoo ko Bomet  
7. Loo missing Jepchumba  
8. Emily Jepchumba lakwani baa keiyo  
9. Iamune mama eeh

**MP**

**Kwenu ni huko Keiyo**  
**Kwetu ni huko Bomet**  
**Maeneo hayo ni mbali**  
**Emily Jepchumba msichana kutoka Keiyo**  
**Habari mama eeh**



Kutokana na mifano ambayo tumetoa hapo juu, imebainika kuwa Yegon amejitwalia wimbo wa Tulwet jinsi ulivyo. Huu ni upeo wa hali ya juu jinsi kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi kinavyotumika katika fasihi za kibaadausasa. Hii inadhihirisha kuwa kipengele hiki kimekubalika katika fasihi za kileo. Yegon ameiiga mistari kutoka wimbo wa Tulwet na kuiweka kwenye muktadha wa wimbo wake na hivyo basi kuboresha utunzi wake. Kama nilivyotanguliza hapo juu, Yegon aliuiga wimbo wa Tulwet kwa sababu bibi wa Ezekiel Kemboi anaitwa Emily Jepchumba. Kwa hivyo uigaji huu ulifaa wimbo wake kwani ulituonyesha mapenzi ya Ezekiel Kemboi (kwani alikuwa akiimba wimbo wa kumsifu yeye) kwa bibi yake Emily Jepchumba.

Fauka ya hayo, Yegon aliuiga wimbo wa Tulwet na kuufanyia marekebisho machache kama inavyobainika hapa katika mistari ya 74, 75 na 76.

**MA**

- 74. Mebwat kemboi
- 75. Kole kikemeten
- 76. Kimiten kebwtin

**MP**

- Usidhani Kemboi**
- Kwamba tumekuwacha**
- Tuko tunakukumbuka**

Mistari hii imeigwa kutoka wimbo wa Kipkemei Tulwet *Emily Jepchumba* katika mistari ya 13,14 na 15 kama inavyodhihirika hapa chini

**MA**

- 13. Mebwat Jepchumba
- 14. Lee kiameten
- 15. Amiten abwatin

**MP**

- Usidhani Jepchumba**
- Kwamba nimekuwacha**
- Niko ninakukumbuka**

Kama inavyoonekana, mabadiliko machache katika mistari hii yamefanywa. Katika mistari wa 13 jina la Jepchumba lilibadilishwa na Yegon kuwa Kemboi katika mistari wa 74. Madhumuni ya kufanya hivyo yalikuwa ni kutosheleza wimbo wake uliokuwa ukimsifu mwanariadha Ezekiel Kemboi. Vilevile katika mistari ya 14 na 15 Tulwet alikuwa ameuimba wimbo wake katika nafsi ya kwanza umoja. Hii ni kwa sababu wimbo

wake ulikuwa ni wa kumsifu mpenzi wake Emily Jepchumba. Yegon alibadilisha hayo na kuwa nafsi ya kwanza uwingi katika mistari ya 75 na 76. Hii ni kwa sababu wimbo wake ulikuwa ni wa kumsifu mwanariadha maarufu ambaye anajulikana na kila mtu. Wimbo wa Yegon unathibitisha sifa ya uigaji wa vipande vya simulizi kuwa lugha imekuwapo tangu kale na chochote tusemacho tayari kimeshasemwa kwa hivyo tunaiga tu. Hivyo basi Yegon aliuga wimbo wa Tulwet na, chambilecho Fairclough (1985), kuufanya uwe wake. Vilevile wimbo wa Yegon unathibitisha sifa ya kibaadausasa kuwa hawathamini mwandishi kama ilivyo wanausasa; na anaruhusiwa kunukuu au hata kuchukua kazi za wengine na kuufanya uwe wake. Ni vyema kutaja pia kuwa mtindo huu ulikuwa kwa manufaa kwa Yegon, kwani aliweza kubuni wimbo wake mpya na hivyo basi kuendeleza fasihi simulizi ya Kikalenjin.

Nyimbo za Kikalenjin za K21 kwa upande mkubwa zinazungumzia mapenzi. Nyimbo hizi ni za vijana chipukizi ambao wanasifu wapenzi wao. Kulingana na wanasayansi wa tabia, mapenzi ni kitovu kikuu cha maisha ya binadamu. Hii imewapelekea wanadamu kuwa na raghba sana kwa mambo ya mapenzi (Altemeyer 2009). Ni kutokana na madai hayo ndipo nyimbo za kimapenzi zinapendwa sana na hadhira lengwa. Hii imewapelekea waimbaji wa Kikalenjin kuimba kwa fujo nyimbo za kimapenzi ili kukidhi mahitaji ya hadhira lengwa. Utafiti huu uligundua kuwa waimbaji hawa chipukizi wanaigana wanapotunga na kuimba nyimbo zao za kimapenzi. Kwa mfano Felix Kimutai na Mike Rotich waliziimba nyimbo zilizo na mada sawia: *Merimella*. Nyimbo za waimbaji hawa zinasawiri sifa mbalimbali kuhusu huyu mpenzi wa kisanaa waliyempa jina, Merimella. Kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi kilibainika pale waimbaji hawa walipoimba nyimbo zao kwa kutumia mhusika mmoja, Merimella.

Kwa upande mkubwa waimbaji hawa wametusawiria jinsi mhusika huyu, Merimella, alivyovutia. Rotich anasawiri Merimella kama mhusika aliyeumbwa akaumbika, na hivyo basi kuwa wa kutamanika:

**MA**

1. Katara ntakikering weeh!
2. Kikuchabin ichabaksek

**MP**

**Natamani kukuona weeh!**  
**Uliumbwa ukaumbika**

Sawa na anavyoeleza Rotich, Kimutai naye ameelezea Merimella kama mpenzi anayependeza sana. Sura yake ni kama ya wazungu:

**MA**

13. Sura yako ni tamu Merimella weeh
14. Birirtangung kunaa baa chumbek

**MP**

**Unapendeza sana Merimella**  
**Sura yako ni kama ya wazungu**

Wazungu kwa muktadha huu wametumiwa kuashiria upeo wa hali ya juu ya msichana anayependeza. Nadhani sababu hasa ya Kimutai kusema hivyo ni kwa sababu ya rangi yake nyekundu. Rangi ambayo vijana wengi wa kisasa wanaona kama ishara ya urembo. Aidha, kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi kilibainika pale Kimutai na Rotich walipotumia mtindo wa kisengere nyuma kuwasilisha nyimbo zao. Kisengere nyuma ni mtindo unaotumiwa kusawiri mambo ambayo yalitendeka hapo awali kabla ya hadithi inayosimuliwa (Pinault 1992). Rotich anatumia mtindo huu kutuambia yale alikuwa ameyatenda na mpenzi wake Merimella hapo awali:

**MA**

7. Abwatii betut nekinye
8. Chekiambe chebikisoro
9. Akechezanii freefreetabo
10. Akechezani koraa

**MP**

**Nakumbuka siku ile**  
**Tukikula *Chebikisoro***  
**Tukicheza mwajificho**  
**Tukicheza mchezo wa anguti**

Katika mistari hii, Rotich anatumia mtindo huu wa kisengere nyuma kutuambia walikuwa na mpenzi wake Merimella wakila *Chebikisoro* na kucheza michezo ya mwajificho na anguti. *Chebikisoro* ni aina ya matunda yanayotundwa msituni. Kwa hivyo kuna uwezekano kuwa wapendwa hawa walikuwa wameenda msituni pamoja. Na wakiwa msituni walikuwa wakicheza michezo ya mwajificho na anguti. Mwajificho ni mchezo

wa kitoto wa kujificha na kutafutana huku anguti ni mchezo wa kurusha gololi kwa vidole. Fauka ya hayo, Rotich anatuambia kuwa akikumbuka siku hiyo wakiwa pamoja anahisi usingizi na kutokwa na machozi:

**MA**

- 23. Inyon weeh Merimella weeh!
- 24. Ngabwatin kochoni rwoandaa
- 42. Asie abwatin
- 43. Ngotosh kosai beek ab gon

**MP**

- Njoo wee Merimella weeh!**
- Nikikukumbuka ninahisi usingizi**
- Halafu nikukumbuke**
- machozi yanaweza kutiririka**

Katika mistari hii, Rotich anatuambia kuwa akimkumbuka wakiwa pamoja na Merimella, anahisi usingizi na kutokwa na machozi. Kuonyesha kwamba mambo ambayo waliyafanya awali yalikuwa yakukumbukika. Haya yanamfanya amsihi Merimella aje tena ili wawe pamoja kama hapo awali. Sawia na hayo, Kimutai anasema katika wimbo wake:

**MA**

- 9. Kung'ate 2008 Merimella weeh
- 10. kingemi keame mbonik
- 11. Kingemi kechezanii peplikan
- 12. Kingemi kechezanii readyreadytabo

**MP**

- Kuanzia 2008 Merimella weeh**
- Tukiwa tukikula *mbonik***
- Tukicheza mchezo wa kamba**
- Tukicheza mchezo wa sakamkewangu**

Kimutai, kama inavyodhihirika hapa, anatumia mtindo wa kisengere nyuma kutuambia yale yaliyotendeka mwaka wa awali wa 2008. Sawia na Rotich, Kimutai anatuambia kuwa walikuwa na mpenzi wake Merimella wakikula *mbonik* na kucheza michezo ya kamba na sakamkewangu. *Mbonik* ni aina ya matunda yanayotundwa msituni. Kwa hivyo kuna uwezekano kuwa wapendwa hawa walikuwa wameenda msituni pamoja. Na wakiwa msituni walikuwa wakicheza michezo ya kamba na sakamkewangu. Mchezo wa kamba ni mchezo wa kuzungusha kamba huku wakirukaruka juu yake. Mchezo wa sakamkewangu ni aina ya mchezo wa kitoto wa kujificha na kutafutana sawia na mwajificho lakini kwa namna tofauti. Vilevile Kimutai anatuambia akikumbuka wakiwa na Merimella anakosa kula au hata kufa:

**MA****MP**

17. Ngananin kumaamishi
18. Ngomechoni iwakchi Merimella weeh
19. Kibara kipkunyur itinyu

**Nikikukumbuka ninakosa kukula  
Haki ukuje tukae pamoja Merimella  
Nitakufa kwa kukukosa kukuona**

Hapa, Kimutai anatuambia kuwa akimkumbuka mpenzi wake Merimella hawezi kukula na hata anaweza kukufa. Kutuonyesha kuwa mambo ambayo aliyafanya na Merimella yalikuwa ya kukumbukika. Hii inamfanya amsihi mpenzi wake Merimella aje wakae pamoja sawia na jinsi Rotich alivyofanya. Waimbaji hawa Rotich na Kimutai wametusawiria mambo yaliyokuwa yamefanyika kwa kutumia mtindo wa kisengere nyuma. Pia kupitia mtindo huu waliweza kutunga nyimbo zao. Kama ilivyodhihirika mambo hayo yalifananana kwa upande mkubwa sana. Hii inabainisha kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi, chambilecho Fredric Jameson, kuwa uigaji wa vipande vya simulizi uhusisha matumizi ya mitindo sawa (1984).

Nyimbo za Kikalenjin za K21 ni mojawapo wa fasihi za kileo. Kwa mujibu wa Mriraria (2007) uwasilishwaji wa fasihi za kileo ni tofauti na fasihi za zamani zilizohitaji kuwepo na pande mbili za majadiliano yaani fanani na hadhira. Katika uwasilishwaji wa fasihi za kileo si lazima pande zote mbili ziwepo. Hadhira ya fasihi ya kileo inaweza iko mbali na fanani. Fasihi hii inawasilishwa kwa hadhira kupitia teknolojia: televisheni, kompyuta, mikanda ya video, mikanda ya CD, barua pepe, simu za mkononi na setelaiti. Kwa muktadha wa utafiti huu, hadhira ni mashabiki wanaosikiliza nyimbo za Kikalenjin. Waimbaji wa Kikalenjin huimba nyimbo zao ili kuburudisha mashabiki wao. Mashabiki hao hununua nyimbo hizi na hivyo basi kuwawezesha waimbaji kujikimu kimaisha. Kwa hivyo waimbaji wa Kikalenjin walibuni na kuimba nyimbo zinazohusu mashabiki wao kama njia mojawapo ya kujishirikisha nao. Ni kupitia uimbaji huu kuhusu mashabiki ndipo waimbaji waliigana nyimbo zao. Kwa mfano, waimbaji Robert Langat na Carlyne Chelagat waliigana kazi zao walipotumia mada sawa katika nyimbo zao: *Mashabiki*.

Uchanganuzi wa ndani unaonyesha kwamba nyimbo hizi zinaigana kwani zinazungumzia mambo sawa.

Kwanza, katika utangulizi, nyimbo hizi mbili za Langat na Chelagat zinawasalamia mashabiki wao. Langat anasema hivi katika mstari wa sita:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
6. Otach kakotiet anun mashabik tugul	<b>Mashabiki wote mpokee salamu</b>

Katika mstari huu, Langat anawasalamia mashabiki wake popote walipo. Mawazo sawia na hayo yanatolewa na Chelagat katika mstari wa 10:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
10. Akatii anee mashabik chemi olin tugul	<b>Ninawasalamia mashabiki wote kwa pamoja</b>

Chelagat katika mstari huu anawasalamia mashabiki wake sawia na Langat. Hata hivyo dhahirisho tosha linaloonyesha kuwa kulikuweco na uigaji baina ya nyimbo hizi mbili ni pale Langat na Chelagat walipowasalamia mashabiki wao, walioko sehemu sawia. Kwa mfano Chelagat anasema hivi katika mistari ya 9, 12 na 16:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
9. Akatii anee mashabik chemii Iten	<b>Ninawasalamia mashabiki wa Iten</b>
12. Eng oloo tugul oleomiten eng Baringo	<b>Mahala pote mlipo huko Baringo</b>
16. Unee mashabik chechuu eng Marakwet?	<b>Mashabiki yangu mnaendeleaje huko Marakwet?</b>

Katika mistari hii, Chelagat anawasalamia mashabiki walioko sehemu mahususi ya Iten, Baringo na Marakwet. Zaidi ya hayo hisia zake kwa mashabiki zake zinaonekana pale alipowajulia hali mashabiki walioko Marakwet (mstari 16). Ikumbukwe kwamba sehemu hizo ni baadhi ya makao wanamoishi Wakalenjin nchini Kenya. Iten ni sehemu kuu wanakoishi jamii ya Wakeiyo, Baringo jamii ya Watugen na Marakwet jamii ya Wamarakwet. (<http://dickinsg.intrasun.tcnj.edu/nations/kenya/kalenjin.html-07/06/2013>).

Langat naye anarejelea sehemu hizo hizo alizorejelea Chelagat katika wimbo wake:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
12. Otach kakotiet chemiten Iten	<b>Mpokee salamu mashabiki mlioko Iten</b>

13. Otach kakotiet chemiten Baringo	<b>Mpokee salamu mashabiki mlioko Baringo</b>
21. Amunee chemiten alin ba Eldoret	<b>Habari ya mashabiki walioko huko Eldoret</b>
22. Marakwet, Kapyego , Kipnai	<b>Marakwet, Kapyego na Kipnai</b>

Sawia na Chelagat, Langat anawasalamia mashabiki wake walioko sehemu mahususi ya Iten, Baringo na Marakwet. Isipokuwa Yegon anaongezea sehemu zaidi za Eldoret, Kapyego na Kipnai. Hata hivyo sehemu hizi zinafahamika kama makao ya jamii ya Wakalenjin. Kwa ujumla utumaji wa salamu kwa mashabiki wao hasa walioko sehemu sawa ni thibitisho tosha kuwa nyimbo za Langat na Chelagat zinadhihirisha kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi.

Fauka ya hayo, nyimbo za Yegon na Chelagat zilionyesha kuwa kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi pale ziliporejelea vituo vya redio vinavyotangaza kwa kutumia lugha ya Kikalenin. Vituo hivyo ni Kass FM na Changei FM. Kass FM na Changei FM ni vituo vya redio vinavyotangaza kwa lugha ya Kikalenjin. Vituo hivi vinatangazia jijini Nairobi. Chelagat katika wimbo wake anasema hivi katika mistari ya 17, 18 na 19:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
17. Kongoi kabisa eng shabik chechoo	<b>Asante sana kwa mashabiki wote</b>
18. Cheboo Changei ak Kass FM	<b>Mashabiki wa redio ya Changei na Kass FM</b>
19. Ketesiekchoo nemailotii chii	<b>Vituo vyetu vya redio visivyobagua</b>
20. Amue anee kongoi shabik chechoo	<b>Mimi ninasema asante kwa mashabiki wetu</b>

Katika mistari hii, Chelagat anasema kuwa anawashukuru mashabiki wa redio ya Kass FM na Changei FM. Vilevile mwimbaji huyu anataja kuwa vituo hivi vya redio havibagui. Mawazo kama haya yanaendelezwa na Langat katika wimbo wake katika mistari ya 29 na 30:

<b>MA</b>	<b>MP</b>
29. Changei FM amwai kongoi ak	<b>Ninawashukuru Changei FM na</b>
30. Mashabik tugul chebaa Kass FM	<b>mashabiki wote wa Kass FM</b>

Sawia na Chelagat, Langat anatoa shukrani kwa mashabiki na vituo vya redio vya Changei FM na Kass FM. Chelangat na Langat kutoa shukrani kwa mashabiki wao na

vituo vya redio kwa usawa unaonyesha kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21.

#### **4.3 HITIMISHO**

Katika sura hii tumedhihirisha upekee wa mhimili ya mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Tumeonyesha jinsi mhimili wa mwingiliano matini umejitokeza kupitia urejeleaji wa simulizi za jadi za Wakalenjin, methali, tasbihi, Bibilia na Katiba ya Kenya. Vilevile tumeonyesha jinsi nyimbo za Kikalenjin zinavyorejelea nyimbo nyingine. Katika kufanya hivyo tumeonyesha kuwa mwingiliano matini ni kitovu kikuu cha utunzaji na uwasilishwaji wa maana katika nyimbo za Kikalenjin. Aidha, tumebainisha kuwa mhimili wa uigaji wa vipande vya simulizi hudhihirika kupitia mistari, ploti na mitindo ya kisengere nyuma na utumaji wa salamu kwa mashabiki unaolingana kati ya nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Mtindo huu wa uigaji wa vipande vya simulizi uendeleza ubunaji wa nyimbo za Kikalenjin.





## SURA YA TANO

### MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.0 UTANGULIZI

Sura hii inaangazia muhtasari wa matokeo, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Azma ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza na kubainisha vipengele vya simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi katika nyimbo teule za Kikalenjin za K21. Utafiti ulifanywa kwa kutumia nyimbo ishirini na nne kutoka lahaja tano kuu za Kikalenjin: Kitugen, Kikeiyo, Kimarakwet, Kinandi na Kikipsigis. Mbinu zilizotumiwa katika ukusanyaji wa data ni utafiti maktabani iliyohusishwa usomaji wa nakala na vitabu mbalimbali vya nadharia ya ubaadausasa, data zilikusanywa kupitia unukuzi wa nyimbo zilizorekodiwa baada ya K21 hadi Agosti 2014 kutoka lahaja hizo tano. Nyimbo ambazo zilitumiwa katika utafiti huu ni zile zilizodhihirisha mitindo ya ubaadausasa kutoka lahaja hizo tano pekee. Tulitumia uchanganuzi kimaudhui katika uchunguzi wa mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo husika. Tulichanganua nyimbo hizo kwa mujibu wa mitindo minne ya ubaadausasa. Mitindo hii ambayo vilevile, ilitumika kama vigezo vya uchanganuzi ni: simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi. Matokeo ya utafiti yalijadiliwa katika sura ya tatu na nne.

#### 5.1 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti uligundua kwamba mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo za Kikalenjin za K21 zilizotumika ni simulizi ndogo ndogo, uchopekaji wa vipande vya simulizi, mwingiliano matini na uigaji wa vipande vya simulizi.

Kuhusu matumizi ya simulizi ndogo ndogo, nyimbo za Kikalenjin za K21 zilihusisha upingaji wa mamlaka makuu ya kijamii ambayo tangu jadi yamekuwa yakienziwa na

kuthaminiwa na wanajamii. Ni katika mamlaka hayo ambapo imani za simulizi kuu zinaendelezwa. Imani hizo zilikuwa zinakandamiza maisha ya binadamu na hivyo basi kupingwa na nyimbo za Kikalenjin za K21. Mamlaka hayo yaliyopingwa katika utafiti huu ni dini, taasisi za binadamu, elimu na kaida za kisiasa.

Kwa upande wa dini, tuligundua kuwa katika dunia ya kibaadausasa dini imekataliwa. Hii ni kwa sababu imani za dini kama maandiko matakatifu, maombi, ushuhuda, maungano, historia ya kanisa, mikutano ya kanisa na matini ya Bibilia zinatiliwa shaka. Dini ilisawiriwa kama kandamifu katika nyimbo za Kikalenjin za K21. Hii ilibainishwa pale mhubiri aliyekuwa akiaminiwa alipodhulumu wafuasi wake kwa kutoheshimu ndoa zao na kuitisha mikutano mingi na kusababisha mke na mume wasiwe na wasaa wa kuendesha mambo yao ya nyumbani. Dini pia imeonyeshwa kama isiyofaa kupitia waumini walio rahisi kudanganyika na wahubiri. Tuligundua pia kuwa katika nyimbo za Kikalenjin za kibaadausasa maombi na nguvu za roho mtakatifu hayaaminiki. Ili lilidhihirika pale maombi ya mhubiri yalipodhihakiwa.

Vilevile nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipinga matumizi ya taasisi za binadamu. Tuligundua kuwa taasisi za binadamu kama ndoa, familia, mifumo ya sheria, haki na jeshi, mashirika ya hospitali, mawasiliano na haki za binadamu haziaminiki katika dunia ya kibaadausasa. Ili ilibainika pale nyimbo za K21 zilipoonyesha wahusika wasioheshimu wazazi wao, wasiotaka kusoma shuleni, wanaokaidi tamaduni za jamii na wanaopinga asasi ya ndoa.

Fauka ya hayo tuligundua kuwa nyimbo za Kikalenjin za K21 zinapinga elimu. Elimu imedhihirishwa kusababisha kinyume na matarajio. Iisababisha umaskini, magonjwa kwa wazazi wanaofadhili elimu na ukosefu wa kazi kwa wasomi. Hii inapelekea elimu

kupingwa katika nyimbo za Kikalenjin za K21 na badala yake kupendekeza njia badalia kama binadamu kufuata talanta zake badala ya elimu.

Tuligundua vilevile kuwa kaida za kisiasa zilipingwa katika nyimbo za Kikalenjin za K21. Ili ilibainika pale nyimbo za Kikalenjin zilipoonyesha watu walioteseka katika msitu wa Mau, serikali ilipowafurusha. Ikumbukwe kwamba serikali iliwatoa raia katika msitu wa Mau kwa madhumuni ya kuhifadhi mazingira. Hata hivyo tekelezo hiyo ilileta mateso makubwa kwa wanadamu. Kwa hivyo nyimbo za Kikalenjin za K21 zinakataa kaida hizo na kupendekeza simulizi ndogo ndogo zinazoakisi hali halisi.

Matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi ulibainika pale nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipovunjwawunjwa na zisizomuwala hivyo basi kuakisi hali halisi ya dunia ya kisasa. Hii ni tofauti na mapendekezo ya akina Aristotle na Plato kuwa fasihi lazima iwe na mshikamano na muwala. Tuligundua kuwa nyimbo za Kikalenjin za K21 hudhihirisha kipengele hiki cha uchopekaji wa vipande vya simulizi kwa njia mbali mbali:

Kwanza, badala ya kuwa na hadithi moja iliyofululiza kuanzia mwanzo hadi mwisho, nyimbo za Kikalenjin za K21 husawiriwa kwa kutumia vijihadithi vingi visivyomuwala. Wakati mwingine nafasi wazi huwachwa baina ya vijihadithi hivi. Ni katika nafasi hizi zinazojalizwa kwa kutumia ishara mbalimbali za maneno ambazo wakati mwingine hazina uhusiano na wimbo wenyewe. Ilibainika kwamba mtindo huu ni mwafaka kwa kusawiri maisha ya kibaadausasa iliyojaa hadithi isiyokamilika kiusimulizi.

Tuligundua kuwa nyimbo za kibaadausasa wakati mwingine tangulizi zao huwa hazioani na wimbo wenyewe. Ilibainika kuwa mbinu hii humpa msikilizaji changamoto kufuatilia maudhui ya wimbo. Japo tulibaini kuwa ili msikilizaji aelewe wimbo ni sharti asikilize kwa umakinifu na kukubali kuzugwa pale inapobidi.

Tatu, Tuligundua kuwa nyimbo za Kikalenjin za ubaadausasa zinahusisha michanganyo ya vijitanzu. Tulibainisha utumaji wa salamu na mazungumzo ya simu kama vijitanzu vilivyotumiwa na waimbaji wa Kikalenjin. Tuligundua kwamba matumizi ya utumaji wa salamu uvuruga maudhui ya wimbo na mpangilio uliozoeleka na basi kuakisi dunia halisi tunayoishi leo. Dunia ambayo haina mpangilio wowote. Matumizi ya mazungumzo ya simu ilitumiwa ili kusawiri dunia ya ubaadausasa iliyo katika mbio ya matumizi ya teknolojia.

Vilevile katika kipengele hiki cha uchopekaji wa vipande vya simulizi, tulibaini kwamba huhusisha ugeukaji wa ploti uliozoeleka wa akina Plato na Aristotle. Tulibaini kuwa mtindo uliozoeleka wa kazi za fasihi kuwa na mwanzo, kati na mwisho unaomalizika kwa furaha uligeukwa pale nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipotumia majadiliano na mtindo wa tashtiti katika wasilisho zao. Fauka ya hayo tuligundua kwamba nyimbo za Kikalenjin za K21 hazina mahitimisho maalum na hazilengi kuhodhi ukweli kama zilivyo simulizi za jadi za akina Plato na Aristotle ambao wanazungumzia ngano kuu za wafalme kama kina Edipode.

Katika matumizi ya kipengele cha mwingiliano matini utafiti huu ulibaini kuwa nyimbo za Kikalenjin za K21 ziliimbwa kwa kuyarejelea matini ya awali. Kati ya matini hayo ya awali tuliyobaini ni pamoja na simulizi za jadi za Wakalenjin, methali, tasbihi, Bibilia, Katiba ya Kenya na urejeleaji wa nyimbo nyingine za awali.

Kwa upande wa urejeleaji wa simulizi za Kikalenjin, tuligundua kuwa simulizi za Kikalenjin ni nyenzo muhimu sana katika jamii ya Kikalenjin. Hii ni kwa sababu zinarithisha mila na desturi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hata hivyo ilibainika kuwa baadhi ya simulizi zilikuwa zimepitwa na wakati na zilitupiliwa mbali katika dunia

ya kibaadausasa. Hii ilidhihirika pale nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipopinga simulizi ya *Toyon beek, beek ap Kimaketit anan Kocheptibi (maji ni ya kila mtu na hayafai kuhodhiwa)*. Simulizi hii ilikuwa inasisitiza kuwa mwanaume anaweza kufanya mapenzi na mwanamke yeyote. Simulizi hii ilitupiliwa mbali kwa kuwa inaendeleza uasherati katika jamii na kusababisha usambazaji wa magonjwa ya zinaa kama UKIMWI.

Vilevile nyimbo za Kikalenjin za K21 zilidhihirisha kipengele cha mwingiliano matini ziliporejelea methali za jamii ya Kikalenjin. Ilibainika kuwa methali katika jamii ya Kikalenjin zilitumiwa na wazee kupitisha ujumbe kwa lugha ya mkato. Katika utafiti huu tuligundua kuwa nyimbo za Kikalenjin za K21 zilitumia methali *ak kwam chitugul maingenyi (na kila mtu ale asali iliyoko kwenye mzinga wake)* iliyo na maana kuwa kila mwanaume anafaa kuheshimu ndoa yake. Methali hii ilitumiwa kutatua changamoto za kijamii za kibaadausasa kama ukosefu wa uaminifu katika ndoa.

Fauka ya hayo, nyimbo za Kikalenjin zilirejelea methali za Waswahili. Methali za Waswahili hutumiwa kuwasilisha ujumbe mbalimbali kwa wanajamii. Nyimbo za Kikalenjin zilitumia methali ili kuwashauri wanajamii kuwa na mienendo mema katika jamii. Hii ilibainishwa pale nyimbo za Kikalenjin zilipotumia methali, *Usione wembamba wa reli gari moshi linapita*, kuwaonya wasichana wadogo kutokuwa na mahusiano ya kimapanzi na wazee wakubwa waliowazidi kiumri. Kwani mahusiano hayo yatawapelekea kudhulumiwa kimapanzi na kutumiwa kama vyombo vya burudani.

Nyimbo za Kikalenjin zilirejelea tashbihi. Tashbihi ni istilahi ambayo hutumiwa kufananisha vitu viwili au zaidi. Huhusisha matumizi ya maneno kama yafuatayo: vile, sawa, kama na mithili ya. Nyimbo za Kikalenjin ziliweza kurejelea tashbihi ili

kuwasilisha ujumbe zao. Katika utafiti huu, nyimbo za Kikalenjin zilitumia tashbihi: *ujanja kama sungura*, ili kutuonyesha jinsi wanawake walivyokuwa wajanja na wadanganyifu katika jamii.

Kipengele cha mwingiliano matini kilijitokeza pale nyimbo za Kikalenjin za K21 ziliporejelea Bibilia takatifu. Bibilia inaaminika iliandikwa hapo awali na watu walioelekezwa na Mungu. Ilibainika kuwa nyimbo za Kikalenjin za K21 zilirejelea Bibilia takatifu ziliporejelea vitabu vya Waamuzi, Hesabu na Wakorinto 1. Nyimbo za Kikalenjin za K21 zilirejelea Bibilia ili kutatua changamoto za dunia ya kibaadausasa. Hii ilidhihirika pale Bibilia ilipotumika kama nyenzo kuu ya kuwashauri watu kuwa na mienendo mizuri ili wasiambukizwe magonjwa ya zinaa kama UKIMWI.

Utafiti huu ulibaini kipengele cha mwingiliano matini pale nyimbo za Kikalenjin ziliporejelea katiba ya Kenya. Katiba ya Kenya ni kielelezo kinachotumiwa na serikali kuongoza nchi. Katika utafiti huu, nyimbo za Kikalenjin zilirejelea vifungu vya 26 na 39 katika sura ya nne ya Katiba. Kwa ujumla nyimbo ziliwahamasisha watu kuhusu haki za binadamu hasa haki ya kuishi na haki ya kuishi popote nchini Kenya.

Kipengele cha mwingiliano matini kilidhihirika pale nyimbo za Kikalenjin za K21 ziliporejelea nyimbo za awali. Tulibaini katika utafiti huu kuwa nyimbo za awali zilizokuwa zikisawiri eneo la Transmara kama pasipofaa na wanawake wanaotoka sehemu hiyo kama wasiopevuka, wajinga, wasiojua mitindo na mambo ya kisasa kwa haraka, wasiojua starehe, mafukara na waliokosa mwelekeo wa kimaisha zilirekebishwa. Urekebishaji huu ulifanywa pale nyimbo za baadaye zilipokataa usawiri huo hasi (kuhusu wanawake wa Transmara) na kisha kupendekeza kuwa wanawake wa Transmara ni wazuri na wamepevuka.

Kipengele cha mwingiliano matini kilijitokeza wakati ambapo nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipodenguana. Hii ilibainika wakati ambapo nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipoimbwa kuwahimiza wake kuwatunza waume wao. Nyimbo hizi zilidenguliwa na nyimbo zilizokuwa zinawahimiza waume kuwatunza wake wao. Ilibainika kuwa nyimbo hizi zilikuwa zinaingiliana kimaudhui na hivyo basi kusababisha kipengele cha mwingiliano matini.

Katika kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi tuligundua kuwa nyimbo za Kikalenjin za K21 zinaiga nyimbo zingine. Hii ilibainika pale nyimbo zilipokuwa na ploti, mistari, wahusika na mitindo ya kisengere nyuma na utumaji wa salamu ulioshabihiana. Kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi kilifanya nyimbo za Kikalenjin za K21 kuonekana kama zilizonukuliwa kutoka kazi za watu wengine.

Kwa upande wa ploti, uigaji wa vipande vya simulizi ulidhihirika katika nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipotumia ploti sawa. Tuligundua kuwa waimbaji wa Kikalenjin wa K21 walijenga nyimbo zao kwa njia ambayo ilitoa mfuatano na usababisho wa matendo yaliyofanana hivyo basi kuwa na ploti sawa. Matendo yaliyodhihirika katika utafiti: watu kufurushwa kutoka msitu wa Mau na serikali tawala ili kuhifadhi msitu huo, watu hawa walipofurushwa kutoka msitu wa Mau waliteseka sana na kupelekea waimbaji kutafuta suluhisho kutoka kwa viongozi wao. Ni matendo hayo yaliyosababisha nyimbo za Kikalenjin kuwa na ploti sawa na hivyo basi kudhihirisha kipengele hiki cha uigaji wa vipande vya simulizi.

Kwa upande wa matumizi ya mistari nyimbo za Kikalenjin za K21 zilidhihirisha uigaji wa vipande vya simulizi. Kipengele hiki kilidhihirika pale nyimbo zilipotumia mistari iliyosawa. Aidha, katika utafiti huu tulibainisha kuwa matumizi ya mistari sawa ilitokea



kwa sababu mbalimbali. Sababu ya kwanza ni pale wimbo unaporejelea wimbo wa awali na kunukuu moja kwa moja mistari na maneno yake. Hata hivyo tulibaini kuwa waimbaji wengine unukuu wimbo wa awali na kufanyia mabadiliko machache ili kukidhi mahitaji ya wimbo wake. Vilevile, katika utafiti huu tuligundua kuwa matumizi ya mistari na maneno sawa yalitokea wakati ambapo nyimbo ziliporejelea mahala sawa. Urejeleaji wa mahala sawa ulipelekea nyimbo husika kutumia mistari na maneno sawa.

Kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi kilibainika nyimbo teule ziliposawiri kuhusu mhusika moja. Katika utafiti huu waimbaji waliimba kuhusu mhusika aliyeitwa Merimella. Waimbaji hawa walisawiri sifa sawa za mhusika huyu Merimella kudhihirisha kuwa nyimbo teule ziliigana.

Katika utafiti huu tuligundua kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi kinatokea wakati ambapo sanaa inapotumia mtindo uliyosawa. Tulibaini kuwa mtindo uliyotumiwa katika nyimbo za Kikalenjin za K21 ni kisengere nyuma. Kisengere nyuma ni mtindo unaotumiwa kusawiri mambo ambayo yalitendeka hapo awali kabla ya hadithi inayosimuliwa. Nyimbo teule zilitumia kisengere nyuma kutuonyesha jinsi vijana walivyokuwa wakipendana kwa kucheza michezo ya kamba, mwajificho, anguti, sakamkewangu na huko wakitunda aina mbalimbali za matunda msituni.

Hatimaye, nyimbo teule za Kikalenjin zilidhihirisha kipengele cha uigaji wa vipande vya simulizi zilipokuwa na mada sawa ya *mashabiki*. Fauka ya hayo, waimbaji waliwasalamia mashabiki waliokuwa katika sehemu sawa za Iten, Baringo na Eldoret. Vilevile ilibainika kuwa matini ya nyimbo za Kikalenjin zilirejelea kwa usawa vituo vya redio vya Changei na Kass FM.

## **5.2. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

### **5.2.1 HITIMISHO LA UTAFITI**

Matumizi ya mitindo ya ubaadausasa katika nyimbo za Kikalenjin za K21 ni nyenzo kuu ya uwasilishwaji wa fasihi simulizi za Kikalenjin. Mitindo hii inasawiri hali halisi ya jamii ya kibaadausasa ya Kikalenjin jinsi inavyofasiriwa na wenyeji. Kipengele cha simulizi ndogo ndogo katika nyimbo za Kikalenjin kilitumika ili kupinga mamlaka kandamifu katika jamii: dini, elimu, taasisi za jamii na kaida za kisiasa. Upingaji huu umesababisha mitazamo tofauti ya kusuluhisha changamoto zinazokumba jamii ya kibaadausasa na basi hivyo kuboresha maisha yao. Matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi ulibainika pale nyimbo za Kikalenjin zilipovunjwawunjwa na zisizokuwa na uaushi wala muwala na basi hivyo kuakisi dunia ya kisasa, dunia iliyotata, iliyobutuka, iliyoparanganyika na iliyojaa uwingi tamaduni, hii inakaidi kaida za akina Aristotle na Plato waliokuwa wanaeleza fasihi kuwa lazima iwe na mshikamano na muwala. Mwingiliano matini umebainika pale nyimbo za Kikalenjin ziliporejelea matini ya awali: simulizi za jadi za Kikalenjin, methali, tasbihi, Bibilia, Katiba ya Kenya na nyimbo nyingine. Matini hayo ya awali yaliwezesha nyimbo za Kikalenjin kutungwa na hivyo basi kuwasilisha maana na ujumbe zao. Aidha, Uigaji wa vipande vya simulizi ulidhihirika pale nyimbo za Kikalenjin za K21 zilipotumia maneno, mistari, ploti na mitindo ya kisengere nyuma na utumaji wa salamu uliosawa. Kipengele hiki kiliendeleza ubunaji wa nyimbo za Kikalenjin.

### **5.2.2 MAPENDEKEZO YA UTAFITI**

- Utafiti ufanywe kuhusu mitindo ya ubaadausasa katika lahaja zingine za Kikalenjin, kwa mfano Kisabaot, Kipokot, Kiteriki na Kisebeei.

- Utafiti ufanywe wa mitindo mingine ya ubaadusasa katika nyimbo za Kikalenjin. Utafiti huu ulijifungia katika mitindo minne pekee. Kwa hivyo mitindo ya ubaadausasa kama kupotea kwa uhalisia na brikolojia inaweza kufanyiwa utafiti.
- Utafiti wa kina ufanywe kuhusu mitindo ya ubaadausasa katika tanzu zingine za jamii ya Kikalenjin kama hadithi, ngano, ushairi na vitendawili.
- Utafiti linganishi ufanywe kuhusu mitindo ya ubaadausasa ya jamii zingine nchini Kenya. Utafiti huu ulijifungia katika jamii ya Kikalenjin na kwa hivyo huwezi kuwakilisha mitindo ya ubaadausasa katika jamii zingine.

### **5.3. HITIMISHO LA SURA**

Sura hii imejadili kwa kina matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Tumebainisha waziwazi matokeo ya utafiti japo kwa muhtasari. Tumehitimisha utafiti huu kwa kudhihirisha kuwa mtindo ya ubaadausasa ni njia mwafaka wa kusawiri dunia ya kisasa. Aidha, tumetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

### **MAREJELEO**

- Albright, D. (2004). *Modernism and Music: An Anthology of Sources*. Chicago: University of Chicago Press.
- Altemeyer, B. (2009). *Sex and Youth*. Butterworth: Heinemann Publisher.
- Barret, T. (1997). Modernism and Postmodernism: an overview with art examples. *James Hutchens & Marianne Suggs, eds Washington, DC: NAEA, 1997*
- Barry, P. (2002). *Beginning theory: An introduction to literary and cultural theory*. Aberystwyth: Manchester University Press.
- Bernstein, J. (1992). 'Whistling in the Dark'. Katika: Barker F. et al (wahariri). *Postmodernism and re-reading of modernity*. Newyork: Manchester University press.

- Bertens, H. (1995). *The Idea of the Postmodernism*. Newyork: Routledge.
- Best, S. na Keller, D. (1991). *Postmodern Theory Critical Interrogations*. London: Routledge.
- Bertoncini, E. (2004). Mayai-Waziri wa Maradhi: Magic Realism in Euphrase Kezilahabi's Long Time Unpublished Short Story. *Swahili Forum, II* (39-44).
- Campbell, C. A. A. (1983). Nyimbo za Kiswahili: A Socio-Ethnomusicological Study of a Swahili Poetic Form. Tasnifu ya PhD (University of Washington).
- Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Harpenden: Pocket Essentials.
- Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi: Heinmann Kenya Limited.
- Childs na Fowler. (2006). *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. Newyork: Routledge.
- Fairclough, N.(1992). *Discourse and Social Change*. Cambridge: Polity Press. Kutoka (<http://en.wikipedia.org/wiki/Intertextuality> 2/10/2013 9.06a.m)
- ..... (1992). *Discourse and Social Change*. Cambridge: Polity Press.
- Diegner, L. (2005). Intertextuality in the Contemporary Swahili Novel: Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and Williame Mkufya's *Ziraili na Zirani*, *Swahili Forum* 18(211-244).
- Fairlamb, L. H. (1994). *Critical Conditions Postmodernity and the Question of Foundation*. Cambridge: Cambridge University press.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford: Clarendon.
- Foucault, M. (1974). *The Archaeology of Knowledge*. London: Tavistock: Kutoka (<http://users.aber.ac.uk/dgc/Documents/S4B/sem13.html#F> 02/10/2013)
- Gloag, K. (2012). *Cambridge Introductions to Music Postmodernism in Music*. Cambridge: Cambrigde University Press.
- Government of Kenya (2010), The Kenyan Constitution (2010). Nairobi: Government Printer.
- Graham, A. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge. Kutoka (<http://grammar.about.com/od/il/g/Intertextuality.htm> 2/10/2013 10.00a.m)

- Grant, I. H. (2001). 'Postmodernism and Science and Technology'. Katika: Sim S. (mhariri). *The Routledge Companion to Postmodernism*. London: Routledge.
- Gromov, D.M. (2008). Fasihi ya Kiswahili na Nadharia ya Fasihi. Katika: O. Ogechi, N.L. Shitemi na K.I. Simala (wahariri). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Hicks, S.R. (2004). *Explaining Postmodernism: Skepticism and Socialism from Rousseau to Foucault*. Arizona: Scholargy Publishing.
- Hutcheon, L. (1985). *A Poetics of Postmodernism: History, Theory, Fiction*. New York: Routledge.
- Kehinde, A. (2003), Intertextuality and the Contemporary African Novel. *Nordic Journal Of African Studies* 12(3): 372–386 (2003).
- Kipkorir, B. (1985). *People of Rift Valley Kalenjin*. London: Evans Brothers Limited.
- Kirumbi, P.S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shugwa ya Publishers Ltd.
- Klages, M. (1990). *Literary Theory: A Guide for the Perplexed*. Boulder: Routledge.
- Khamis, S.A.M. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na taaluma ya Kiswahili. Katika: O. Ogechi, N.L. Shitemi na K.I. Simala (wah.). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- ..... (2007). The Swahili Novelist at the Crossroad: The Dilemma of identity and Fecundity. *Swahili Forum*, 14:165-180.
- Kramer, J. D. (1996). *Postmodern Concepts of Musical Time*. New York: Routledge.
- Lee, S.H. (2009). Christianity and the Postmodern turn: a Critique of Postmodern Epistemology. *Tasnifu ya Uzamili*. (Haijachapishwa). South African Theological Seminary.
- Lewis, B. (2001). Postmodernism and Literature. Katika: Sim S. (mhariri). *The Routledge Companion to Postmodernism*. London: Routledge.
- McHale, B. (1992). *Constructing Postmodernism*. London: Routledge.
- Mukudi, E. (2004). Education for all: A framework for addressing the persisting illusion for the Kenyan context. *International Journal of Educational Development* 24 (231-240).
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mrikaria, S.E. (2009). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. *Swahili Forum* 14 (197-206).
- Mwamzandi, I, Y. (2013). Riwaya za Karne ya 21 na Udurusu wa Nadharia za Fasihi.

*Swahili Forum 20 (48-66).*

- Ndungo, C. M. & Wafula, R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi.
- North, D. C. (1990). *Institutions, Institutional Change and Economic Performance*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College: Rock Island.
- Plottel, P. na Charney, K. (1978). Introduction to Intertextuality: New Perspectives in Criticism. *New York Literary Forum, 1978: 143-157*.
- Pinault, D. (1992). *Story-Telling Techniques in the Arabian Nights*. New York: Brill Publishers.
- Ritgerotil, B.A. (2006). *Postmodernism and The Simpsons: Intertextuality, Hyperreality and Critique of Metanarratives*. London: Routledge.
- Rice, P. & Waugh, P. (2001). *Modern Literary Theory*. Newyork: Oxford University press.
- Scott, D. (2001). Postmodernism and Music. Katika: Sim S. (mhariri). *The Routledge Companion to Postmodernism*. London: Routledge.
- Simatei, P. (2010). Kalenjin popular music and the contestation of national space in Kenya, *Journal of Eastern African Studies, 4:3, 425-434, DOI:*
- Sim, S. (2001). *The Routledge Companion to Postmodernism*. London: Routledge.
- Suriano, M. (2007). Mimi Ni Msanii, Kioo Cha Jamii' Urban Youth Culture In Tanzania As Seen Through Bongo Flewa And Hip-Hop. *Swahili Forum 14 (2007): 207-223*.
- Tilak, R. (1993). *History and Principles of Literary Criticism*. New Delhi: Rama Educational Publishers.
- Thomas, N. (2006). *The Holy Bible: The Old and the New Testament*. Green Edition: National Publishing Company.
- Thonya, L. M. (1978). *Misingi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Black Star Agencies.
- Waliaula, W. K. (2010). Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha Kati ya Dunia Yao na The Tin Drum. *Swahili Forum, 17 (2010): 143-157*.

- Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications Limited.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishing Ltd.
- ..... (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishing Ltd.
- Wanyama, M.N. (2005). 'Ujumi Katika Muziki wa Kiafrika: Mfano wa Muziki wa Tohara ya Wabukusu'. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa).
- Wegesa, B. na Macharia, S. D. (2008). Postmodernism or Chaos? Theoretical Consideration in Reading New Directions in Some Cultural Practices in Kenya. Katika: N.O. Ogechi, N.L. Shitemi na K.I. Simala (wah.). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Winczewski, J.M. (2008). Consumption, Pastiche and Identity in Postmodern Visual Culture. University of Pretoria. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa).

**KIAMBATANISHO 1.****1. WIMBO: IBINI KUNUR****MTUNZI: MILLICENT JEROTICH  
MA**

1. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!
2. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!
3. Kiaro baba Faith Komasut chepkubet ak kamit ye,  
  
koko yaa ye amungwae, aibu kwisha!
4. Kiaro baba Faith Komasut chepkubet ak kamit ye,  
  
koko yaa ye amungwae, aibu kwisha!
5. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!
6. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, Mutya Mungu!
7. Iyaru koku konami fitina ak karu apwerit kutoit kebesho, aelewi rika!
8. Iyaru koku konami fitina ak karu apwerit kutoit kebesho, aelewi rika!
9. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange Mutya Mungu!
10. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!
11. Iyaru tiibik chailachi ngoriak cha nwaken, akole fashion funika uchi!
12. Iyaru tiibik chailachi ngoriak cha nwaken, akole fashion funika uchi!
13. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!
14. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!
15. Murenik kutuka, obakach ruando centre kerke  
  
ak kokai chesebe, mayai akili kwisha!
16. Murenik kutuka, obakach ruando centre kerke  
  
ak kokai chesebe, mayai akili kwisha!
17. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!
18. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!
19. Sikarun kelechet kionde TMM makitinye cha lee

**KIZAZI KITOVU****MP**

**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Nilimwona baba Faith akipigania jikoni na mamake nini hii, aibu kwisha!**  
**Nilimwona baba Faith akipigania jikoni na mamake nini hii, aibu kwisha!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, pole Mungu!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Utapata babu akifanya fitina hadi wake wa ndugu zake wanakosana bure, aelewi rika!**  
**Utapata babu akifanya fitina hadi wake wa ndugu zake wanakosana bure, aelewi rika!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, pole Mungu!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Wasichana wanavaa nguo fupi ati ni mtindo wa kisasa, funika uchi!**  
**Wasichana wanavaa nguo fupi ati ni mtindo wa kisasa, funika uchi!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Vijana pevuka, wacheni kwenda kulala mjini**  
**tabia hii ni sawa na kuku anayeangua mayai, akili kwisha!**  
**Vijana pevuka, wacheni kwenda kulala Mjini**  
**tabia hii ni sawa na kuku anayeangua mayai, akili kwisha!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya kiajabuajabu, Pole Mungu!**  
**Halafu tutaambiwa kuwa tumewapatia**



kwanyik ap Kalenjin, shows denied

20. Sikarun kelechet kionde TMM makitinye cha lee

kwanyik ap Kalenjin, shows denied

21. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!

22. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!

23. Iwendi iyori jito nee ngete asubuhi ak kuyee

maiye k kotomakungetke, bure kabisa!

24. Iwendi iyori jito nee ngete asubuhi ak kuyee

maiye k kotomakungetke, bure kabisa!

25. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!

26. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!

27. Iwendi town iyori koinange altaeke biika borwee kwai, aibu kwisha

28. Iwendi town iyori koinange altaeke biika borwee kwai, aibu kwisha

29. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange mutya Mungu!

30. Ibini kunur kuyebik tukuk nengero igwange, mutya Mungu!

31. Eeh! Wacha tu

32. Marakwet daughter

33. Akati makiche

34. Mautye Chemagel Sisters ak Cheronget

## 2. WIMBO: KIOMONGU SUBUI

### MTUNZI: CYRUS LANGAT

#### MA

1. Ooh! asaa Isimba aah kaa otkee
2. Meche siku tingwak, wee menyee Kabisimba
3. Che mekuruit kimagetit
4. Kiomongu subui koron, akakomot gitaiyu
5. Korir korityu, kole kakobet lakwenyu
6. Woo wee kiaseret anee
7. Ochameke Thomas Sosiotindet, Kabisimba
8. Kobirchi simit bamwai, kolechi konyo Chumba
9. Konyokutikang lakwek, kokakubakach sugul

10. Sikutachikee tianda, nataa kotalentainyu

11. Okass amwawak sikikchu

12. Motohaltee tukukwak

13. Kasarii makumii kasit

14. Rabishek chekemeche,

15. Matos Kegilchikee somanet

16. Mamikie naakasee engclass

17. Ibwoo bak seretet

**Dawa ya TMM (Tuliza Mzee Mkorofi)**  
wanawake wa Kalenjin hatuna hiyo  
dawa, tunakataa madai hayo

**Halafu tutaambiwa kuwa tumewapatia**  
**Dawa ya TMM (Tuliza Mzee Mkorofi)**  
wanawake wa Kalenjin hatuna hiyo  
dawa, tunakataa madai hayo

**Kizazi cha kisasa wanafanya mambo ya**  
**kiajabuajabu, Pole Mungu!**

